

**MSAMIATI MKOPO KATIKA KIKIPSIGIS: UCHANGANUZI WA  
KIMOFONEMIKI NA KIISIMUJAMII**

NA

CHERONO NAOMI JESCAH

TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI, IDARA YA KISWAHILI NA  
LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MOI

NOVEMBA 2018

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu Chochote kingine. Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini yangu na/au ya chuo kikuu cha Moi.

**Cherono Naomi Jescah**

.....

.....

SASS/PGK/04/13

Sahihi

Tarehe

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi

**Prof. Nathan Oyori Ogechi**

.....

.....

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika  
Chuo Kikuu cha Moi  
S.L.P. 3900  
ELDORET

Sahihi

Tarehe

**Munyua John Gichuki**

.....

.....

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika  
Chuo Kikuu cha Moi  
S.L.P. 3900  
ELDORET

Sahihi

Tarehe

**TABARUKU**

*Naitabaruku kazi hii kwa kwa wazazi wangu wapendwa: Baba; Josiah Koske, Mama; Jane Koske kwa malezi mema, kwa kunipa ari ya masomo tangu utotoni na kuyatia maisha yangu msingi thabiti na kwa msukumo wa kuikamilisha tasnifu hii.*

*Kwa mpenzi wangu Anthony Biwott , kwa kunitia moyo na kinipa kariha ili niikamilishe kazi.*

*Mwanangu mpendwa Caleb Kiprotich na mpwa wangu mpendwa Jesslyn Cheruto kwa hamasa maishani ya kutaka mjiendeleze na mfanikiwe kitaaluma.*

*Kwa dada zangu Daisy Ruth Chebet na MaryLinnet Chepkoech, Kaka zangu Moses John Kipyegon na Rodgers Isaac Keter.*

## IKISIRI

Kila lugha ni mfumo huru unaojitosheleza kisarufi. Ingawa hivyo, wasemaji wa lugha tofauti wanapotagusana kimawasiliano, lugha zao huweza kuathiriana kisarufi, na athari mojawapo huwa ni ukopaji wa msamiati. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu ulichunguza kanuni zinazofuatwa katika uingizwaji wa msamiati mkopo wa Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis. Ili kutimiza lengo hili, utafiti ulianza kwa kutambua na kuainisha msamiati mkopo katika nyanja za kisemantiki, na kisha kulinganisha mifumo ya kifonolojia ya lugha zote tatu ili kuweza kuelewa tukio la utohozi wa msamiati mkopo. Aidha, utafiti ulifafanua mabadiliko ya kimofonemiki yanayotokea katika msamiati mkopo unapoingizwa katika mfumo wa Kikipsigis na kisha kubainisha kategoria za kisarufi ili kutambua mofu za umoja na wingi. Vilevile, sababu za ukopaji zilichunguzwa. Data ya utafiti iliteuliwa kimakusudi ambapo vituo vitatu vya redio vinavyotangaza kwa Kikalenjin vilitumika katika kukusanya data: Chamegei FM, Kass FM na Kitwek FM. Data vilevile ilikusanywa kutoka kwa vitabu vilivyochapishwa kwa Kikalenjin. Data ilichanganuliwa kimakinifu kwa kuzingatia uchanganuzi wa kimaelezo ukiongozwa na nadharia ya fonolojia zalishi ya Clements na Keyser. Nadharia hii ni muhimu katika kufafanua fonolojia ya lugha kwa kuwa inajikita katika muundo wa silabi. Vilevile mawazo ya Myers-Scotton kuhusu ukopaji yaliongoza utafiti ili kubainisha vichocheo vya ukopaji. Utafiti ulitambua kuwa Kikipsigis hufupisha irabu ndefu katika msamiati mkopo. Vilevile, irabu unganifu husahilishwa ili zikubalike katika Kikipsigis. Kimsingi tulitambua kuwa Kikipsigis hutohoa irabu geni kwa kutumia irabu asili zinazokaribiana kimatamshi. Ilibainika pia kwamba Kikipsigis hakiruhusu mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Kwa hivyo, Kikipsigis hutohoa msamiati wa aina hii kwa kuchopeka irabu. Kuhusu ngeli za nomino, ilibainika kuwa irabu mzizi wa msamiati mkopo una irabu /u/ au /i/ mzizi huo huchukua mofu /inik/ katika wingi ilhali msamiati ulio na irabu /a/, /ɔ/ au /e/ huchukua mofu /isiek/ katika wingi. Katika kuchunguza vichocheo vya ukopaji, tasnifu ilibainisha kwamba Kikipsigis hukopa msamiati ili kurejelea dhana ngeni isiyokuwepo katika utamaduni wake. Hata hivyo, uchanganuzi ulionyesha kuwa Kikipsigis wakati mwingine hukopa msamiati hata kama kina njia ya kurejelea dhana fulani kwa mfano matumizi ya maelezo kurejelea dhana husika. Msamiati mkopo wa aina hii hupendelewa na wanaujozi lugha wa Kikipsigis, Kiswahili na Kiingereza.

## ABSTRACT

Every language is a system that is grammatically independent. Nevertheless, when speakers of different languages are in contact, their languages influence each other grammatically in different ways such as borrowing. Based on this, the present research examined the rules governing adaptation of loanwords in Kipsigis from Kiswahili and English. In a bid to fulfill this objective, the research identified and classified loanwords into semantic fields and then compared the phonological systems of the three languages in order to ease the understanding of loanwords adaptation process. The research analyzed morphophonemic changes that loanwords undergo during adaptation and went ahead to determine their grammatical categories whereby the singular and plural morphs were identified. The research further determined the sociolinguistic motivations for borrowing. Purposive sampling was used to sample three Kalenjin radio stations for data collection, namely Changei FM, Kass FM and Kitwek FM and also from a selection of published Kalenjin texts. Descriptive data analysis was done critically based on CV phonology theory by Clements & Keyser. This theory is very important in describing language phonology since it is syllable based. In addition, Myers-Scotton's theoretical claims on borrowing were crucial in determining motivations for borrowing. It has been established through this research that Kipsigis reduces long vowels in loanwords. English diphthongs are also simplified in order to be accepted in Kipsigis phonological system. The study noted that Kipsigis adopts new vowels by replacing them with native ones which are articulatorily closest to them. The research also found out that Kipsigis doesn't allow phoneme sequence cluster in the onset of words. It therefore adapts such words through insertion of vowels in between the consonants. On noun classes, the research found out that loanwords containing /u/ or /i/ vowels take the morph /inik/ in plural while those with /a/, /ɔ/ or /e/ take /isiek/. Concerning motivations for borrowing, this thesis noted that Kipsigis has borrowed words to refer to new concepts. However, the analysis showed that some words are borrowed even when Kipsigis has its own ways of referring to some words i.e using explanations. Bilinguals of Kipsigis, English and Kiswahili prefer using these borrowed words.

## YALIYOMO

IKIRARI .....	ii
TABARUKU .....	iii
IKISIRI .....	iv
ABSTRACT.....	v
YALIYOMO.....	vi
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xi
ORODHA YA MSAMIATI .....	xii
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xiii
SHUKRANI.....	xiv
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>MISINGI YA UTAFITI .....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala La Utafiti.....	2
1.2 Suala La Utafiti .....	4
1.3 Madhumuni Ya Utafiti.....	5
1.4 Maswali Ya Utafiti.....	5
1.5 Sababu Za Kuteua Mada.....	6
1.6 Upeo wa Utafiti.....	6
1.7 Umuhimu wa Utafiti .....	8
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	9
1.8.1 Dhana ya ukopaji.....	9
1.8.2 Mchakato wa ukopaji .....	12
1.8.3 Ukopaji na ujozi lugha .....	14
1.8.4 Ukopaji na ubadilishaji msimbo.....	15
1.9 Msingi wa Kinadharia.....	16
1.9.1 Nadharia ya fonolojia zalishi ya muundo wa konsonanti na irabu [KI].....	16
1.9.2 Nadharia ya lugha solo.....	20
1.10 Mbinu za Utafiti.....	22
1.10.1 Uteuzi wa sampuli.....	22
1.10.2 Ukusanyaji wa data .....	23
1.10.3 Vifaa vya kukusanya data .....	23
1.10.4. Uchanganuzi wa data .....	24

<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>25</b>
<b>MSAMIATI MKOPO WA KIINGEREZA NA KISWAHILI KATIKA KIKIPSIGIS .....</b>	<b>25</b>
2.0 Utangulizi.....	25
2.1 Utambuzi wa Msamiati Mkopo .....	25
2.2 Kategoria za Msamiati Mkopo katika Kikipsigis .....	39
2.3 Hitimisho.....	42
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>43</b>
<b>MIFUMO YA KIFONOLOJIA.....</b>	<b>43</b>
3.0 Utangulizi.....	43
3.1. Mfumo wa Fonimu katika Kikipsigis .....	43
3.1.1. Irabu katika Kikipsigis .....	44
3.1.2 Mfumo wa Konsonanti katika Kikipsigis .....	45
3.2 Mfumo wa Fonimu Katika Kiswahili .....	49
3.2.1 Irabu katika Kiswahili .....	49
3.2.2 Mfumo wa konsonanti katika Kiswahili .....	50
3.3 Mfumo wa fonimu katika Kiingereza .....	52
3.3.1 Irabu za Kiingereza .....	52
3.3.2 Mfumo wa Konsonanti katika Kiingereza .....	54
3.4 Miundo ya silabi katika lugha zote tatu .....	54
3.4.1 Miundo ya silabi katika Kikipsigis.....	55
3.4.2 Miundo ya silabi katika Kiswahili .....	59
3.4.3 Miundo ya silabi katika Kiingereza .....	62
3.5 Hitimisho.....	66
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>67</b>
<b>MABADILIKO YA KIMOFOFONEMIKI KATIKA MSAMIATI MKOPO WA KIKIPSIGIS .....</b>	<b>67</b>
4.0 Utangulizi.....	67
4.1 Utohozi wa Irabu za Kiingereza .....	67
4.1.1 Ufupishaji wa irabu ndefu .....	68
4.1.2 Usahilishaji wa irabu unganifu.....	69
4.1.3 Uyeyushaji.....	71
4.1.4 Muungano wa irabu.....	72
4.2 Utohozi wa Irabu za Kiswahili .....	73

4.2.1 Uchopezi wa irabu.....	73
4.2.2 Kuafikiana kwa irabu .....	75
4.2.3 Mvutano wa irabu.....	76
4.2.4 Udondoshaji wa irabu.....	77
4.2.5 Uyeyushaji.....	79
4.3 Utohozi wa konsonanti kutoka Kiingereza .....	79
4.3.1 Kuimarika kwa fonimu konsonanti .....	79
4.3.2 Kudhoofika kwa fonimu konsonanti .....	85
4.3.3 Udondoshaji wa sauti /h/ .....	88
4.4 Utohozi wa Konsonanti kutoka Kiswahili .....	88
4.4.1 Kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti.....	88
4.4.2 Kuimarika kwa konsonanti.....	89
4.4.3 Kudhoofika kwa fonimu .....	95
4.4.4 Uchopezi wa konsonanti .....	98
4.4.5 Udondoshaji wa konsonanti .....	99
4.5 Ongezeko la Silabi katika Msamiati Mkofo.....	102
4.5.1 Usilabishaji kupitia uchopezi wa irabu .....	102
4.5.2 Usilabishaji kupitia uchopezi wa konsonanti .....	104
4.6 Kategoria za Kisarufi za Msamiati Mkofo.....	106
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>113</b>
<b>SABABU ZA KIISIMUJAMII ZINAZOCHANGIA UINGIZWAJI WA</b>	
<b>MSAMIATI MKOFO KATIKA KIKIPSIGIS.....</b>	<b>113</b>
5.0 Utangulizi.....	113
5.1 Ukopaji wa Kiutamaduni .....	116
5.1.1 Uwanja wa sayansi na teknolojia .....	116
5.1.2 Uwanja wa afya na matibabu .....	117
5.1.3 Uwanja wa elimu.....	117
5.1.4 Uwanja wa vifaa vya nyumbani .....	119
5.1.5 Uwanja wa siasa .....	120
5.1.6 Uwanja wa dini.....	121
5.1.7 Uwanja wa uchumi na biashara.....	122
5.1.8 Uwanja wa ajira/ kazi .....	123
5.1.9 Uwanja wa vyakula na vinywaji .....	124
5.1.10 Uwanja wa kilimo .....	125



5.1.11 Uwanja wa mavazi .....	126
5.1.12 Uwanja wa usafiri na miundo misingi.....	127
5.1.13 Uwanja wa michezo .....	128
5.2 Ukopaji wa Kimtindo.....	129
5.2.1 Uwanja wa vifaa vya kinyumbani.....	129
5.2.2 Uwanja wa siasa.....	130
5.2.3 Uwanja wa mavazi .....	131
5.3 Ukopaji wa Msamiati Kukidhi Haja ya Kutumia Msamiati Mahususi.....	131
5.3.1 Uwanja wa kidini .....	131
5.3.2 Uwanja wa vyakula na vinywaji .....	132
5.3.3 Uwanja wa msamiati wa kijumla .....	132
5.4 Ukopaji wa Msamiati ili Kuondoa Utata wa Kimaana .....	133
5.4.1 Uwanja wa afya na matibabu .....	133
5.4.2 Uwanja wa mavazi .....	133
5.4.3 Uwanja wa msamiati wa kijumla .....	133
5.5 Ukopaji wa Msamiati ili Kurahisisha Mawasiliano.....	134
5.5.1 Uwanja wa uchumi na biashara.....	134
5.6 Ukopaji wa Kidaraja .....	135
5.6.1 Uwanja wa sayansi na teknolojia .....	135
5.6.2 Uwanja wa elimu.....	136
5.6.3 Uwanja wa uchumi na biashara.....	136
5.6.4 Uwanja wa ajira/ kazi.....	136
5.6.5 Uwanja wa usafiri na miundo misingi.....	137
5.6.6 Uwanja wa michezo .....	137
5.7 Hitimisho.....	137
<b>SURA YA SITA.....</b>	<b>139</b>
<b>MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>139</b>
6.0. Utangulizi.....	139
6.1. Matokeo .....	139
6.2. Hitimisho.....	142
6.3. Mapendekezo .....	143
MAREJELEO .....	144
VIAMBATISHO.....	147
Kiambatisho I: Barua .....	147

Kiambatisho II: Hojaji..... 148

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1.1: Msamiati wa Siasa .....	26
Jedwali 2.1.2: Msamiati wa Sayansi/Teknolojia.....	28
Jedwali 2.1.3: Msamiati wa Kielimu .....	29
Jedwali 2.1.4: Msamiati kuhusu ajira .....	30
Jedwali 2.1.5: Msamiati wa kidini .....	31
Jedwali 2.1.6: Msamiati wa tiba na masuala ya afya.....	32
Jedwali 2.1.7: Msamiati wa michezo .....	33
Jedwali 2.1.8: Msamiati wa Kilimo .....	34
Jedwali 2.1.9: Msamiati wa usafiri .....	35
Jedwali 2.1.10: Msamiati wa mavazi .....	36
Jedwali 2.1.11: Msamiati wa vyakula.....	37
Jedwali. 2.2.1: Aina za maneno .....	39
Jedwali 3: Mfumo wa irabu za Kikipsigis kwa mujibu wa Toweett.....	44
Jedwali 4: Mfumo wa irabu za Kikipsigis kwa mujibu wa Sang na Jerono .....	44
Jedwali 5: Mifano ya maneno ya irabu za Kikipsigis .....	45
Jedwali 6: Mfumo wa Konsonanti katika Kikipsigis.....	46
Jedwali 7: Konsonanti za Kikipsigis.....	49
Jedwali 8: Mfumo wa irabu katika Kiswahili .....	50
Jedwali 9: Mfumo wa konsonanti katika Kiswahili.....	51
Jedwali 10: Mfumo wa irabu katika Kiingereza .....	52
Jedwali 11: Mfumo wa irabu unganifu katika Kiingereza.....	52
Jedwali 12: Maneno yaliyo na irabu unganifu katika Kiingereza.....	53
Jedwali 13:Mfumo wa irabu katika Kiingereza .....	54

**ORODHA YA MSAMIATI**

<i>Irabu tatu-unganifu</i>	triphthongs
<i>Irabu unganifu</i>	diphthongs
<i>Lugha bebwa</i>	lending language
<i>Lugha solo</i>	borrowing language
<i>Maingilio</i>	interference
<i>Msamati wa Kuhamisha</i>	loanshift
<i>Tafsiri -mkopo</i>	loan translation
<i>Uhuluti</i>	loanblends
<i>Ukopaji wa kimtindo</i>	core borrowing
<i>Ukopaji wa kiutamaduni</i>	cultural borrowing

**ORODHA YA VIFUPISHO**

- FZ - Fonolojia Zalishi  
I - Irabu  
K - Konsonanti  
KI - Konsonanti Irabu

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu kwa neema zake na kwa kunipa uwezo na kuniongoza masomoni hadi kufika kiwango hiki.

Natoa shukurani kwa wasimamizi wangu Prof. Nathan Oyori Ogechi na John Gichuki Munyua kwa nasaha na kunihimiza kuandaa tasnifu hii. Natoa shukurani pia kwa mkuu wa idara Dkt. Mark Kandagor kwa msukumo wa kuikamilisha kazi hii. Vilevile nawashukuru wahadhiri katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunipa ushauri katika utafiti wangu na kwa kunielimisha katika kozi mbalimbali.

Shukurani tele ziwaendee wazazi wangu kwa kunihimiza, kunipa msaada wa kifedha na kwa maombi yao ya kila mara ili niweze kujimudu maishani. Kwa mpenzi wangu, mwanetu na mpwa wetu nawashukuru kwa kunitia moyo wakati wote, asanteni sana. Kwa ndugu zangu nawashukuru na kuwaombea mfanikiwe maishani.

Namshukuru pia Bw. Magugu Vincent kwa kuihariri kazi yangu. Nakutakia ufanisi katika shahada yako ya uzamifu. Nawashukuru pia wazamili wenzangu ambao tumeshirikiana, kutiana moyo na kuelekezana katika kufanya tafiti zetu mbalimbali.

Mwisho natoa shukurani kwa wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine na kwa wale walionipa mawaidha yaliyochangia ufanisi wa tasnifu hii.

## **SURA YA KWANZA**

### **MISINGI YA UTAFITI**

#### **1.0 Utangulizi**

Sura hii imetoa maelezo kuhusu misingi ya utafiti na uchanganuzi wa data. Sura yenyewe imegawika katika sehemu kumi ambapo sehemu ya kwanza inaelezea kuhusu usuli wa suala la utafiti unaojikita katika kuchunguza msamiati mkopo wa Kikipsigis kwa kuzingatia mielekeo ya kimofonemiki na kiisimujamii. Sehemu hii pia ilitalii lugha ya Kikipsigis ambayo ni lahaja ya Kikalenjin. Sehemu ya pili inatoa ufafanuzi kuhusu suala la utafiti huu kwa kina. Sehemu ya tatu inabainisha madhumuni ya utafiti huku maswali ya utafiti yakibainishwa katika sehemu ya nne. Sehemu hii inafuatiwa na sababu za uteuzi wa mada zilizobainisha kwamba utafiti ulihamasishwa na ari ya kutaka kufahamu na kuweka wazi fonolojia ya usilabishaji wa msamiati mkopo kwa upande mmoja na katika upande wa pili sababu za kiisimujamii zinazoongoza tukio la ukopaji wa msamiati. Katika sehemu ya sita, upeo wa utafiti ubainishwa ili kuweka wazi mipaka ya utafiti huu. Katika sehemu ya saba tulijadili umuhimu wa utafiti huu haswa katika taaluma ya fonolojia, mofolojia na isimujamii jinsi inavyobainika katika madhumuni ya utafiti. Sehemu hii ilifuatiwa na mihimili ya kinadharia pamoja na mawazo ya kitaaluma yaliyoongoza utafiti huu. Sehemu ya tisa iliangazia maoni ya wataalamu mbalimbali waliofanya utafiti katika uwanja huu. Sehemu ya mwisho ilibainisha mbinu zilizotumika katika utafiti huu kwa kuonyesha namna sampuli ilivyoteuliwa, vifaa vilivyotumika katika ukusanyaji wa data, jinsi data ilivyokusanywa na kubainisha namna data ilivyochanganuliwa.

### 1.1 Usuli wa Suala La Utafiti

Suala la ukopaji wa msamiati kutoka lugha moja hadi lugha nyingine limeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali na hivyo kuonekana kuwa suala linaloathiri lugha karibu zote ulimwenguni. Bynon (1977) anafafanua dhana ya ukopaji kama uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine. Nao Crystal (1997) na Myers-Scotton (2006) wanaeleza kuwa ukopaji ni uingizaji wa msamiati au kipengele cha kiisimu katika lugha moja kutoka lahaja au lugha nyingine. Kwa hivyo, ukopaji ni mchakato unaosababisha neno la kigeni kuingizwa katika lugha. Hali hii hutokana na sababu mbalimbali kwa mfano, mitagusano kati ya wasemaji wa lugha mbili au zaidi (Mbaabu, 1985:33). Huenda hali hii hutokea kwa kuwa lugha zozote zinapoingiliana katika muktadha wa mawasiliano kuna uwezekano wa kupokezana msamiati ili kuwezesha utekelezaji wa mahitaji ya kimawasiliano. Hivyo basi ukopaji wa msamiati kutoka lugha moja hadi nyingine ni jambo lisiloepukika katika lugha mbalimbali ulimwenguni ikiwemo Kiswahili, Kiingereza na lugha za kiasia kama vile Kikalenjin.

Kikalenjin ni lugha ya kinailotiki inayozungumzwa nchini Kenya, Uganda Mashariki (Sebei) na Kaskazini mwa Tanzania (Dagota) (Sang & Jerono, 2012). Kikalenjin kina lahaja kumi ambazo ni Kipsigis, Nandi, Tugen, Keiyo, Marakwet, Sabaot, Pokot, Terik, Seng'wer na Okiek (Seroney, 2009). Kati ya lahaja hizi, Kipsigis ndiyo iliyo na wasemaji wengi (Sambu, 2007). Wasemaji wa lugha hii walianza kutagusana na Waingereza katika karne ya 18. Kufikia karne ya 19 mitagusano yao iliendelezwa na majilio ya wamishenari waliofika Afrika kueneza dini ya kikristo na pia walowezi kutoka Uingereza ambao walizungumza Kiingereza na baadaye kujifunza lugha za wenyeji ikiwemo Kiswahili (Sang & Jerono, 2012). Kwa hivyo, wamishenari na walowezi walitagusana na Wakipsigis kupitia matumizi ya Kiswahili.



Kutokana na maelezo ya wataalamu tuliokwisha wataja hapo juu, ni wazi kuwa lugha tofauti zinapotagusana kwa njia moja au nyingine, hazina budi kukopa msamiati kutoka lugha nyingine.

Nchini Kenya, Kiingereza kiliteuliwa kuwa lugha rasmi nacho Kiswahili kuwa lugha ya taifa na baadaye lugha rasmi (RoK, 2010). Kwa hivyo, lugha hizi zimepewa hadhi ya juu katika jamii na huenda hali hii imesababisha lugha ya Kikipsigis kukopa msamiati kutoka lugha hizi (Kiswahili na Kiingereza).

Msamati mkopo hautumiki tu katika maandishi bali pia katika lugha semwa kwa mfano katika vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na hata kwenye mtandao. Kuna vituo mbalimbali vya redio na televisheni vinavyotangaza katika Kikipsigis kama vile, Kass Tv, Changei Fm, Kass Fm, Kitwek Fm na Radio Injili.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu msamiati mkopo na baadhi ya tafiti hizo tangulizi, zimejikita katika kuchunguza fonolojia ya msamiati mkopo katika lugha za Kiafrika. Oduma (2006) kwa mfano, alichunguza mabadiliko ya kifonolojia katika msamiati mkopo wa Kiingereza na Kiswahili katika Kiteso, Wamalwa (1997) alichunguza usharabu wa msamiati wa Kiswahili katika Kibukusu. Utafiti huu ni tofauti na tafiti tangulizi kwa kuwa umechunguza namna msamiati uliokopwa kutoka lugha ya Kiingereza na Kiswahili hutoholewa katika Kikipsigis kwa kuzingatia mabadiliko ya kimofonemiki na pia kuchunguza sababu za kiisimujamii zinazochangia hali hii. Utohozi kama mchakato wa kiisimu ulichunguzwa kwa kuzingatia mitazamo miwili. Kwanza, kwa kuupambanua kama utaratibu wa kusharabu msamiati kutoka kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na kuingiza katika mfumo wa Kikipsigis kupitia mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia. Pili, tulichunguza sababu za kiisimujamii zinazochangia mchakato wa ukopaji. Kadiri

tujuavyo, utafiti wa aina hii haujafanyika katika taaluma ya Kiswahili. Utafiti huu ulifuata mkondo wa tafiti za mtagusano wa lugha zinazotumia mielekeo-mseto katika uchanganuzi wa data ambapo mbinu za uchanganuzi za isimu fafanuzi hususan mofofonemiki zilichangiwa na zile za isimujamii (Myers-Scotton na Jake, 2000, Myers-Scotton, 2002).

Odhiambo na Oduma (2011), wanaeleza kuwa ni lazima kila lugha inayokopa msamiati kutohoa msamiati huo mkopo katika mfumo asilia wa kifonolojia wa lugha husika. Katika utafiti huu basi tunajiuliza: Je, Kikipsigis kinapokopa msamiati kunatokea utohozi kila wakati? Iwapo ndio, ni kanuni zipi za kimofofonemiki zinazoweza kutumika katika ufafanuzi wa msamiati huo? Je, maneno hayo yaliyokopwa hutokea katika kategoria gani za maneno na za kisarufi? Ni kwa nini Kikipsigis kikope msamiati kutokana na lugha hizi mbili?

## **1.2 Suala La Utafiti**

Kila lugha ni mfumo huru unaojitosheleza kisarufi. Ni kwa sababu hiyo ambapo kila lugha huweza kuchunguzwa muundo wake pasi na kurejelea lugha yoyote nyingine, ama mtu akaweza kuishi maisha yake yote bila ya kuijua lugha yoyote nyingine isipokuwa lugha yake ya mama. Ingawa hivyo, wasemaji wa lugha tofauti wanapotagusana kimawasiliano, lugha zao huweza kuathiriana kisarufi. Athari mojawapo huwa ni ukopaji wa msamiati. Msamiati unaoingizwa katika lugha moja kutoka kwa lugha geni si lazima ufahamike asili yake kwa wengi wa wasemaji kwa kuwa mara nyingi unatoholewa ili kuafikiana na msamiati asili. Utafiti huu ulichunguza mbinu zitumikazo wakati Kikipsigis kinakopa msamiati kutoka kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Hivyo basi, utafiti ulilenga kupambanua michakato ya kimofofonemiki inayotumika katika utohozi wa msamiati husika na

sababu za kiisimujamii zinazochangia kuingizwa kwa msamiati wenye asili hizo katika dafina ya msamiati wa Kikipsigis. Katika michakato ya kimofonemiki tulizingatia fonimu na miundo ya silabi katika maneno yaliyotoholewa ili kubainisha iwapo yalifuata miundo ya maneno kama ilivyo katika maneno asili ya Kikipsigis. Kiisimujamii tulidadisi hali ambazo zilichochea uingizwaji wa msamiati mkopo katika Kikipsigis.

### **1.3 Madhumuni Ya Utafiti**

Utafiti huu ulilega kuchunguza utohozi wa msamiati mkopo katika Kikipsigis kwa kutumia mtazamo mseto wa Kiisimu fafanuzi na Kiisimujamii. Ili kulitimiza lengo hili, madhumuni yafuatayo yalizingatiwa:

- a) Kutambua na kuainisha msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis.
- b) Kulinganisha mifumo ya kifonolojia ya lugha zote tatu ili kuweza kuelewa tukio la utohozi wa msamiati mkopo.
- c) Kufafanua mabadiliko ya kimofonemiki yanayotokea katika msamiati mkopo unapoingizwa katika mfumo wa Kikipsigis.
- d) Kubainisha sababu za kiisimu-jamii zinazosababisha uingizwaji wa msamiati mkopo katika Kikipsigis.

### **1.4 Maswali Ya Utafiti**

Ili kuyafikia madhumuni ya utafiti huu, maswali yafuatayo yalituongoza:

- a) Je, msamiati unaokopwa hutokea kwenye kategoria gani za kisarufi katika Kikipsigis?
- b) Je, kunatokea mabadiliko yepi ya kimatamshi (kifonolojia) na kimaumbo (kimofolojia) katika msamiati mkopo wa Kikipsigis?

- c) Je, msamiati mkopo katika Kikipsigis unawakilisha dhana zisizo asili katika utamaduni wa Wakipsigis?

### **1.5 Sababu Za Kuteua Mada**

Uteuzi wa mada ya utafiti huu ulihamasishwa na ari yetu ya kutaka kufahamu na kuweka wazi fonolojia ya usilabishaji wa msamiati mkopo kwa upande mmoja na katika upande wa pili sababu za kiisimujamii zinazoongoza tukio la ukopaji wa msamiati katika Kikipsigis. Katika kuichunguza mada hii tulilenga kuimarika kitaaluma katika taaluma za fonolojia, mofolojia na isimujamii. Vilevile, kadri tujuavyo kufikia sasa hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu mabadiliko ya kimofofonemiki katika msamiati wa Kiswahili na Kiingereza unapoingizwa katika Kikipsigis na kwa hivyo, utafiti huu utaziba pengo hili.

### **1.6 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza uliotoholewa katika Kikipsigis. Hata ingawa Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka lugha nyinginezo za Kibantu na Kinailotiki kama vile Kikuyu, Ekegusii na Dholuo, utafiti huu ulijikita katika msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza pekee. Hii ni kwa sababu lugha hizi mbili ni rasmi na hutumika katika kufundisha shuleni.

Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulibainisha kuwa kuna msamiati uliokopwa katika Kikipsigis kutoka Kiswahili au Kiingereza, ulio na asili yake katika lugha nyingine kwa mfano; neno meza katika Kiswahili lina asili katika Kireno *nesso*, limekopwa kama *meset* katika Kikipsigis. Utafiti huu hata hivyo haukujihusisha na asili ya msamiati mkopo katika Kiingereza na Kiswahili ili kuepuka matatizo ya

kietimolojia. Kwa hivyo tulitumia msamiati jinsi ulivyokopwa kutoka kwa Kiingereza na Kiswahili bila kuzingatia asili ya msamiati husika.

Data ya utafiti huu ilikusanywa kwenye vituo vitatu vya redio vinavyotangaza kwa Kikalenjin vilivyoteuliwa kimakusudi kwa kuwa ni maarufu na husikika katika maeneo mengi mnamozungumzwa lugha hii. Ingawa kuna vyombo vingine vya habari kama vile televisheni na magazeti, utafiti huu ulijikita tu katika vituo vya redio kwa kuwa watu wengi wanamiliki na kutumia redio kuliko vyombo hivyo vingine. Ogechi (2011) anaeleza kuwa kwa muda mrefu sana redio imekuwa chombo cha pekee cha habari kilichotumiwa na binadamu. Tofauti na vyombo vingine vinavyohitaji umeme (televisheni), au gharama ya kununua kila siku (magazeti), redio huweza kutumia betri ambazo hupatikana kwa urahisi hata katika sehemu za mashambani ambazo hazina umeme. Vituo hivyo vya redio ni Changei Fm, Kass Fm na Kitwek Fm. Katika vituo hivi vya redio tulikusanya data katika matangazo ya biashara, vifo, michezo na katika taarifa za habari zinazosomwa katika vituo hivyo pasi na kuzingatia ripoti za nyanjani. Hii ni kwa sababu ripoti za nyanjani huhusisha matumizi ya lahaja mbalimbali kwa kutegemea eneo linahusika na ripoti inayotolewa. Vile vile data ilikusanywa kutoka kwa vitabu vya kidini vilivyoandikwa kwa Kikalenjin kama vile Bibilia, TKK, vitabu vya nyimbo na mafunzo vya kidini.

Data ilikusanywa kwa muda wa miezi minne; Oktoba, Novemba, Disemba 2014 na January 2015, ili kutuwezesha kukusanya data nyingi kwa ajili ya suala la utafiti. Kimsingi, utafiti huu ulijikita katika mabadiliko ya kimofonemiki katika utohozi wa msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza hadi Kikipsigis na wala haukuvuka mipaka hiyo. Kiisimujamii tulijihusisha na mtagusano baina ya Kiswahili, Kiingereza na Kikipsigis kihistoria ili kubaini sababu zinazoweza kuelezea kwa nini msamiati husika ukapata kuingizwa katika Kikipsigis.

Katika utambuzi na uainishaji wa data ilibainika kwamba Kikipsigis kimekopa aina mbalimbali za maneno kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na viunganishi. Utafiti huu ulijikita katika utohozi wa nomino pekee.

### **1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Halliday (1998) anaeleza kuwa kipengele chochote kinachohusu msamiati kinastahili kufanyiwa utafiti kwa kuwa ni sehemu muhimu mno katika sarufi ya lugha. Kwa hivyo, utafiti huu ni muhimu katika taaluma ya fonolojia na mofolojia hasa kuhusiana na fonolojia ya msamiati mkopo kwani ulituwezesha kubaini michakato ya kimofonemiki katika utohozi wa msamiati mkopo katika Kikipsigis. Isitoshe, utafiti huu ulibainisha mabadiliko yanayotokea katika msamiati mkopo wa Kiswahili na Kiingereza unapoingizwa katika Kikipsigis.

Aidha, utafiti huu umetoa mchango mkubwa katika taaluma ya isimujamii kwa kubainisha motisha za ukopaji wa msamiati. Katika tafiti nyingi zilizofanywa hapo awali, watafiti wameshughulikia tu mabadiliko ya kifonolojia ya msamiati mkopo katika lugha pokezi bila kuonyesha sababu zinazoishurutisha lugha kukopa msamiati. Hivyo basi utafiti huu ni muhimu kwani ulipiga hatua zaidi ya kubainisha sababu za kiisimujamii za uingizwaji wa msamiati mkopo na kuangazia sio tu mabadiliko ya kifonolojia, bali kimofonemiki katika msamiati mkopo.

Mchakato wa utohozi wa msamiati mkopo ulituwezesha kupambanua muundo wa silabi katika lugha ya Kikipsigis. Hali hii imechangia katika kuonyesha jinsi lugha inavyoimarika kutokana na ukopaji wa msamiati ili kukidhi mahitaji ya kimawasiliano katika jamii. Kwa kuwa mabadiliko ya lugha ni sifa kuu katika lugha yoyote ile, michakato na matokeo ya mabadiliko katika lugha hubainishwa kupitia msamiati katika lugha husika.

Utafiti huu pia ni muhimu katika kuchochea uchunguzi zaidi kuhusu ukopaji wa msamiati katika lugha nyingine za Kiafrika. Isitoshe, tasnifu hii ni kichocheo cha utafiti kuhusu suala pana la athari ya ujozi lugha katika jamii.

## **1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

### **1.8.1 Dhana ya ukopaji**

Tafiti mbalimbali kuhusu ukopaji wa msamiati katika lugha tofautitofauti zimeangaziwa na wanaisimu wanaojishughulisha na mabadiliko katika lugha (Walusimbi, 2002). Hii ni kwa sababu msamiati katika lugha yoyote ile, ni kipengele muhimu katika kubainisha mabadiliko ambayo yametokea katika lugha maalum. Walusimbi (kama hapo juu) anazidi kueleza kuwa tafiti hizo zimebainisha kuwa mojawapo ya matokeo ya mitagusano kati ya lugha mbili au zaidi ni ukopaji wa msamiati kutoka lugha moja hadi nyingine. Hali hii hutokea kwa sababu lugha zozote zinapoingiliana katika muktadha wa mawasiliano kuna uwezekano wa kupokezana msamiati ili kuwezesha mawasiliano.

Fromkin na Rodman (1988:135) wanaeleza kuwa msamiati mpya huweza kuingizwa katika lugha ili kuwezesha upanuzi wa msamiati kupitia njia mbalimbali kama vile ukopaji, tafsiri, ubunaji, unominishaji, unyambulishaji na hata upanuzi wa maana kisemantiki. Wanazidi kufafanua kuwa njia kuu ya kuongeza maneno mapya katika lugha ni kupitia mchakato wa ukopaji. Mchakato huu hutokana na lugha moja kuchukua neno au mofimu kutoka lugha nyingine na kuongeza katika leksia ya lugha hiyo. Hivyo basi leksia ya lugha huweza kugawika katika sehemu mbili: maneno asilia na maneno mkopo. Kulingana na maelezo haya ni kweli kuwa lugha inapokopa msamiati hupanua msamiati wake kwa kuingiza msamiati mpya wa kurejelea dhana geni katika utamaduni wa lugha hiyo. Fromkin na Rodman (kama hapo juu) wanazidi

kueleza kuwa lugha yoyote huweza kukopa msamiati moja kwa moja kutoka lugha nyingine au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza imekopa neno “feast” moja kwa moja kutoka lugha ya Kifaransa ilhali imekopa neno “algebra” kutoka lugha ya Kiarabu kupitia Kihispania. Hivyo basi neno hili limekopwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja kutoka Kiarabu kupitia Kihispania. Kwa hivyo mchakato wa ukopaji huweza kuhusisha zaidi ya lugha tatu ambapo lugha ‘a’ huweza kukopa msamiati kutoka lugha ‘b’; iliyokopa kutoka lugha ‘c’. Lugha ya Kikipsigis vilevile imekopa msamiati kutoka lugha ya Kiingereza au Kifaransa kupitia kwa Kiswahili. Kwa mfano msamiati mkopo ‘*kampunit*’ limekopwa kutoka kwa Kiswahili ‘kampuni’ ambapo Kiswahili kilikopa kutoka neno la Kiingereza ‘*company*’. Hata hivyo, utafiti huu haukujihususha na kuchunguza iwapo msamiati uliokopwa ulikopwa moja kwa moja au kupitia lugha nyingine.

Myers-Scotton (2002) anaeleza kuwa katika kuchunguza historia ya ukopaji, wataalamu wengi wamemwegemea mtaalamu Haugen (1950) anayefafanua ukopaji kuwa ni jaribio la kuzalisha katika lugha moja (lugha pokezi) ruwaza zinazotokea tayari katika lugha nyingine (lugha changizi). Kwa kutumia neno ruwaza, Haugen anarejelea elementi za kileksia na wala sio ruwaza za kisarufi kwa kuwa katika makala yake anatupa kategoria ya maneno-mkopo na mifanyiko ya uzalishaji katika lugha pokezi. Anazidi kueleza kuwa sio lazima lugha changizi kuwa na habari kuwa msamiati wake unakopwa na lugha nyingine, vilevile lugha inayokopa hailipi msamiati huo uliokopwa. Kulingana na Kembo-Sure (1993), maelezo haya ya Haugen yanafaa tu katika kuelezea kuhusu uhamishaji wa elementi za kileksia kutoka lugha moja hadi lugha nyingine kwa sababu yanakosa kutambua dhana ya ubunifu na uzalishaji katika ‘ukopaji’ na kusababisha dhana hii ya ‘ukopaji’ kurejelewa na wanaisimu wengine kama hali ya ‘maingilio’ katika lugha. Hali hii basi imewafanya



wanaisimu wengine kurejelea ukopaji kama ‘maingilio ya kileksia’ au ‘maingilio ya kisemantiki’. Kembo-Sure anaeleza kuwa maelezo haya yanasisitiza athari hasi ya mtagusano lugha na kupuuza athari chanya ya kiisimu na kijamii itokanayo na ujozi-lugha.

Kembo-Sure (1993) anafafanua ‘ukopaji’ kama mchakato tendi na zalishi unaosababisha neno la kigeni kuingizwa katika lugha nyingine (lugha pokezi) kwa kutoholewa ili likubalike katika muundo wa kifonetiki, kifonolojia na wa kimofolojia wa lugha hiyo pokezi. Kutokana na maelezo haya ni sharti msamiati unaolingizwa katika lugha pokezi kufanyiwa mabadiliko ya kifonolojia kulingana na mfumo wa lugha pokezi ili msamiati huo ukubalike kimatumizi katika lugha pokezi. Maelezo haya ya Kembo-Sure ni muhimu katika utafiti wetu kwani tuliangazia mabadiliko ya kifonolojia na kimofolojia yanayotokea katika msamiati unaokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza hadi Kikipsigis.

Haugen (1950) aliainisha aina tatu za matokeo ya mchakato wa ukopaji wa kileksia: kwanza ni ‘nenomkopo’ ambalo linarejelea neno linalochukuliwa kutoka lugha ya kigeni na kuingizwa katika mfumo wa kisarufi wa lugha pokezi. Pili ni ‘msamiati wa kuhamisha’ ambao ni msamiati unaochukuliwa kutoka lugha ya kigeni lakini umbo wake unatokana na lugha pokezi. Huhusisha tafsiri-mkopo na ukopaji wa kisemantiki. Tatu ni ‘msamiati wa kuchanganya’ ambao hurejelea mchanganyo wa msamiati wa lugha ya kwanza na ule wa lugha ya pili, Haugen alitumia pia msamiati ‘uhuluti’ kurejelea mkopo wa aina hii. Hata hivyo migawanyo hii ya Haugen haizingatiwi sana kwa sasa kwa kuwa tafiti zimeangazia aidha ‘mikopo’ au ‘msamiati-mkopo’.

Kuhusu suala la msamiati-mkopo, wanaisimu mbalimbali wamejaribu kubainisha kati ya msamiati-mkopo na ukopaji. Wanaisimu Thomason na Kaufman (1976), Heath

katika Methrie (2001) na Myers-Scotton (2006) wanaunga mkono dhana kuwa dhana hizi mbili zinarejelea msamiati unaochukuliwa kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Kwa upande mwingine, wanaisimu wengine wanapinga maoni haya na wamejaribu kubainisha tofauti kati ya dhana hizi mbili kwa kutoa sifa za kila moja. Kwa mfano, Haugen (1950) anafafanua dhana ‘ukopaji’ kama jaribio la kuzalisha katika lugha moja (lugha pokezi), ruwaza zilizopo tayari katika lugha nyingine (lugha changizi). Kwa hivyo kwake Haugen, msamiati-mkopo ni aina tu ya ukopaji. Naye Heath katika Methrie (2001) anayapinga madai haya kwa kueleza kwamba mikopo hairejelei neno moja ila hurejelea vipengele vya kiisimu ambavyo havijakamilika au vikiwa vimekamilika basi ni zaidi ya neno na huweza hata kuwa kirai ilhali msamiati-mkopo hurejelea neno moja tu lililokopwa. Kutokana na mitazamo ya wanaisimu hawa, utafiti wetu ulipendekeza kuwa ‘msamiati-mkopo’ na ‘mikopo’ hutoa maelezo kuhusu dhana moja ambayo ni uamilifu wa kiisimu ambapo lugha moja (lugha pokezi) hukopa msamiati kutoka lugha nyingine (lugha-changizi).

### **1.8.2 Mchakato wa ukopaji**

Webb & Kembo-Sure (2000) wanaeleza kuwa katika mchakato wa ukopaji msamiati, lugha iliyo na hadhi ya chini hukopa kutoka kwa lugha iliyo na hadhi ya juu. Naye Myers-Scotton (2002) anaeleza kuwa mojawapo ya matokeo ya ujozi-lugha ni ukuzaji wa elementi za kileksia baina ya lugha zinazohusika ambapo lugha iliyo na hadhi ya chini hukopa msamiati kutoka lugha iliyo na hadhi ya juu. Kwa hivyo kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu huwa ni kwamba mkondo wa ukopaji ni kutoka lugha iliyo na hadhi kuelekea kwa lugha isiyo na hadhi, labda kwa sababu ya farahi iliyo nayo lugha iliyo na hadhi ya juu.

Myers-Scotton (kama hapo juu) anazidi kueleza kuwa kuna aina mbili za ukopaji: ukopaji wa kiutamaduni na ukopaji wa kimtindo. Ukopaji wa kiutamaduni unarejelea ukopaji wa msamiati wa kurejelea dhana au vitu ambavyo ni vya kigeni katika utamaduni wa lugha husika. Hapa, msamiati-mkopo huweza kubeba sifa za kifonolojia kutoka lugha changizi hadi lugha pokezi. Kwa upande mwingine, ukopaji wa kimtindo hurejelea ukopaji wa msamiati unaowakilisha dhana zilizopo tayari katika lugha pokezi. Msamiati wa aina hii huingizwa sana katika lugha husika kwa sababu ya ubadilishaji msimbo.

Iribemwangi na Mukhwana (2011), wanaeleza kuwa ukopaji wa maneno huenda sambamba na urekebishaji wa neno ili lifuate kanuni za kifonolojia za lugha pokezi. Urekebishaji huu ndio utohozi na hufanya neno likubalike katika lugha hiyo pokezi. Hii ni kusema kuwa lugha hutumia ukopaji katika kujiongezea msamiati haja inapotokea. Yule (2006) anaelea kuwa njia kuu ya upanuzi wa msamiati katika lugha ni mbinu ya ukopaji wa maneno ambapo neno fulani huchukuliwa kutoka lugha changizi na kuingizwa katika lugha pokezi. Lugha hukopa msamiati kutoka lugha nyingine kutokana na sababu za kiisimu-jamii. Whitefield (1970) anaelea kuwa neno halikopwi tu kwa sababu dhana ambayo neno hilo linarejelea haipatikani katika lugha pokezi, ila watu hukopa kwa kuwa neno hilo ni la kigeni na kuonekana kuwa zuri zaidi kuliko lile asilia. Vilevile ukopaji husababishwa na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia na hata kuibuka kwa dhana geni katika nchi. Isitoshe, ubadilishaji msimbo katika mazingira ya mtagusano-lugha huweza kuleta ukopaji kati ya lugha solo na lugha bebwa (Myers-Scotton, 1997). Utafiti wetu ulizigatia maelezo ya wataalamu hawa katika kuchunguza sababu zinazoifanya lugha ya Kikipsigis kukopa msamiati kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Upanuzi wa misamiati husababisha mabadiliko katika lugha husika. Lugha hupanua msamiati wake ili kuweza kurejelea dhana geni na kuwezesha mahitaji ya kimawasiliano katika jamii. Bright (1997) katika Coulmas (1997) anaeleza kuwa lugha hubadilika mara kwa mara katika muundo wake (fonolojia, sarufi, semantiki na misamiati). Kwa hivyo, mabadiliko ya kimsamiati ni muhimu ili kuwezesha lugha kurejelea mambo mapya yanayoingizwa katika lugha hiyo. Hii ndio kichocheo cha utafiti huu kuchunguza motisha zinazoifanya lugha ya Kikipsigis kukopa na kuutumia msamiati wa Kiswahili na Kiingereza.

### **1.8.3 Ukopaji na ujozi lugha**

McMahon (1994) anaeleza kuwa kwa kiwango fulani ukopaji hutegemea ujozi lugha. Anafafanua kuwa mchakato wa lugha moja kukopa msamiati kutoka lugha nyingine hutegemea ujuzi alionao mtu huyo kuhusu lugha zote husika (lugha changizi na lugha pokezi). Nao LaCharite na Paradis (2000) wanaeleza kuwa wakopaji wa msamiati wa kileksia ni wana-ujuzi lugha na wanapaswa kufahamu fonolojia ya misimbo yote miwili yanayohusika katika ukopaji; yaani fonolojia ya lugha changizi na lugha pokezi. Kutokana na ufahamu huu basi wao huweza kuhamisha sauti kutoka lugha moja, lugha changizi hadi lugha nyingine, lugha pokezi. Wanaisimu hawa wanazidi kufafanua kuwa baada ya wanaujozi lugha kutohoa msamiati katika lugha pokezi, basi wanajamii wengine huutumia msamiati huo uliotoholewa. Msamiati huo huwa umekubaliwa na jamii ya wanaujozi lugha. Wanatoa mfano wa fonimu /x/ ambao ni sauti ya Kiarabu lakini imekopwa katika Fula na wanaujozi lugha walio na ujuzi wa Fula na Kiarabu waliosoma katika shule za Koran. Baada ya wanaujozi lugha hao kukopa fonimu hii inakubalika katika jamii na kutumiwa na wanajamii wengine. Utafiti wetu vilevile ulibainisha kuwa katika jamii ya wakipsigis wapo wanaumojia lugha wanaotumia msamiati mkopo bila hata kufahamu ulitoka katika lugha gani ila

kwa sababu umekubalika na kutumika katika jamii nao pia wameutumia namna unavyotumika na wanajamii wengine.

#### **1.8.4 Ukopaji na ubadilishaji msimbo**

Myers-Scotton (1988) anaeleza kwamba ukopaji huhusisha matumizi ya msamiati mkopo ambao unasambaa na kutumika katika jumuiya lugha na huwa umekubalika katika jamii husika. Nao Paradis na LaCharite (1997) wanaeleza kuwa katika ukopaji, msamiati mkopo huingizwa katika lugha solo na kutoholewa kufuata mfumo wa lugha hiyo kimofolojia, kifonolojia na hata kisintaksia. Ubadilishaji msimbo kwa upande mwingine huhusisha matumizi ya maneno ya kigeni ambayo hayatoholewi kifonolojia au kimofolojia katika lugha solo.

Myers-Scotton (1992) anafafanua kwamba tofauti nyingine kati ya ubadilishaji msimbo na ukopaji upo kwenye mtindo wa urudufu wa msamiati mkopo na uwezo wa kutabiri utohozi wake. Kwamba ukopaji katika lugha solo hutokea mara kwa mara na kuna uwezekano wa kutabiri mchakato wake wa kutohozi katika lugha solo. Hata hivyo katika ubadilishaji msimbo maneno yanayotumika hutokea mara chache na hayatabiriki. Vilevile msamiati mkopo hutumika sana katika maneno ambayo ni ya kigeni katika jumuiya lugha fulani.

Naye Muysken (1995) anaeleza kuwa ubadilishaji msimbo ni matumizi ya lugha mbili katika kishazi au tamko moja. Anafafanua kuwa ubadilishaji msimbo hutofautiana na dhana ya ukopaji kileksia kwa sababu katika ukopaji elementi za kileksia kutoka lugha moja huingizwa katika leksia ya lugha nyingine ambayo ni pokezi. Ubadilishaji msimbo kwa upande wake ni zao la mazungumzo kati ya wanaujozi lugha.

Asher & Simpson (1994) nao wanaeleza kuwa dhana ya ukopaji hurejelea maneno ya kigeni ambayo huingizwa katika leksia ya lugha pokezi lhali ubadilishaji msimbo

huhusisha matumizi ya maneno ya lugha nyingine katika lugha pokezi lakini maneno hayo huwa hayaingizwi katika leksia ya lugha hiyo pokezi.

Hatua hii ya kutofautisha baina ya ubadilishaji msimbo na ukopaji katika utafiti huu ni muhimu kwa kuwa tuliangazia msamiati mkopo na hivyo basi kuweka tofauti ya dhana hizi wazi ulituwezesha kukusanya data iliyotoholewa kikamilifu katika lugha pokezi ambayo ni Kikipsigis.

## **1.9 Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Fonolojia Zalishi (FZ) ya muundo wa konsonanti na irabu [KI] iliyoasisiwa na wataalamu Clements na Keyser (1983). Pili ni nadharia ya lugha solo iliyoasisiwa na Myers-Scotton (2002). Nadharia ya FZ ilituwezesha kuchanganua mabadiliko ya kimofonemiki wakati ambapo Kikipsigis kinakopa msamiati kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza ilhali nadharia ya lugha solo ilituongoza kubainisha sababu za kiisimujamii zinazosababisha ukopaji wa msamiati.

### **1.9.1 Nadharia ya fonolojia zalishi ya muundo wa konsonanti na irabu [KI]**

Nadharia ya FZ ya muundo wa konsonanti na irabu [KI] iliasisiwa na wataalamu Clements na Keyser (1983) ili kutoa maelezo kuhusu muundo wa silabi katika lugha. Nadharia hii ni mwendelezo wa mawazo ya Khan (1976) kuhusu uwakilishaji wa silabi. Inabaini silabi kwa kudai kuwa ina muundo wa mfungo wa utatu. Mfungo huo una silabi-kichwa [\$] ambayo inatokana na mfungo wa konsonanti na irabu [KI] iliyo na elementi ya konsonanti na Irabu. Elementi ya irabu katika mfungo huu inawakilisha kilele cha usonorari ilhali elementi ya konsonanti inawakilisha mwanzo wa silabi. Kwa hivyo waasisi hawa waliongeza mfungo wa KI katika uwakilishaji wa kifonolojia inayobainisha nafasi za uamilifu katika silabi.

Clements na Keyser (1983) Wanaeleza kuwa nadharia hii inatekeleza majukumu manne ambayo ni muhimu katika kufafanua fonolojia ya lugha:

**a) Kanuni bia za muundo wa silabi**

Nadharia hii inatoa maelezo kuhusu kanuni bia zinazofafanua muundo wa silabi. Inapambanua silabi kwa kudai kuwa ina muundo uliogawika katika sehemu tatu ambapo kila sehemu inawakilisha msamiati maalum (Clements na Keyser (1983:25). Msamiati katika sehemu ya kwanza una elementi moja yaani kipashio kimoja kimatamshi. Katika sehemu ya pili, yaani kifungo cha Konsonanti na Irabu [KI] kuna elementi mbili: konsonanti na irabu. Katika sehemu ya tatu; kiwango cha kipande sauti, msamiati una viambajengo vya Konsonanti na Irabu.

Kifungo cha [KI] hurejelewa pia kama msingi wa muundo wa silabi kwa kuwa kina nafasi za konsonanti na za irabu zinazojazwa na viambajengo vya msamiati husika. Kwa hivyo viambajengo hivi huingizwa katika nafasi hizo za K na I ili kuunda neno linalokubalika katika lugha husika.

Sehemu hizi tatu hubainisha jinsi ambavyo muundo wa silabi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

**b) Aina za miundo ya silabi**

Nadharia hii ya FZ pia inabainisha aina za miundo ya silabi na namna miundo hiyo hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Pia hupambanua kanuni za lugha maalum zinazoongoza muundo wa silabi. Inatufafanulia mchakato wa utohozi wa msamiati mkopo kupitia kwa muundo wa silabi kwa kutumia konsonanti na irabu. Hivyo basi, nadharia hii ni muhimu katika kupambanua muundo wa silabi wa msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis.

Kulingana na nadharia hii, vipengele vya kifungo cha konsonanti – irabu [KI], huongoza uamilifu katika silabi; yaani, hubainisha vipengele vilivyo kiini na vile visivyo-kiini katika silabi. Kiini cha silabi ni sehemu inayosikika sana katika silabi husika kuliko sehemu ya mwanzo na sehemu ya mwisho katika silabi. Clements na Keyser (1983:31) walipendekeza aina zifuatazo za kimsingi za silabi katika lugha:

- (i) Konsonanti-Irabu [KI]
- (ii) Irabu [I]
- (iii) Konsonanti-Irabu-Konsonanti [KIK]
- (iv) Irabu-Konsonanti [IK]

Pendekezo hili liliongoza utafiti wetu katika kuchanganua miundo ya silabi katika msamiati mkopo wa Kiswahili na Kiingereza unapotoholewa katika mfumo wa Kikipsigis.

### c) Mchakato wa usilabishaji

Nadharia hii inatoa maelezo kuhusu kanuni zinazoongoza mchakato wa usilabishaji katika lugha kwa kudai kuwa kila lugha ina kanuni zake maalum za usilabishaji. Kanuni hizi huweza kubadilisha viambajengo vya konsonanti na vya irabu katika neno husika. Kwa mfano Kiingereza huruhusu mfululizo wa konsonanti mwanzoni mwa neno kama ilivyo katika neno ‘*group*’ na ‘*Christmas*’. Vile vile Kiswahili jinsi ilivyo katika maneno kama vile, ‘mchele’ na ‘mkate’. Kikipsigis kwa upande wake hakiruhusu mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno.

Hivyo basi, nadharia hii ni muhimu kwa kuwa ilituwezesha kubainisha namna Kikipsigis hufanya mabadiliko katika msamiati ulio na mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Utafiti huu ulibainisha kuwa Kikipsigis huzingatia uchopezi wa irabu ili kuruhusu msamiati wa aina hii katika mfumo wake wa kifonolojia. Kwa



hivyo, neno ‘*group*’ linatoholewa kuwa ‘*kurupit*’, ilhali neno ‘mchele’ linakuwa ‘*muchelek*’.

**d) Utata kuhusu mipaka ya silabi**

Nadharia hii vilevile inapambanua suluhisho la utata kuhusu mipaka ya silabi. Clements na Keyser (kama hapo juu) wanaeleza kuwa sauti za irabu ndizo zinasosababisha kilele cha silabi. Kwamba sehemu ya neno iliyo na elementi ya konsonanti katika ufungo wa KI, haina usilabi ilhali sehemu iliyo na elementi ya irabu ina usilabi na vilevile usonorati. Kanuni zinazosuluhisha utata huu zinaeleza kuwa:

- *Maneno yanayoanza kwa mfuatano wa konsonanti, hutoholewa ili kufuata mfumo wa silabi katika lugha husika.*

(Ty)

- *Maneno yanayoishia kwa mfuatano wa konsonanti vilevile hutoholewa ili kufuata mfumo wa silabi katika lugha husika.*

(Ty)

Kwa hivyo, kwa mujibu wa nadharia hii, ni sharti silabi zichunguzwe kwa misingi ya sheria/ kanuni za lugha husika. Hii ni kwa sababu lugha mbalimbali hutofautiana katika mpangilio wa fonimu zinazounda silabi na hatimaye neno linalokubalika katika lugha husika.

Nadharia hii ni muhimu katika uchanganuzi wa msamiati mkopo katika Kikipsigis kutoka Kiswahili na Kiingereza kwa kuwa ilituwezesha kubainisha na kufafanua michakato ambayo msamiati mkopo kutoka lugha hizi mbili hupitia kabla ya kukubalika katika Kikipsigis.

### 1.9.2 Nadharia ya lugha solo

Nadharia ya lugha solo iliasisiwa na mtaalamu Myers-Scotton (1997). Nadharia hii ilielekezwa katika kutoa maelezo kuhusu muundo wa maneno katika ubadilishaji msimbo. Hata hivyo, Myers-Scotton na Jake (2000) na Myers-Scotton (2002) wameiboresha nadharia hii ili kutoa maelezo kuhusu miundo tofauti tofauti ya mtagusano lugha kama vile kujifunza lugha ya pili, ukopaji na hata uundaji wa Krioli. Utafiti huu hata hivyo ulijikita tu katika aina moja ya matokeo haya ya mtagusano lugha ambayo ni ukopaji wa msamiati kutoka Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis.

Nadharia hii kulingana na Myers-Scotton (2002) imejengwa katika ubainishaji wa dhana mbili; kwanza ni ubainishaji kati ya lugha solo na lugha bebwa. Lugha solo ni lugha kuu katika mchakato wa ukopaji wa msamiati kutoka lugha moja hadi nyingine. Hutawala mpangilio wa maneno na sarufi ya msamiati mkopo. Katika utafiti huu, lugha solo ni lugha ya Kikipsigis kwa kuwa inatawala muundo wa silabi katika utohozi wa msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza. Kwa upande mwingine, lugha bebwa ni lugha inayotoa elementi za kileksia zinazoingizwa katika lugha solo yaani msamiati mkopo. Msamiati huo hupitia mabadiliko ya kimofonemiki ili kukubalika katika mfumo wa lugha solo ambayo ni kuu katika mchakato wa ukopaji. Kwa mfano, msamiati wa Kiswahili ‘mwalimu’ unapokopwa katika lugha ya Kikipsigis hutoholewa kuwa *mwalimuyot* ili kuingia katika mfumo wa Kikipsigis. Hivyo basi Kikipsigis kitakuwa lugha solo ilhali Kiswahili kitakuwa lugha bebwa.

Pili ni ubainishaji kati ya mofimu-beba maana na mofimu ya kimfumo. Mofimu-beba maana hurejelea aina mbalimbali ya maneno yanayokopwa kama vile nomino na vitenzi. Maneno haya hutoka kwa lugha bebwa. Mofimu za kimfumo hurejelea

mofimu zinazoongoza upatanishi wa kisarufi kati ya neno moja na lingine kama vile viambishi na vihusishi. Kwa mfano neno la Kiingereza “premier league” hutoholewa kama “*ligit ab primia*” katika Kikipsigis. Kwa hivyo neno ‘ligi’ litakuwa linabeba maana (mofimu-beba maana) ilhali kiambishi ‘ab’ katika Kikipsigis kitakuwa mofimu ya kimfumo. Hivyo basi mofimu ya kimfumo hutoka katika lugha solo ilhali mofimu-beba maana hutoka kwa lugha bebwa.

Utafiti huu vilevile uliongozwa na mawazo ya Myers-Scotton kuwa mitagusano ya lugha husababisha athari katika lugha zinazotagusana. Anaeleza kuwa mitagusano ya lugha huathiri leksia, fonolojia na hata mofosintaksia ya lugha mbili au zaidi zinazotagusana. Anazidi kufafanua kuwa matokeo ya mtagusano lugha ni pamoja na ukopaji wa msamiati, ujozi lugha na uundaji wa pijini na krioli. Hata hivyo utafiti huu ulijikita tu katika ukopaji wa msamiati. Msamiati unaokopwa huweza kutumiwa kurejelea dhana geni katika lugha husika ama dhana zilizopo tayari katika lugha hiyo.

Myers-Scotton (2002) anazidi kueleza kuwa ukopaji wa msamiati husababishwa na hadhi ya lugha katika jamii ambapo lugha iliyo na hadhi ya chini hukopa kutoka lugha iliyo na hadhi ya juu ili kujisanisibisha na lugha hiyo. Mtaalamu huyu anaeleza pia kuwa lugha huweza kukopa msamiati hata wakati ambapo ina msamiati asilia wa kurejelea dhana husika. Hii ni kwa sababu maneno mkopo huwa mafupi kwa mfano msamiati wa Kiingereza unaorejelea takwimu hupendelewa kwa kuwa ni mfupi katika lugha ya Shona hata ingawa lugha hii ina msamiati asilia wa takwimu (Myers-Scotton, 2002). Katika utafiti huu, mawazo haya ya Myers-Scotton yalituongoza katika kubainisha visababishi vya ukopaji na vilevile iwapo kuna sababu nyinginezo mbali na alizozitaja Myers-Scotton zinazochangia ukopaji wa msamiati wa Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis

Nadharia hizi mbili ni faafu katika utafiti huu kwa kuwa nadharia ya FZ ya muundo wa konsonanti na irabu ilituwezesha kubainisha utohozi wa kimofonemiki unaotokea wakati msamiati mkopo kutoka Kiingereza na Kiswahili unapoingizwa katika Kikipsigis ilhali nadharia ya lugha solo ilituongoza kudadisi sababu za ukopaji wa msamiati.

## **1.10 Mbinu za Utafiti**

### **1.10.1 Uteuzi wa sampuli**

Sampuli ya utafiti huu ilituuliwa kimakusudi. Aina hii ya uteuzi wa sampuli ilitumika ili kuhakikisha kuwa tunakusanya data nyingi iliyotuwezesha kuangazia suala la utafiti kikamilifu. Vituo vitatu vya redio vinavyotangaza kwa Kikalenjin viliteuliwa kimakusudi kwa kuwa ni maarufu, huangazia masuala mbalimbali katika jamii na husikika katika maeneo mengi mnamozungumzwa lugha hii. Kwa hivyo, tulihisi kwamba kulikuwa na uwezekano wa kukusanya data nyingi na ifaayo kwa minajili ya utafiti huu. Vituo hivyo vya redio vilikuwa; Chamgei Fm, Kitwek Fm na Kass Fm.

Katika vituo hivi, tulikusanya data kutoka kwa taarifa za habari zilizosomwa kwenye vituo hivyo pasi na kuzingatia ripoti za nyanjani. Vilevile tulikusanya data kutoka kwa matangazo ya vifo, biashara na michezo. Matangazo haya huja baada ya taarifa za habari kukamilika. Data ilikusanywa kwa muda wa miezi minne; kutoka mwezi wa Oktoba, 2014, hadi Januari, 2015 ili kutuwezesha kukusanya data tofautitofauti kwa kuwa mambo yanayoangaziwa katika vyombo vya habari hutegemea matukio yanayoendelea katika nchi. Mara nyingi msamiati hurudiwa katika siku za wiki iwapo matukio ya wiki hiyo yanafanana. Muda huu pia ulituwezesha kukusanya data nyingi ya kuangazia suala la utafiti. Katika miezi hii minne tulisikiliza na kunakili msamiati mkopo katika vituo hivi vitatu kila siku. Tulisikiliza na kunakili msamiati mkopo

uliojitokeza katika taarifa za habari na matangazo husika ya Changei Fm kila asubuhi, Kitwek Fm wakati wa mchana na kisha Kass Fm wakati wa jioni. Tulirekodi pia matangazo hayo kwa ajili ya marejeleo iwapo tungehitajika kufanya hivyo.

### **1.10.2 Ukusanyaji wa data**

Data ya kimsingi iliyotumika katika utafiti huu ilikuwa msamiati mkopo katika Kikipsigis kutoka Kiswahili na Kiingereza. Ukusanyaji wake ulihusisha kusikiliza na kunakili msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza uliotumika katika vituo vya redio vilivyoteuliwa. Vilevile, ili kupata data nyingi, tulisoma vitabu vilivyoandikwa katika Kikalenjin na kisha kuteua msamiati mkopo katika Kikipsigis kutoka Kiswahili na Kiingereza. Vitabu hivyo vilikuwa vitabu vya kidini na TKK (Tujifunze Kusoma Kikwetu). Vitabu vya TKK ni vile vilivyotumika katika ufundishaji wa lugha za kwanza katika shule za misingi. Zoezi hili la ukusanyaji wa data lilitupa jumla ya msamiati 275; ambayo ilikuwa ni data nyingi kuliko tulivyotarajia. Hata hivyo, tulihisi kwamba ilikuwa vyema kuwa na hazina kubwa ya msamiati ili kuwezesha utafiti kufanyika.

Baada ya kukusanya data, tuliandaa hojaji iliyotumika katika kuthibitisha iwapo msamiati uliokusanywa ulikuwa unapatikana katika Kikipsigis na vilevile kuthibitisha jinsi ya kuandika msamiati husika katika Kikipsigis. Watafitiwa sita waliteuliwa kimakusudi katika kuthibitisha msamiati uliokusanywa. Watafitiwa hawa walikuwa walimu wa isimu, wawili kutoka chuo kikuu, wawili kutoka shule za upili na wawili kutoka shule za msingi. Wote walikuwa wazawa wa Kikipsigis.

### **1.10.3 Vifaa vya kukusanya data**

Redio ilikuwa kifaa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa matangazo tuliyoyazingatia ili kupata data ya utafiti huu yalipeperushwa kupitia chombo hicho.

Vifaa vilivyotumwa kukusanya data ni kalamu na daftari ili kunakili msamiati mkopo uliokusanywa kutoka kwa vituo vya redio vilivyoteuliwa na vitabu vilivyosomwa. Tepu rekoda ilitumiwa kurekodi taarifa za habari na matangazo husika ili kurejelewa na mtafiti panapo haja.

#### **1.10.4. Uchanganuzi wa data**

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mwelekeo mseto wa uchanganuzi kwa kuzingatia madhumini ya utafiti. Uchanganuzi wa kitakwimu ulitumika katika kupanga data katika majedwali ili kubainisha kategoria za msamiati uliokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis. Katika uchanganuzi wa kisifa, utafiti ulijikita katika uchanganuzi fafanuzi ili kubainisha mabadiliko ya kimofofonemiki yanayotokea katika msamiati mkopo kwa kuongozwa na nadharia ya FZ wa KI. Aidha, majedwali na vielelezo vilitumika kuonyesha mabadiliko hayo ya kimofofonemiki kabla ya kutoa maelezo mwafaka ya mabadiliko hayo. Kisha uchanganuzi wa sababu za kiisimujamii zinazochangia uingizwaji wa msamiati mkopo uliongozwa na nadharia ya lugha solo.

**SURA YA PILI**  
**MSAMIATI MKOPO WA KIINGEREZA NA KISWAHILI KATIKA**  
**KIKIPSIGIS**

**2.0 Utangulizi**

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza utohozi wa msamiati mkopo katika Kikipsigis. Sura hii inajihusisha na utimizwaji wa madhumuni mawili ya utafiti; kutambulisha msamiati mkopo kutoka Kiingereza na Kiswahili katika Kikipsigis, na pili, kubainisha kategoria za msamiati mkopo katika Kikipsigis. Katika kutambua msamiati mkopo, tumeainisha data ya utafiti huu katika mawanda mbalimbali ambamo msamiati huo unatumika. Mawanda hayo ni kama vile sayansi/teknolojia, biashara, elimu, dini, uchumi, nyumbani/jamii na kazini.

Uainishaji huu wa data katika nyanja mbalimbali ni muhimu ili kutuwezesha kutambua sekta ambazo Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka kwazo. Vile vile, uainishaji huu ni muhimu katika kubainisha sababu za ukopaji wa msamiati jinsi itakavyobainika katika sura ya tano.

Msamiati mkopo pia uliainishwa katika aina mbalimbali za maneno ili kubainisha kategoria za msamiati mkopo katika Kikipsigis. Kategoria hizo ni nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, vihusishi, viunganishi na vihisishi. Uainishaji huu ulituwezesha kufahamu aina za maneno ambazo Kikipsigis kimekopa sana iwe ni nomino au vitenzi au aina nyingine yoyote ya maneno.

**2.1 Utambuzi wa Msamiati Mkopo**

Baada ya kukusanya data kutoka kwa vituo vya redio vilivyotajwa, tulidondoa data zilizorudiwarudiwa kwa sababu msamiati katika taarifa na matangazo yaliyohusika yalirudiwarudiwa kwa kutegemea matukio ya wiki husika. Baada ya kudondoa,

tulianisha msamiati mkopo katika nyanja mbalimbali. Uainishaji huu ulituwezesha kubaini nyanja ambazo Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka kwazo na kufanya ulinganifu katika lugha bebwa husika, yaani Kiingereza na Kiswahili. Uainishaji huu umedhihirishwa kupitia kwa majedwali yafuatayo:

**Jedwali 2.1.1: Msamiati wa Siasa**

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Referendum	<i>Rearendum</i>	Kura ya maoni
Minister	<i>Ministayat</i>	Waziri
Parliament	<i>Paliamen</i>	Bunge
Ward	<i>Wotit</i>	Wadi
Area	<i>Eryait</i>	Eneo
Chief	<i>Chip</i>	Chifu
Committee	<i>Kamitii</i>	Kamati
Councillor	<i>Kansolayat</i>	Diwani
Campaign	<i>Kambein</i>	Kampeni

<b>Kiwahili</b>	<b>Kipsigis</b>
Katiba	<i>Katipa</i>
Askari	<i>Asigorindet</i>
Chama	<i>Chamait</i>
Serikali	<i>Sergalit</i>
Kaunti	<i>Kaundi</i>
Spika	<i>Spika</i>
Korokoroni	<i>Korgoret</i>
Gavana	<i>Kapanayat</i>
Seneta	<i>Senetayat</i>
Kortini	<i>Kotini</i>
Kesi	<i>Kesiit</i>
Lesheni	<i>Lesyenit</i>
Kura	<i>Kurayat</i>
Uhuru	<i>Uuru</i>
Pendera	<i>Penderet</i>

Wakipsigis waliishi katika makundi yaliyojulikana kama 'kokwet' katika umoja na kokwotinwek katika wingi. Haya ni makundi yaliyojumuisha familia kati ya ishirini



hadi arobaini. Neno *Kokwet* linatokana na neno *kok* linalomaanisha mahali maalumu nje, mbele ya nyumba kuu anapobarizi mwanamume. Aghalabu huwa chini ya mti au kijumba kidogo cha msonge wenye ukuta ulio wazi.

Vilevile, *kokwet* hurejelea mikutano ya kijamii inayoongozwa na *poiyo ap kokwet* (mkuu wa *kokwet*) na kuhudhuriwa na wanaume pekee. Wanawake na watoto walihudhuria tu walipohitajika kutoa ushuhuda. Mikutano hiyo ililenga kujadili masuala ya uongozi katika jamii, kutafuta suluhisho la migogoro katika jamii, kukashifu wanaotenda mambo kinyume na matarajio ya jamii na hata kuandaa sherehe za mavuno shambani n.k. Mikutano hiyo ilifanyika katika eneo mbali na makazi ya watu. Kwa hivyo, jamii hii ilikuwa na misamiati ya kurejelea dhana za uongozi/siasa kama vile *kokwet*, *kandoindet*, *tuiyet*, *emet*, *oret*, *koret*, *poiyo ab tumdo* n.k. Hivi sasa, mfumo huu wa uongozi umebadilika kadri maisha ya jamii yanavyozidi kubadilika. Hali ilivyo sasa ni kuwa Wakipsigis wanafuata mfumo wa uongozi ulioletwa na serikali ya Waingereza waliokuwa wakoloni nchini Kenya. Hali hii imechangia pakubwa ukopaji wa misamiati katika uwanja huu ili kurejelea dhana za uongozi/siasa ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis, kwa mfano maneno k.v. *kapanayat* (gavana), *kurayat* (kura), *paliamen* (bunge), *uuru* (uhuru) na nyinginezo.

**Jedwali 2.1.2: Msamiati wa Sayansi/Teknolojia**

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Computer	<i>Kompyutait</i>	Tarakilishi
Digital	<i>Tichitol</i>	Kidijitali
Analog	<i>Analok</i>	Analogi
Television	<i>Telepisyon</i>	Runinga
Machine	<i>Mosyinit</i>	Mashine
Studio	<i>Stutyo</i>	Studio
Bomb	<i>Pomit</i>	Bomu
Redio	<i>Retio</i>	Redio
Factory	<i>Paktori</i>	Viwanda
Cement	<i>Simendi</i>	Simiti
Fredge	<i>Prichit</i>	Jokovu

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
Simu	<i>Simoit</i>
Bunduki	<i>Pundugit</i>
Risasi	<i>Risasyat</i>
Chuma	<i>Chumoiyot</i>
Kampuni	<i>Kambuniit</i>
Stima	<i>Sitimet</i>

Msamiati wa sayansi na teknolojia hurejelea dhana geni ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis. Hii ni kwa sababu dhana hizi zililetwa na wageni kutokana na maendeleo ya kiteknolojia ulimwenguni kote. Kwa mfano, vifaa vya kimawasiliano kama vile kompyuta, simu, redio, televisheni havikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis kabla ya majilio ya wageni. Waliwasiliana kupitia kwa njia mbalimbali k.v. *sugutit* (ngoma) *wagaat* (mayowe) *kigondiit* (tarumbeta), *marianet* (upipigaji wa mluzi), *iyeto* (moshi), *mestowot* (mjumbe aliyetumwa kutembea masafa marefu kupeleka ujumbe) miongoni mwa njia nyinginezo.

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesababisha kuwepo na njia mbadala ya mawasiliano katika jamii. Bila shaka pameibuka istilahi mbalimbali ya kurejelea vifaa hivi vya kisayansi pamoja na mbinu za mawasiliano. Istilahi hizi zimeingizwa katika

Kikipsigis kupitia utohozi ili kuwawezesha Wakipsigis kupata istilahi za kurejelea dhana hizo.

### Jedwali 2.1.3: Msamiati wa Kielimu

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Nursery	<i>Nasaret</i>	Chekechea
School	<i>Sukulit</i>	Shule
Test	<i>Testi</i>	Mtihani
Diploma	<i>Tiploma</i>	Stashahada
Professor	<i>Propesayat</i>	Profesa
Secondary	<i>Secondary</i>	Shule ya upili
Diary	<i>Taiyari</i>	Shajara
Project	<i>Prochekt</i>	Mradi
Budget	<i>Pachet</i>	Bajeti
Report	<i>Ripot</i>	Ripoti
Group	<i>Kurupit</i>	Kikundi
Permit	<i>Pamit</i>	Idhini
Rubber	<i>Rapa</i>	Kifutio

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
Gazeti	<i>Kasetit</i>
Hesabu	<i>Esapuuk</i>
Kitabu	<i>Kitapuut</i>
Kalamu	<i>Kalamit</i>
Masomo	<i>Somanet</i>
Karatasi	<i>Kartasiit</i>
Mwalimu	<i>Mwalimuyot</i>
Barua	<i>Paruet</i>
Tarehe	<i>Tarigiit</i>
Bahasa	<i>Paasyait</i>
Wiki	<i>Wigiit</i>

Hekima na maarifa katika utamaduni wa Wakipsigis yalipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia mazungumzo. Kwa hivyo, wakoloni na wamisheni walipofika nchini Kenya na kuanzisha mfumo wa elimu, Wakipsigis hawakuwa na budi ila kukopa misamiati katika uwanja huu. Kwa mfano, kitabu, kalamu, shule,

karatasi, profesa na nyinginezo ili kuweza kurejelea dhana hizi ambazo hazikuwepo katika utamaduni wao.

**Jedwali 2.1.4: Msamiati kuhusu ajira**

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Officer	<i>Opisayat</i>	Afisa
Office	<i>Opisit</i>	Ofisi
Police	<i>Polisiot</i>	Polisi
Conductor	<i>Kondaktayat</i>	Utingo
Hoteli	<i>Oтелиit</i>	Mkahawa
Mechanic	<i>Maganigayat</i>	Fundi wa mitambo
Director	<i>Tairektayat</i>	Mkurugenzi
Council	<i>Kansol</i>	Kamati
Butchery	<i>Pucherit</i>	Buchari
Member	<i>Membayat</i>	Mwanachama
Choir	<i>Kwaya</i>	Kwaya

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
Wakili	<i>Ogilyot</i>
Dereva	<i>Inderepayat</i>
Mgomo	<i>Komanet</i>
Mshahara	<i>Musyara</i>
Ruhusa	<i>Rusa</i>
Fundi	<i>Pundiyot</i>
Kazi	<i>Kasit</i>
Dakika	<i>Tagigaisiek</i>
Duka	<i>Tuget</i>
Faida	<i>Paita</i>

Katika jamii ya Wakipsigis, wanaume waliruhusiwa kuoja wanawake zaidi ya mmoja kwa sababu wanajamii walithamini watoto wengi. Hali hii ilitokana na imani kuwa watoto ndio waliotegemewa kuwasaidia wazazi kufanya kazi ili familia ipate riziki. Kazi hizo zilikuwa za ukulima, ufugaji na biashara. Kwa hivyo, misamiati ya ajira iliyokopwa katika jamii hii inarejelea kazi ambazo hazikuwepo katika utamaduni wao; zilitokana na mabadiliko katika jamii yaliyochangiwa na majilio ya wakoloni na wamisheni.

**Jedwali 2.1.5: Msamiati wa kidini**

<b>Kiingereza</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>	<b>Tafsiri</b>
Reverend	<i>Reparen</i>	Mchungaji
Sabath	<i>Sapato</i>	Sabato
Christmas	<i>Kirismas</i>	Krismasi
Christians	<i>Kiristianik</i>	Wakristo
Pastor	<i>Pastayat</i>	Mhubiri
Satan	<i>Syetani</i>	Shetani
Padre	<i>Patiryot</i>	Kasisi

<b>Kiswahili</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>
Ubatizo	<i>Kapatisanet</i>
Kanisa	<i>Kaniset</i>
Hekalu	<i>Egaluut</i>
Katoliki	<i>Katolik</i>
Malaika	<i>Malaigayat</i>
Yesu	<i>Cheiso</i>
Msalaba	<i>Musalapet</i>

Wakipsigis walikuwa na mitindo yao ya kidini ambapo walimheshimu na kumwabudu Mungu. Walimrejelea mwenyezi Mungu kwa jina *Asis* (Jua). Hii ni kutokana nguvu za jua na umuhimu wake kwa binadamu, wanyama, mimea na kila kitu duniani. Jua liliwakumbusha uwepo na ukuu wa Mwenyezi Mungu. Wakipsigis walimwabudu Mungu wakitazama upande wa mashariki wakati jua linapochomoza na magharibi jua lituapo. Walipotoa maombi maalum, walijumuika katika mahali patakatifu (*kapkorosut*). Kwa hivyo, jamii hii ilikuwa na misamiati asilia ya kurejelea dhana za kidini. Hata hivyo, wamisheni walipofika barani Afrika kusambaza dini, athari za dini yao katika dini ya Wakipsigis zilisheni kote kote, tukio ambalo lilisababisha kuenea kwa dhana geni za kidini ambazo zilikopwa na Wakipsigis kutoka kwa dini ya Kikristo, kama vile, *kaniset/egaluut* (kanisa), *msalapet* (msalaba), *pastayat* (*pastor*) miongoni mwa nyinginezo.

**Jedwali 2.1.6: Msamiati wa tiba na masuala ya afya**

<b>Kiingereza</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>	<b>Tafsiri</b>
Mortuary	<i>Mochari</i>	Mochari
Tetanus	<i>Tetas</i>	Pepopunda
Hospital	<i>Sipitaliit</i>	Hospitali
Ward	<i>Wotit</i>	Wodi
Net	<i>Netit</i>	Chandarua
Syringe	<i>Sirinjit</i>	Sirinji
Lab	<i>Lapit</i>	Maabara

<b>Kiswahili</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>
Daktari	<i>Tagitarindet</i>
Sindano	<i>Sindanut</i>

Matibabu katika jamii ya Wakipsigis yalitolewa na tabibu wa kienyeji aliyelitwa *Chepkerichot/Chepsogeiyot*. Tabibu huyo aliyatibu magonjwa kwa kutumia dawa za kienyeji kwa mfano majani na mizizi ya miti mbalimbali. Dawa hiyo ilirejelewa kamakerichot katika umoja na *kerichek* katika wingi. Hii ndiyo maana Walowezi walipopanda majani chai katika maeneo ya Kericho, Sotik na Bomet (wanakoishi Wakipsigis), wenyeji waliona majani chai kama mmea unaoweza kutoa dawa kupitia majani na mizizi yake. Hii ndio sababu eneo hilo likaitwa *Kericho* kutokana na neno *kerichot*. Katika utafiti huu, data ilibainisha kuwa asilimia kubwa ya misamiati mkopo kutoka Kiingereza na Kiswahili hurejelea dhana ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis kama vile *sindanut* (sindano), *sipitaliit* (hospitali) na *wotit* (wadi) miongoni mwa mengine. Hata hivyo, msamiati *tagitari* umekopwa ilhali wakipsigis walikuwa na neno *chepkerichot* kumrejelea tabibu. Sababu za ukopaji wa aina hii zimefafanuliwa katika sura ya tano.

**Jedwali 2.1.7: Msamiati wa michezo**

<b>Kiingereza</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>	<b>Tafsiri</b>
Premier	<i>Premia</i>	Premia
League	<i>Ligit</i>	Ligi
Medal	<i>Metoliot</i>	Nishani
Point	<i>Poindit</i>	Pointi
Lane	<i>Lenit</i>	Njia nyembamba
Club	<i>Kilapit</i>	Kilabu
Game	<i>Kemit</i>	Mchezo

<b>Kiswahili</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>
Mpira	<i>Mbiret</i>
Timu	<i>Timit</i>
Kadi	<i>Katit</i>
Uwanja	<i>Kiwanchet</i>

Suala la michezo lilikuwa adimu miongoni mwa jamii ya Wakipsigis. Ingawa watoto walicheza michezo ya kukumbizana miongoni mwa michezo mingine, hapakuwepo michezo rasmi kama ilivyo sasa. Michezo ilihusishwa sana na watoto wadogo na hivyo watu wazima hawakuhusika kwa namna yoyote. Majilio ya wageni yaliathiri pakubwa ulingo huu. Kadri jamii ilivyoendelea ndivyo michezo ilishika kasi. Kwa sasa michezo ni mingi hadi imekuwa kitega-uchumi na kusababisha wanajamii wote kujihusisha kikamilifu. Kuenea huku kumesababisha lugha ya Kikipsigis kukopa misamiati ili kurejelea dhana hizo. K.m. *mbiret* (mpira), *timit* (timu), *kilapit* (club).

**Jedwali 2.1.8: Msamiati wa Kilimo**

<b>Kiingereza</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>	<b>Tafsiri</b>
Phosphate	<i>Pospet</i>	Mbolea
Pump	<i>Pambit</i>	Pampu
Fertilizer	<i>Patalaisa</i>	Mbolea
Plot	<i>Plotit</i>	Ploti
Tractor	<i>Toroktet</i>	Trekta
Wheelbarrow	<i>Wilbaroit</i>	Toroli
Forest	<i>Poresti</i>	Msitu
Scheme	<i>Sigiim</i>	Eneo

<b>Kiswahili</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>
Kilo	<i>Kiloit</i>
Panga	<i>Panget</i>
Reki	<i>Rekit</i>
Uma	<i>Umait</i>

Kabla ya majilio ya Wakoloni, Wakipsigis hawakujihusisha na ukulima wowote, maisha yao yalitegemea uwindaji wa wanayama pori kwa ajili ya nyama na damu na utundaji wa matunda ya mweituni. Baadaye walianza ufugaji na ukulima wa mimea mbalimbali k.v. chai, mahindi, maharagwe, kahawa miongoni mwa nyinginezo ambayo walijifunza kutoka kwa wageni. Kutokana na hayo, walijifunza mbinu za kisasa za ukulima na hivyo kulazimika kukopa misamiati ya kurejelea dhana hizi za kigeni kama vile *panget*, *kiloit*, *pospet*, *pampit* miongoni mwa mengine.



**Jedwali 2.1.9. Msamiati wa usafiri**

<b>Kiingereza</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>	<b>Tafsiri</b>
Bus	<i>Pasit</i>	Basi
Bicycle	<i>Poskilit</i>	Baiskeli
Lorry	<i>Lorit</i>	Lori
Tractor	<i>Toreket</i>	Trekta

<b>Kiswahili</b>	<b><i>Kikipsigis</i></b>
Ndege	<i>Indegeit</i>
Gari	<i>Karit</i>
Daraja	<i>Tarachet</i>
Pikipiki	<i>Pigipigiit</i>
Meli	<i>Melit</i>
Barabara	<i>Paraparet</i>
Lami	<i>Lamit</i>
Safari	<i>Saparit</i>
Bahari	<i>Pariit</i>

Maendeleo ya teknolojia yamesababisha mabadiliko mengi katika maisha ya Wakipsigis. Maendeleo haya yanahusishwa sana na majilio ya wageni hasa kutoka Ulaya ambao walieneza elimu na kuboresha maisha ya Waafrika. Yote haya yameathiri pakubwa uwanja wa usafiri. Awali, Wakipsigis walisafiri kwa miguu na au kwa kutumia wanyama kama vile punda na fahali. Walipofika wageni, walileta mbinu mbadala ya kurahisisha usafiri k.v. kutumia reli, maji (bahari), barabara na anga. Ni kutokana na njia hizi za usafiri ndipo paliibuka vyombo vya usafiri k.v. treni, meli, ndege, gari n.k. Kwa hivyo, palikuwa na hitaji la istilahi za kurejelea njia hizi za usafiri pamoja na vyombo vyenyewe. Hapa ndipo misamiati ikakopwa kutoka kwa Kiingereza na Kiswahili, k.m. *pasit, karit, loriit, poiskiliit, melit, tarachet na paraparet.*

**Jedwali 2.1.10: Msamiati wa mavazi**

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Sweater	<i>Swetait</i>	Sweta
Blanket	<i>Purangetit</i>	Blanketi
Sheet	<i>Sitit</i>	Shiti
Mattress	<i>Matresit</i>	Gondoro
Shirt	<i>Syatit</i>	Shati
Long trouser	<i>Long'it</i>	Suruali ndefu
Towel	<i>Toguloit</i>	Taulo
Jacket	<i>Chegetit</i>	Jaketi
Handkerchief	<i>Ankachip</i>	Kitambaa

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
Nguo	<i>Ingoriet</i>
Mshipi	<i>Mosipiit</i>
Kitambaa	<i>Kitambaet</i>
Marinda	<i>Marindet</i>
Kiatu	<i>Kweyot</i>
Leso	<i>Lesoit</i>
Kibeti	<i>Kipetit</i>
Kichanuo	<i>Kichanwet</i>

Kabla ya majilio ya mitindo ya mavazi ya kimagharibi, Wakalenjin walikuwa na mavazi yao asilia ambayo yalikuwa ni ngozi za wanyama wa kufugwa ama wa porini (*muito*). Wanyama hao waliuliwa na kisha ngozi zao kutumika kutengeneza mavazi ya wanajamii mbalimbali. Waingereza walipofika nchini Kenya kuleta ukoloni waliyaona mavazi hayo kuwa duni. Kwa hivyo, waliwaathiri Wakenya kimavazi na kwa sasa jamii karibu zote za Kenya zimeiga mitindo ya mavazi ya kimagharibi. Hivyo basi Wakipsigis walikopa msamiati kurejelea mavazi hayo ya kigeni kama vile *mosipiit, sitit, longit, kweyot, ngoriet, marindet n.k.*

**Jedwali 2.1.11: Msamiati wa vyakula**

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Cabbage	<i>Kepich</i>	Kabechi
Soup	<i>Supu</i>	Supu
Sugar	<i>Sugaruk</i>	Sukari
Supper	<i>Sapa</i>	Chajio
Lunch	<i>Lanchi</i>	Chamcha
Spinach	<i>Sipinach</i>	Spinachi

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
Mchele	<i>Muchelek</i>
Nyanya	<i>Nyanyaat</i>
Njugu	<i>Inchuguuk</i>
Viazi	<i>Pyasinik</i>
Maharagwe	<i>Marakweek</i>
Ndizi	<i>Indisiot</i>
Machungwa	<i>Machungwat</i>
Ngano	<i>Inganuk</i>
Mhogo	<i>Mogo</i>
Chumvi	<i>Chumbik</i>
Chai	<i>Chaik</i>

Chakula kinachopendwa na Wakipsigis tangu zamani ni *kimnyet* (ugali) na *chego* (maziwa). Jamii hii ilikuwa na msamiati wa kurejelea vyakula vya aina mbalimbali. Hata hivyo, Waingereza walipoleta vyakula vyao nchini Kenya, Wakipsigis walikopa msamiati wa Kiingereza na Kiswahili ili kuvirejelea kama vile *muchelek* (mchele), *magatiat* (mkate), *inganuk* (ngano) na *sukaruk* (*sukari*). Vyakula hivi havikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis.

Wakipsigis vilevile wamekopa msamiati kama vile *lanchi* na *sapa*. Misamiati hii inarejelea nyakati hizi zilirejelewa katika lugha hii kwa kutumia maelezo. *Lanchi* ilirejelewa kama *omitwogik chepo beet* ilhali *sapa* ilirejelewa kama *omitwogik chepo lang'at*. Sababu za ukopaji wa aina hii zimeelezwa katika sura ya tano.

**Jedwali 2.1.12. Msamiati wa Kinyumbani na samani**

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
Stool	<i>Stulit</i>	Kiti
Thermos	<i>Tamosit</i>	Themosi
Jug	<i>Chagit</i>	Jagi/dumu
Carton	<i>Katonit</i>	Katoni
Verandah	<i>Parandait</i>	Baraza
Frame	<i>Premit</i>	Kiunzi

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
Sahani	<i>Saniit</i>
Mlango	<i>Mlangoit</i>
Kikombe	<i>Kigombet</i>
Meza	<i>Meset</i>
Kitanda	<i>Kitandet</i>
Karai	<i>Karait</i>
Sufuria	<i>Sopuriet</i>
Kioo	<i>Kiyoit</i>
Bafu	<i>Papit</i>
Glass	<i>Kilasit</i>
Ghorofa	<i>Koropet</i>
Dirisha	<i>Tirisyet</i>
Saa	<i>Sait</i>
Picha	<i>Pichait</i>
Dakika	<i>Tagigait</i>
Chupa	<i>Chupoit</i>

Webb & Kembo-Sure (2000) wanaeleza kuwa lugha hazikopa msamiati wa kurejelea dhana za kimsingi. Hii ni kwa sababu kila lugha inajisimamia na kujitosheleza. Kwa hivyo ina msamiati wake wa kiasili wa kurejelea dhana za kimsingi. Hivi ndivyo hali ilivyo katika Kikipsigis. Hata hivyo, kuna vifaa vya kigeni ambavyo havikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis, vililetwa na wageni. Kwa hivyo, Wakipsigis walikopa msamiati wa kurejelea vifaa hivyo kama vile *sopuriet* (sufuria), *kilasit* (glass), *tamosit* (thermos) *n.k.*

Kimsingi, uainishaji huu wa msamiati mkopo umeonyesha kwamba Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka nyanja mbalimbali ambazo hazikuwepo katika utamaduni wake ili kuziba pengo la ukosefu wa msamiati kutokana na uingizaji wa vifaa na vyombo vipya/vya kigeni. Katika kufanya hivyo, Wakipsigis wameweza kuwasiliana na kupata njia za kurejelea dhana za kigeni.

Katika nyanja zilizokuwepo katika utamaduni wake, ilibainika kwamba msamiati uliokopwa hurejelea dhana za kileo ama fahiwa za kileo, kutokana na maendeleo ya kisasa. Sababu za ukopaji wa aina hizi zimejadiliwa katika sura ya tano.

## 2.2 Kategoria za Msamiati Mkopo katika Kikipsigis

### Jedwali. 1.2.1: Aina za maneno

Nomino	Vitenzi	Vivumishi	Vielezi	Viunganishi	Vihusishi	Vihisishi	Jumla
235	24	5	7	4	0	0	275

### Nomino

Katika utafiti huu, data iliyokusanywa ilibainisha kwamba asilimia kubwa ya msamiati mkopo ni nomino. Kwa mfano, kati ya maneno 275, maneno 235 ni nomino ambayo ni asilimia 86.4. Matokeo haya yanaelekea kuafikiana na ya Dzahene-Quarshie (2012) ambaye katika utafiti wake wa msamiati mkopo wa Kiingereza katika kurasa za michezo katika magazeti ya Kiswahili, alipata kwamba kati ya maneno yaliyokusanywa, nomino ilichukua asilimia 77.6. Hali hii huenda inatokana na kule kutumika kwa nomino sana katika mazungumzo au maandishi kuliko aina nyingine ya maneno. Katika semantiki, nomino huelezewa kama neno linalomtaja mtu, kitu au hali. Kijelezi hiki kinajumuisha idadi kubwa sana ya maneno ambayo kwa mujibu wa utendaji kazi; nomino hutenda, hutendwa na hutendewa katika sentensi. Katika sintaksia utendaji wa nomino katika sentensi hurejelewa kwa kutumia dhana za kiima, kipozi na kitondo. Kwa hivyo, uwezo wa nomino wa kuchukua nafasi

hizo katika muundo wa sentensi bila shaka ni thibitisho wazi kuwa matumizi yake yanayapiku matumizi ya aina nyingine ya maneno katika mawasiliano.

### **Vitenzi**

Kuhusiana na vitenzi, utafiti huu ulibanisha kwamba kati ya maneno 275, vitenzi vilikuwa 21 ambayo ni asilimia 7.7%. Idadi hii ndogo ya ukopaji wa vitenzi inaonyesha utoshelevu wa Kikipsigis kuhusiana na kategoria hii ya msamiati. Aidha, hata vitenzi vinavyokopwa vinawakilisha fahiwat tofauti kwa ulinganisho na kitenzi asili chenye uhusiano wa kisemantiki.

### **Vitenzi kutoka Kiswahili**

	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kitenzi asili</b>
i.	Chelewa	<i>Chelewan</i>	<i>Ekyi</i>
ii.	Chora	<i>Choran</i>	-
iii.	Pima	<i>Piman</i>	-
iv.	Ruka	<i>Rugan</i>	<i>Itwal</i>
v.	Cheza	<i>Chesan</i>	<i>Ureren</i>
vi.	Soma	<i>Soman</i>	-
vii.	Saidia	<i>Saitian</i>	<i>Toret</i>
viii.	Choma	<i>Choman</i>	<i>Peel</i>
ix.	sherehekea	<i>Syeregean</i>	<i>Boiboenchin</i>
x.	Chanja	<i>chanchan</i>	-
xi.	Jali	<i>Chalan</i>	<i>Mageenki</i>
xii.	Jaza	<i>Chasan</i>	<i>Inyit</i>
xiii.	Kaza	<i>Kasan</i>	<i>Igilgei</i>
xiv.	Laumu	<i>Laumen</i>	<i>Kitam</i>
xv.	lazimisha	<i>Lasimisan</i>	
xvi.	Ongoza	<i>Ongosan</i>	<i>Kindoo</i>
xvii.	Panga	<i>Pangan</i>	
xviii.	Vunja	<i>Punchan</i>	<i>Put</i>
xix.	Changa	<i>Changan</i>	<i>Iyum</i>

### Vitenzi kutoka Kiingereza

	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
i.	Type	<i>Taipen</i>	Kupiga taipu
ii.	Check	<i>Chegen</i>	Kukagua
iii.	Preach	<i>Pirichen</i>	Kuhubiri
iv.	Treat	<i>Tiriten</i>	Kutibu
v.	Spray	<i>Sipureen</i>	Kunyunyizia

Katika mifano hii tunaona kwamba Kikipsigis kimekopa vitenzi kutoka Kiswahili zaidi kuliko Kiingereza.

### Vivumishi

Katika utafiti huu, kati ya maneno 275 yaliyokopwa, vivumishi ni vitano, asilimia 1.8%. Vivumishi hivi hata hivyo vimekopwa kutoka lugha ya Kiswahili pekee. Hali hii inaonyesha kuwa lugha ina utoshelevu mkubwa kwenye kategoria hii ya maneno.

	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
<b>i.</b>	Mkora	<i>Magorayat</i>
<b>ii.</b>	Mrembo	<i>Muremboyot</i>
<b>iii.</b>	Goigoi	<i>Goigoyot</i>
<b>iv.</b>	Mjanja	<i>Muchanchayat</i>
<b>v.</b>	Kidogo	<i>Kitoko</i>

### Vielezi

Vielezi vimechukua asilimia 2.5% na vilevile vyote vilikopwa kutoka lugha ya Kiswahili.

	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
i.	Zaidi	<i>Saiti</i>
ii.	Kabisa	<i>Kapisa</i>
iii.	Ovyo ovyo	<i>Opyoopyo</i>
iv.	Haraka	<i>Araga</i>
v.	Ghafla	<i>Kapla</i>
vi.	Sana	<i>Sana</i>

## Viunganishi

Kati ya maneno 275 yaliyokusanywa, viunganishi ni 4 ambayo ni asilimia 1.5%.

Viunganishi hivi pia vimekopwa kutoka lugha ya Kiswahili pekee. Mfano:

	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
<b>i.</b>	Basi	<i>Pasi</i>
<b>ii.</b>	Lakini	<i>Lagini</i>
<b>iii.</b>	Tena	<i>Tena</i>
<b>iv.</b>	Alafu	<i>Alapu</i>

### 2.3 Hitimisho

Utafiti huu ulibainisha kwamba Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka lugha ya Kiingereza na Kiswahili katika nyanja mbalimbali. Msamiati huo hukopwa kujaza pengo la ukosefu wa msamiati wa kurejelea dhana geni. Hata hivyo, Kikipsigis kimekopa msamiati hata ikiwa kuna msamiati asilia kwa sababu mbalimbali kama vile kuongezea fahiwa mpya. Aidha msamiati mkopo ni mfupi na mahususi ukilinganishwa na msamiati asilia. Ufafanuzi wa sababu za ukopaji umeshughulikiwa katika sura ya tano. Kikipsigis kimekopa nomino kuliko aina nyingine ya maneno.



## SURA YA TATU

### MIFUMO YA KIFONOLOJIA

#### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tulilinganisha mifumo ya kifonolojia ya lugha bebwa: Kiswahili na Kiingereza, na lugha solo: Kikipsigis, ili tuweze kuelewa mchakato wa utohozi wa msamiati mkopo. Tulianza kwa kubainisha irabu, konsonanti na silabi katika Kikipsigis na kisha Kiswahili na Kiingereza. Sura hii ilituwezesha kubainisha namna irabu, konsonanti na hata silabi kutoka Kiswahili na Kiingereza hutoholewa ili kuuwezesha msamiati mkopo kutoka lugha hizi bebwa kukubalika katika Kikipsigis. Kwa mujibu wa Katamba (2000), msamiati mkopo hupitia utohozi wa kifonolojia na kimofolojia ili kuuwezesha msamiati huo kufuata mfumo wa kifonolojia na muundo wa silabi katika lugha pokezi.

Tulibainisha kwamba kuna ukosefu wa baadhi ya irabu na konsonanti katika Kikipsigis zilizopo katika lugha hizi bebwa, kwa hivyo, ili kuziba pengo hili, Kikipsigis hubadilisha sauti hizo zisizokuwepo kuwa zile zinazopatikana katika lugha hii ama zile zinazokaribiana kimatamshi bila kubadilisha maana ya msamiati husika.

Kwa hivyo, katika sura hii tumetoa maelezo kuhusu mifumo ya fonimu katika lugha zote tatu, miundo ya silabi katika lugha hizo ili kutuwezesha kuelewa utohozi wao katika sura ya nne inayojikita katika kubainisha namna irabu, konsonanti na silabi kutoka lugha bebwa hutoholewa inapoingizwa katika lugha solo ambayo ni Kikipsigis.

#### 3.1. Mfumo wa Fonimu katika Kikipsigis

Katika sehemu hii, tumebainisha fonimu katika Kikipsigis kwa kuanzia irabu kisha konsonanti na baadaye tukabainisha silabi zake.

### 3.1.1. Irabu katika Kikipsigis

Kwa mujibu wa Toweett (1979), Kikipsigis kina irabu kumi ambazo ni irabu-fonimu. Katika uanishaji wa irabu hizi, Toweett alizingatia urefu, ufupi, ukaze na uhafifu wa irabu. Katika utafiti huu, tulitazama irabu hizi za Kikipsigis kwa kuzingatia urefu na ufupi jinsi inavyobainika katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali 2: Mfumo wa irabu za Kikipsigis kwa mujibu wa Toweett (1979)**

Hafifu		Kaze		Hafifu		Kaze	
Fupi	Ndefu	Fupi	Ndefu	Fupi	Ndefu	Fupi	Ndefu
i	i:			u	u:		
		<i>i</i>	<i>i:</i>			<i>u</i>	<i>u:</i>
e	e:			o	o:		
		<i>e</i>	<i>e:</i>			<i>o</i>	<i>o:</i>
			a				<i>a</i>
			a:				<i>a:</i>

Tofauti na Toweett (kama hapo juu), Sang & Jerono (2012: 207) katika uanishaji wa fonimu zilizosawazishwa katika lahaja tatu za Kikalenjini (Kipsigis, Kitugen na Kinandi) wanaeleza kuwa Kikipsigis kina irabu tisa kama ilivyo katika Kinandi na Kitugen. Wanaeleza kuwa lahaja hizi tatu za Kikalenjini zina mfumo sawa wa irabu tisa kama ilivyo katika jedwali 2.

**Jedwali 3: Mfumo wa irabu za Kikipsigis kwa mujibu wa Sang na Jerono (2012)**

	Mbele	Katikati	Nyuma
Juu funge	i		u
Juu	I		U
Kati funge	e		o
Kati	ε		ɔ
Chini		<b>a</b>	

Katika uainishaji huu, Sang & Jerono (kama hapo juu) walizingatia msogeo wa ulimi na hivyo kuainisha irabu za juu, kati na chini kama ilivyo katika jedwali 2.

Irabu hizi zinadhihirika kwenye mifano ifuatayo:

**Jedwali 4: Mifano ya maneno ya irabu za Kikipsigis**

<b>Alama ya Kifonetiki</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
i	<i>pir</i>	Chapa
i:	<i>siir</i>	Kufaulu
I	<i>sir</i>	Andika
II	<i>siit</i>	Sugua
e	<i>ken</i>	Subiri
e:	<i>ke:r</i>	Kutazama
ε	<i>pet</i>	Kata
εε	<i>seer</i>	Tawanya
a	<i>am</i>	Kula
a:	<i>isyaach</i>	Sakura
u	<i>us</i>	Kunyanyasa
u:	<i>uus</i>	Kupangusa
ʊ	<i>uny</i>	Ficha
ʊʊ	<i>kuu</i>	Kutoa kitu
o	<i>pol</i>	Piga kelele
o:	<i>poor</i>	Putu
ɔ	<i>ton</i>	Kata
ɔ:	<i>soom</i>	Omba

Utafiti huu unakubaliana na Sang & Jerono (2012) kuwa Kikipsigis kina irabu tisa zilizoorodheshwa hapo juu . Irabu hizi ndizo zimezingatiwa katika utafiti huu.

**3.1.2 Mfumo wa Konsonanti katika Kikipsigis**

Toweett (1979) anaeleza kuwa Kikipsigis kina konsonanti kumi na nne ambazo ni konsonanti kumi na tatu bila kujumuisha kikwaruzo cha glota /h/. Konsonanti hizi zimeainishwa kwa kutegemea namna ya utamkaji na pahala pa utamkaji. Kwa kuzingatia namna ya utamkaji kuna aina zifuatazo za konsonanti: vipasuo, vikwaruzo,

vipasuo-kwaruzo, nazali, vimadende, kitambaza. Kwa kuzingatia mahali pa kutamkia kuna; vimidomo, viufizi, vikaakaa gumu, vikaakaa laini na vikoromeo.

Konsonanti hizi kwa ujumla ni p, t, k, m, n, s, ny, ng', ch, l, r, j na w. Toweett (kama hapo juu) amezianisha fonimu konsonanti hizi katika jedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali 5: Mfumo wa Konsonanti katika Kikipsigis Toweett 1979**

	Midomo	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	Koromeo
<b>Vipasuo</b>	p	t		k	
<b>Vikwaruzo</b>		s	j	w	h
<b>Vipasuo-kwaruzo</b>			c		
<b>Nazali</b>	m	n	ɲ	ŋ	
<b>Vitambaza</b>		l			
<b>Vimadede</b>		r			

Hata hivyo, tunahisi kwamba uainishaji huu wa Toweett (1979) kuhusu vikwaruzo /j/ na /w/ siyo sahihi kwani /j/ na /w/ vimerejelewa na wataalamu mbalimbali wa kiisimu kama vile Nchimbi (1979:628), Massamba na Wenzake (2004:44) kuwa ni viyeyusho. Hii ni kwa sababu sauti hizi si konsonanti wala irabu na mara nyingine hurejelewa kama nusu irabu. Viyeyusho hivi siyo irabu kamili kwa kuwa hazitamkiki na pia havina uwezo kama ule wa irabu wa kuunda silabi vinapounganishwa na konsonanti. Hii ina maana kwamba viyeyusho haviwezi kuchukua nafasi ya irabu kuunda kilele cha silabi lakini huweza kutumika kifonolojia kama konsonanti. Hata hivyo fonimu hizi siyo konsonanti kamili kwa kuwa katika utamkaji wake hakuna mzuio wa aina yoyote wa hewa. Hivyo basi sauti /j/ na /w/ ni viyeyusho wala sio vikwaruzo jinsi alivyoainisha Toweett (kama hapo juu).

Kwa upande mwingine Sang na Jerono (2012) wanaeleza kuwa Kikipsigis kina konsonanti kumi na sita jinsi ilivyo katika Kinandi na Kitugen ambapo tano ni vipasuo (p, t, d, c, k), tatu ni vikwamizo (s,β,ʎ), mne ni nazali (m, n, ɲ, ɳ), kitambaza kimoja(l), kimadede kimoja (r) na viyeyusho viwili (j, w).

Utafiti huu unakubaliana na Sang na Jerono (2012) kuwa sauti /β/ na /ʎ/ zinapatikana katika Kikipsigis ila hazikuainishwa na Toweett (1997). Vilevile utafiti huu unakubaliana na Sang na Jerono (kama hapo juu) kuhusu kuwepo kwa sauti /d/ kama konsonanti ya Kikipsigis. Sauti hii haikuainishwa na Towett. Katika utafiti wetu tulibainisha kwamba sauti hii hutokea katika mazingira maalum, kwa mfano katika msamiati asilia wa Kikipsigis, /d/ hutokea katika maneno yanayotanguliwa na kitambaza /l/ na nazali /m/. Kwa mfano katika msamiati asilia; ‘keldo’ (mguu), ‘keldet’ (jino), ‘poldet’ (wingu) na ‘oldo’ (mahali). Vilevile ‘tumdo’ (sherehe), ‘timdo’ (msitu) na ‘tumden’ (mwaga).

Kutokana na mielekeo ya watafiti hawa, tunakubaliana na Sang na Jerono (2012) kuwa kuna konsonanti ambazo Toweett (1997) hakuziainisha kama vile vipasuo ng’ong’o /<sup>m</sup>b/, /<sup>n</sup>d/ na /<sup>ɲ</sup>g/ ambazo pia hazijaainishwa katika jedwali la AKIKI lakini hupatikana katika Kikipsigis.

Utafiti huu ulitambua kuwepo kwa sauti /<sup>n</sup>c/ (nych)/ kama ilivyo katika neno asilia [nyanychet] na msamiati mkopo [kiwanychet] na vilevile sauti /<sup>s</sup>j/ kama ilivyo katika neno [isja:c], (kubeba begi mgongoni), [sja:m] (hali ya kupitia palipo nyasi ndefu). Hata hivyo uchunguzi wetu ulibainisha kuwa sauti hii /<sup>s</sup>j/ huweza kuwa ni zao la uyeyushaji kutokana na kule kufuatana kwa irabu **i** na **a** yaani **isi+ach**, **si+am** ambapo **i+a = y**. Kwa hivyo kuundwa kwa maneno isyaach na syaam.

Vilevile, ingawa Toweett (1979), aliainisha sauti [h] kama kikwaruzo cha glota katika Kikipsigis, utafiti wetu ulibainisha kuwa fonimu hii haipo katika konsonanti za Kikipsigis na ndio maana hudondoshwa inapotokea katika msamiati mkopo wa Kiswahili na Kiingereza unapoingizwa katika Kikipsigis. Kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
hoteli	<i>oteliit</i>
hekalu	<i>egaluut</i>
haraka	<i>araga</i>

Mifano hii basi inadhihirisha wazi kuwa konsonanti /h/ inadondoshwa kwa kuwa haipo katika Kikipsigis ili kukidhi mahitaji ya muundo wa maneno katika Kikipsigis na kuziba pengo linalotokana na konsonanti /h/ ambayo haipo katika Kikipsigis:

**/h/ → Ø**

Katika utafiti huu tunachukulia kwamba Kikipsigis kina konsonanti ishirini na moja, konsonanti hizi ambazo ni fonimu zimeorodheshwa kwa njia ifuatayo:

**Jedwali 6: Konsonanti za Kikipsigis**

<b>Alama ya kifonetiki</b>	<b>Othografia</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Tafsiri</b>
/p/	P	<i>pai</i>	lisha
/β/	b	<i>beek</i>	maji
/t/	t	<i>taaita</i>	kifungua mimba
/d/	d	<i>keldet</i>	jino
/k/	k	<i>ketit</i>	mti
/s/	s	<i>saa</i>	omba
/j/	y	<i>yoot</i>	kuinua kitu
/w/	w	<i>wal</i>	kubadilisha
/c/	ch	<i>cham</i>	penda
/ɣ/	g	<i>got</i>	nyumba
/m/	m	<i>mat</i>	moto
/n/	n	<i>nam</i>	kushika kitu
/ɲ/	ny	<i>nyei</i>	tafuna
/ŋ/	ng'	<i>ng'aal</i>	danganya
/l/	l	<i>lit</i>	noa
/r/	r	<i>riir</i>	lia
<sup>m</sup> b/	mb	<i>imbaret</i>	shamba
<sup>n</sup> d/	nd	<i>indaret</i>	nyoka
<sup>ɲ</sup> g/	ng	<i>ingoriet</i>	nguo
<sup>ɲ</sup> c/	nych	<i>nyanychet</i>	bahari
<sup>s</sup> j/	sy	<i>isyaach</i>	beba kitu mgogoni


### 3.2 Mfumo wa Fonimu Katika Kiswahili

#### 3.2.1 Irabu katika Kiswahili

Mfumo wa irabu katika Kiswahili umetafitiwa na wataalamu mbalimbali kama vile Ashton (1944:3), Polome (1967:38), Nchimbi (1992:2), Mgullu (1999:66), Massamba na wenzake (2004:38). Wataalamu hawa wameafikiana kuwa Kiswahili kina jumla ya fonimu za irabu tano ambazo ni /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/ na /u/.

Mchoro ufuatao unabainisha mahali fonimu hizi hutamkwa:

**Kielelezo. 1: Mahali pa kutamkia fonimu za irabu (Mgullu, 1999:66)**



Irabu hizi zinadhihirika katika maneno yafuatayo;

**Jedwali 7: Mfumo wa irabu katika Kiswahili**

Alama ya kifonetiki	Othografia	Kiswahili
a	a	Paa
ε	ε	Pea
i	i	Pia
ɔ	ɔ	Poa
u	u	Pua

**3.2.2 Mfumo wa konsonanti katika Kiswahili**

Wanaisimu mbalimbali wamefanya uchunguzi kuhusu konsonanti katika Kiswahili na uchunguzi wetu umebainisha kwamba wanaisimu hawa hawajakubaliana kuhusu idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili. Baadhi ya wanaisimu hawa ni kama vile Nchimbi (1979:628) ambaye alianisha konsonanti ishirini na tisa, Kapinga (1983:11) aliyeorodhesha konsonanti ishirini na tano, Mgullu (1999:69) aliainisha konsonanti ishirini na nne, Massamba na wenzake (2004:44) walianisha konsonanti ishirini na tisa.



Massamba na wenzake (2004) katika uanishaji wao, walieleza kuwa sifa muhimu ya kubainisha fonimu ni mpumuo kwa kuwa ni sifa bainifu katika Kiswahili sanifu, kwa hivyo, waliorodhesha sauti zifuatazo zilizo na mpumuo [ph,th,ch,kh]. Hata hivyo tunakubaliana na Mgullu (1999:70) kuwa, kuwepo au kutokuwepo kwa mpumuo katika baadhi ya konsonanti za Kiswahili sanifu halifai kuingizwa kwa sababu katika Kiswahili sanifu mpumuo hautumiwi kamwe kutofautisha maana za maneno kama unavyotumiwa, kwa mfano, katika lahaja za Kimvita. Kama mpumuo ungekuwa unatumiwa kutofautisha maana, bila shaka konsonanti yenye mpumuo ingekuwa ni fonimu tofauti na ile isiyo na mpumuo.

Katika uanishaji wa Nchimbi (1979), alipendekeza matumizi ya alama mpya zifuatazo;  $[\text{p}^h]$ ,  $[\text{b}^h]$ ,  $[\text{m}^h]$ , badala ya /mb/, /nj/, /ng/, /nd/. Katika pendekezo hili, Nchimbi alikusudia kuepuka tatizo la ujozi pweke na vilevile la uzidishaji wa visaidizi. Katika utafiti huu tunakubaliana na Nchimbi kuwa Kiswahili kina konsonanti ishirini na tisa jinsi inavyodhihrika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 8: Mfumo wa konsonanti katika Kiswahili (Nchimbi 1979:628)**

Aina	Midomo	Midomo- meno	Meno	Meno na ufizi	ufizi	Kaaka gumu	Kaaka laini	Glota
Vipasuo	p	b			t d		k g	
Vipasuo ng'ong'o	$^m\text{b}$				$^n\text{d}$	$^n\text{j}$	$^n\text{g}$	
Vikwamizwa		f v	$\theta$ $\delta$		s z	$\int$	$^v$	h
Nazali	m				n	$^n$	$\eta$	
Vizuiwa kwamizwa						c	j	
Kitambaza					l			
Kimadede					r			
Viyeyusho	w					j		

### 3.3 Mfumo wa fonimu katika Kiingereza

#### 3.3.1 Irabu za Kiingereza

**Jedwali 9: Mfumo wa irabu katika Kiingereza (Roca na Johnson, 1999 katika Osama A.G. (2004))**

	Mbele		Kati		Nyuma			
	Kaze	Hafifu	Kaze	Hafifu	Mviringo		Tandazi	
					Kaze	Hafifu	Kaze	Hafifu
Juu	i	I			u	ʊ		
Wastani		ɛ	ɜ	ə	ɔ			ʌ
Chini		æ				ɒ		ɑ


Kwa mujibu wa Roach (2000), Kiingereza kina irabu saba fupi [I, ʊ, ʌ, æ, ɒ, e, ə] irabu tano ndefu [i:, ɜ:, ɑ:, ɔ:, u:] na irabu unganifu nane [ Iə, eə, ʊə, eI, aI, ɔI, əʊ, əʊ]. Vile vile kina irabu tatu-unganifu.

**Jedwali 10: Mfumo wa irabu unganifu katika Kiingereza**

Alama Kifonetiki	ya	Othografia	Kiingereza		Tafsiri
<b>Irabu fupi</b>					
I		i	[pIt]	‘pit’	Shimo
ʊ		u	[pɒt]	‘put’	Weka
ʌ		u	[pʌt]	‘putt’	Pigampira kuelekea shimoni
Æ		a	[pæt]	‘pat’	Kikofi
ɒ		a	[pɒt]	‘pot’	Chungu
E		e	[pet]	‘pet’	Kipenzi
ə		e	[ʌpə]	‘upper’	Juu
<b>Irabu ndefu</b>					
i:			[ki:]	‘key’	Ufunguo
ɜ:			[kɜ:]	‘cur’	Mbwa koko
ɑ:			[kɑ:]	‘car’	Gari
ɔ:			[kɔ:]	‘core’	Kokwa
u:			[ku:]	‘coo’	Lia polepole

## Irabu unganifu katika Kiingereza

Roach (kama hapo juu) anaeleza kwamba katika Kiingereza irabu unganifu huhusisha msongeo wa irabu moja kuelekea kwa irabu nyingine ili ziweze kutamkwa kwa kuunganishwa. Kwa kuzingatia urefu wa utamkaji, irabu unganifu zina urefu kama wa irabu ndefu ila tu sehemu ya mwanzo wa irabu unganifu ni ndefu zaidi na huhitaji nguvu nyingi ya matamshi kuliko sehemu ya pili. Mifano ya irabu unganifu;



Mifano katika maneno;

### Jedwali 11: Maneno yaliyo na irabu unganifu katika Kiingereza

Alama ya kifonetiki	Kiingereza	Tafsiri
eI	beI	'bay' Ghuba
aI	baI	'buy' Nunua
ɔI	bɔI	'boy' Mvulana
Iə	pIə	'peer' Mwenzi aliye sawa
eə	peə	'pear' Pea
ʊə	pʊə	'poor' Masikini
əʊ	gəʊ	'go' Enda
aʊ	kaʊ	'cow' Ng'ombe

### 3.3.2 Mfumo wa Konsonanti katika Kiingereza

**Jedwali 12: Mfumo wa irabu katika Kiingereza: (Roach 2000)**

	Midomo	Midomo	Meno	Ufizi	meno-	Kaakaa	Kaakaa	glota	
	P	b		t	d	gumu	laini		
Vipasuo									
Vikwamizo		f	v	θ	ð	s	z	ʃ	ʒ
Viziuwa kwamizwa									h
Viyeyusho kimadende	w					r			j
Kitambaza									l
Nazali	m								n

Kimsingi, majedwali haya yanabainisha kuwa baadhi ya konsonanti zilizopo katika Kiswahili na Kiingereza hupatikana katika Kikipsigis. Hata hivyo, kuna konsonanti zinazopatikana katika lugha hizi mbili ilhali hazipo katika Kikipsigis. Kwa mfano, konsonanti /f/ na /v/ ambazo zipo katika Kiswahili na Kiingereza lakini hazipo katika Kikipsigis. Hivyo basi hali kama hii ina athari katika tukio la ukopaji jinsi inavyobainika katika sura ya nne.

### 3.4 Miundo ya silabi katika lugha zote tatu

Katika sehemu hii tumechunguza miundo ya silabi katika Kikipsigis, Kiswahili na Kiingereza kwa kuzingatia kwamba silabi ni kipashio muhimu kinachotumika kuelezea muundo wa lugha hasa katika kiwango cha fonolojia. Fonolojia ni kipengee cha taaluma ya isimu kinachojihusisha na mifumo ya sauti katika lugha yoyote na namna sauti hizo hufuata mpangilio maalum ili kuvijenga vipashio vikubwa zaidi kama silabi (Mgullu, 1999). Wanaisimu huamini kuwa ili kujenga vipashio hivi vikubwa, fonolojia ya lugha yoyote ile hutumika kama mfumo wa kuzipanga fonimu

za lugha hiyo katika utaratibu maalum ili kuunda vipashio hivyo vikubwa kama vile silabi.

Mgullu (1999) akimnukuu Fudge (1990) anaeleza kuwa silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho kwa ukubwa kipo kati ya fonimu na neno. Aghalabu silabi huwa ndefu zaidi kuliko fonimu lakini ndogo kuliko neno kamili. Vilevile silabi hutegemea lugha inayohusika. Kwa hivyo katika utafiti huu tumechukulia silabi kuwa tamko linaloundwa kwa fonimu moja au zaidi. Hivyo basi, uwezo wa kutambua mfuatano unaoruhusiwa na lugha fulani ni sehemu ya umilisi wa kifonolojia wa lugha hiyo kwani kila lugha ina muundo wake wa silabi jinsi inavyodhihirika katika lugha hizi tatu za utafiti huu.

### **3.4.1 Miundo ya silabi katika Kikipsigis**

Kama tulivyodokeza, silabi hurejelea kipashio cha utamkaji ambacho kwa kawaida ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno. Mgullu (1999) anaeleza kwamba silabi ni kipashio kimojawapo kinachotumika katika kuelezea muundo wa lugha hasa katika kiwango cha fonolojia arudhi na kwamba muundo wa silabi hutegemea lugha husika. Hivyo basi kila lugha ina muundo wake wa silabi na kwa hivyo, kipengele hiki kilifaa utafiti huu kwani ulituwezesha kubainisha namna msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza unavyoathiriwa na muundo wa silabi katika lugha ya Kikipsigis. Wanaisimu mbalimbali wanaeleza kuwa kunazo aina mbili ku za silabi; silabi wazi na silabi funge.

Kikipsigis kina muundo wa silabi wazi na funge. Silabi wazi hurejelea silabi zinazoishia kwa irabu. Kwa kuwa matamshi ya irabu huwa hayakatiki kwa ghafla kama yale ya konsonanti, basi silabi wazi huonekana kuwa huru au wazi zaidi. Silabi funge ni zile silabi ambazo huishia na konsonanti. Matamshi ya konsonanti huwa

hayaendelei kama yale ya irabu, hukatika ghafla na ndiyo maana zikaitwa silabi funge. Kikipsigis kina maumbo yafuatayo ya silabi:

### Silabi iundwayo kwa irabu pekee [I]

Irabu yoyote katika Kikipsigis ina uwezo wa kuunda silabi ya irabu pekee katika umbo la neno kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo. Silabi hizi huweza kutokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa maneno;

### Silabi inayoundwa kwa irabu /a/

	<b>Kikipsigis</b>		<b>tafsiri</b>
Mwanzoni:	<i>[a-nɛ]</i>	<i>ane</i>	mimi
Katikati	<i>[mi-a-cɛn]</i>	<i>miachen</i>	mambo mazuri

### Silabi iundwayo kwa irabu /ɛ/

	<b>Kikipsigis</b>		<b>tafsiri</b>
Mwanzoni:	<i>[ɛ-cɛg]</i>	<i>echeg</i>	sisi
Katikati	<i>[a-ɛŋ]</i>	<i>aeng</i>	mbili
Mwishoni	<i>[la-ɛ]</i>	<i>lae</i>	anabeba

### Silabi inayoundwa kwa irabi i/

	<b>Kikipsigis</b>		<b>Tafsiri</b>
Mwanzoni	<i>[i-nɛ]</i>	<i>inye</i>	wewe
Katikati	<i>[ma-i-nɛ-ndet]</i>	<i>mainendet</i>	sio yeye
Mwishoni	<i>[u-i]</i>	<i>ui</i>	nenda

**Silabi iundwayo kwa irabu /ɔ/**

	<b>Kikipsigis</b>		<b>tafsiri</b>
Mwanzoni:	<i>[ɔ-ba]</i>	oba	nendeni

**Silabi inayoundwa kwa irabu /u/**

	<b>Kikipsigis</b>		<b>tafsiri</b>
Mwanzoni	<i>[u-<sup>n</sup>]</i>	uny	ficha
Katikati	<i>[ta-u-net]</i>	taunet	mwanzo
Mwishoni	<i>[ke-u]</i>	keu	kuhama

**Silabi ya konsonanti na irabu [KI]**

Maneno yanayoundwa kwa konsonanti kisha irabu huchukua muundo huu wa KI.

Hudhihirika kupitia mifano ifuatayo:

	<b>Kikipsigis</b>		<b>tafsiri</b>
	<i>[kɔ-lɛ]</i>	<i>kole</i>	hivi
	<i>[lɔ-lɛ]</i>	<i>lole</i>	waka
	<i>[kɔ]</i>	<i>ko</i>	ndani
	<i>[mɔ-gɔ-rɛ-ni]</i>	<i>mogoreni</i>	anatajirika
	<i>[kɔ-nu]</i>	<i>konu</i>	leta

**Silabi inayoundwa kwa konsonanti pekee [K]**

Katika Kikipsigis, baadhi ya silabi huchukua muundo wa konsonanti pekee kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

	<b>Kikipsigis</b>		<b>tafsiri</b>
	<i>[chɔ-r-wɛt]</i>	<i>chorwet</i>	rafiki
	<i>[chɔ-m-yɛt]</i>	<i>chomyet</i>	upendo

### Silabi inayoundwa kwa konsonanti, irabu na konsonanti [KIK]

Kikipsigis vilevile ina muundo wa silabi wa KIK ambayo huunda silabi iliyo funge.

Muundo huu wa silabi hutokea mwishoni mwa takriban asilimia kubwa ya maneno katika lugha hii. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii:

<b>Kikipsigis</b>		<b>Tafsiri</b>
<i>[sal]</i>	<i>sal</i>	paka rangi
<i>[tar]</i>	<i>tar</i>	maliza
<i>[kwe-net]</i>	<i>kwenet</i>	katikati
<i>[la-gɔk]</i>	<i>lagok</i>	watoto
<i>[mat]</i>	<i>mat</i>	moto
<i>[let]</i>	<i>let</i>	mwisho
<i>[Kip-si-gis]</i>	Kipsigis	Kipsigis

### Silabi inayoundwa kwa konsonanti, konsonanti na irabu [KKI]

Baadhi ya maneno katika Kikipsigis pia huchukua muundo wa KKI kama inavyodhihirika katika maneno yafuatayo:

<b>Kikipsigis</b>		<b>Tafsiri</b>
<i>[a-si-sta]</i>	<i>asista</i>	jua
<i>[pi-stɔ-et]</i>	<i>pistoet</i>	ukosefu wa heshima
<i>[iste-gen]</i>	<i>istegen</i>	ondoka

### Silabi inayoundwa kwa nusu irabu na irabu (kI)

Hali hii hutokea katika maneno machache kama vile:

<b>Kikipsigis</b>		<b>Kiswahili</b>
<i>ki-wɔ-to</i>	<i>kiwito</i>	mpaka



### Silabi inayoundwa kwa konsonanti, nusu irabu na irabu [KkI]

Kikipigis vilevile ina muundo wa maneno yanayochukua muundo wa kononanti, nusu irabu [/w/ na /j/] na kisha irabu jinsi ilivyo katika mifano ifuatayo:

<b>Kikipigis</b>		<b>tafsiri</b>
<i>[mwa-i-ta]</i>	<i>mwaita</i>	mafuta
<i>[kɔ-bwa]</i>	<i>kobwa</i>	kufura
<i>[kɛ-ma-kyi]</i>	<i>kemakyi</i>	kutakia
<i>[kwɔ-ndɔ]</i>	<i>kwondo</i>	mwanamke
<i>[cwɛn]</i>	<i>chwen</i>	kuchapa

### Silabi ya irabu na konsonanti [IK]

Lugha hii pia ina muundo wa silabi wa irabu na konsonanti kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

<b>Kikipigis</b>		<b>tafsiri</b>
<i>[ak]</i>	<i>ak</i>	na
<i>[al-do]</i>	<i>aldo</i>	anauza
<i>[il]</i>	<i>il</i>	vunjika
<i>[kɛ-ɔm-<sup>n</sup>da]</i>	<i>keomnda</i>	kujaribu

Silabi ya IK katika lugha hii hutokea sana mwanzoni mwa maneno jinsi inavyodhihirika katika mifano tuliyotoa.

### 3.4.2 Miundo ya silabi katika Kiswahili

lugha ya Kiswahili ina miundo ifuatayo ya silabi:

#### Silabi zinazoundwa kwa irabu pekee [I]

Aina hii ya silabi huundwa kwa irabu pekee na huweza kutokea katika mazingira ya mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

Mwanzoni mwa neno:

<i>[u-a]</i>	katika	ua
<i>[ɔ-a]</i>	katika	oa
<i>[u-li-li-ma]</i>	katika	ulilima
<i>[a-na-i-ta]</i>	katika	anaita

Katikati ya neno:

Hali hii hutokea pale ambapo irabu mbili huwa zimefuatana katika neno bila kutengwa na konsonanti kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<i>[ba-a-da]</i>	katika	baada
<i>[u-a-si]</i>	katika	uasi
<i>[la-i-ni]</i>	katika	laini
<i>[ma-a-na]</i>	katika	maana

Mwishoni mwa neno;

Aina hii ya silabi hutokea wakati ambapo irabu ya mwisho katika neno imetanguliwa na silabi iliyo na irabu nyingine kwa mfano:

<i>[li-mi-a]</i>	katika	limia
<i>[ya-i]</i>	katika	yai
<i>[ki-u]</i>	katika	kiu
<i>[li-ma-u]</i>	katika	limau

### **Silabi za konsonanti na irabu [KI]**

Silabi za aina hii huundwa wakati ambapo konsonanti huungana na irabu ili kuunda tamko moja kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

<i>[ma-ma]</i>	katika	mama
<i>[ci-mba]</i>	katika	chimba
<i>[θe-la-θi-ni]</i>	katika	thelathini
<i>[ka-la-mu]</i>	katika	kalamu

Katika Kiswahili, muundo huu wa KI ndio ambao unatumiwa zaidi kuliko miundo mingine yote. Muundo huu wa silabi hata hivyo hupendelewa na sio tu katika Kiswahili bali pia katika lugha zote ulimwenguni.

### **Silabi zinazoundwa kwa konsonanti pekee [K]**

Katika Kiswahili vilevile kuna konsonanti zinazoruhusiwa kutamkika katika neno bila irabu. Konsonanti hizo huwa zile za aina ya nazali. Huwa na usonorati na hivyo kuweza kuunda kilele kinachotamkika na hivyo basi kusimama pekee kama silabi. Konsonanti hizi hata hivyo huwa silabi katika mazingira maalum au maneno maalum kwani sio lazima ziwe silabi za konsonanti moja kila wakati zinapotumika katika maneno. Mifano ya silabi za aina hii:

<i>[m-tu]</i>	katika	mtu
<i>[n-ci]</i>	katika	nchi
<i>[n-zi-gε]</i>	katika	nzige
<i>[a-li-m-pi-ga]</i>	katika	alimpiga

### **Silabi za konsonanti + nusuirabu + irabu**

Hii ni aina nyingine ya silabi za Kiswahili ambayo huundwa wakati ambapo konsonanti huungana na nusuirabu na irabu na kuunda kilele kimoja kwa pamoja. Katika muundo huu wa silabi, konsonanti ndizo huwa mwanzoni mwa silabi husika zikifuatwa na nusu irabu /w/ ama /j/ na kisha kufuatwa na irabu mwishoni kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<i>[m-pwa]</i>	katika	mpwa
<i>[<sup>n</sup>wε-lε]</i>	katika	nywele
<i>[mwa-ŋa]</i>	katika	mwanga
<i>[ji-pja]</i>	katika	jipya

### 3.4.3 Miundo ya silabi katika Kiingereza

Kwa mujibu wa Roach (2000), silabi huweza kuwa na sehemu zifuatazo; Mwanzo wa silabi, kilele cha silabi na mwisho wa silabi. Katika Kiingereza, kuna baadhi ya silabi zilizo na:

- Mwanzo wa silabi pekee kama vile; ‘key’ – [ki:] (ufunguo)
- Mwisho wa silabi pekee kama vile; ‘am’ - [æm] (mimi)
- Mwanzo na mwisho wa silabi kama vile; ‘run’ – [rʌn] (kimbia)

#### Silabi ya irabu moja pekee [I]

Aina hii ya silabi hutokea pale ambapo irabu moja hutumika kuunda silabi kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

Silabi		Kiingereza	tafsiri
[a]	katika	‘a’	-o,ote / mmoja
[ɔ:]	katika	‘or’	au

#### Silabi ya konsonanti na irabu [KI]

Aina hii ya silabi hutokea pale ambapo konsonanti inaungana na irabu kuunda tamko moja ambapo konsonanti hutangulia irabu kwa mfano;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[to]	‘to’	hadi

**Silabi ya irabu na konsonanti [IK]**

Silabi ya aina hii hutokea pale ambapo irabu inaungana na konsonanti ili kuunda tamko moja. Hapa irabu hutangulia konsonanti kama ilivyo katika mfano ufuatao;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[at]	at	kwa
[in]	in	katika

**Silabi ya irabu + konsonanti + konsonanti [IKK]**

Aina hii ya silabi hutokea pale ambapo irabu inaungana na konsonanti na kisha konsonanti nyingine ili kuunda silabi moja kwa mfano;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[ask]	'ask'	uliza

**Silabi ya konsonanti + irabu + konsonanti [KIK]**

Kiingereza huwa na silabi ya KIK ambapo aina hii ya silabi huwa na sehemu ya mwanzo ya silabi na sehemu ya mwisho kwa mfano;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[sæt]	<i>sat</i>	keti
[fil]	<i>fill</i>	jaza
[rʌn]	<i>run</i>	kimbia

**Silabi ya konsonanti + konsonanti + irabu [KKI]**

Aina hii ya silabi huwa na konsonanti mbili kabla ya irabu katika sehemu ya mwanzo wa silabi kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[stɪŋ]	<i>sting</i>	uma
[sməʊk]	<i>smoke</i>	moshi

**Silabi inayoundwa na konsonanti + konsonanti + irabu + konsonanti [KKIK]**

Katika aina hii ya silabi, konsonanti huungana na konsonanti pamoja na irabu na konsonanti nyingine ili kuunda silabi moja kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

silabi	Kiingereza	tafsiri
stɒp]	<i>stop</i>	maliza

**Silabi ya konsonant + irabu + konsonanti + konsonanti [KIKK]**

Katika Kiingereza, konsonanti huweza kuungana na irabu na konsonanti na kisha konsonanti nyingine ili kuunda silabi ya KIKK kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[salt]	salt	chumvi
[tank]	tank	tangi

**Silabi ya konsonanti + konsonanti + irabu + konsonanti + konsonanti [KKIKK]**

Katika aina hii ya silabi, konsonanti mbili huungana na irabu na kisha konsonanti mbili ili kuunda tamko au silabi moja kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

silabi	Kiingereza	tafsiri
[sticks]	sticks	vijiti

**Silabi ya konsonanti + irabu + konsonanti + konsonanti + konsonanti [KIKKK]**

Katika aina hii ya silabi, konsonanti huungana na irabu pamoja na konsonanti nyinginezo tatu ili kuunda tamko moja. Kwa mfano;

<b>silabi</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>tafsiri</b>
[bæŋks]	banks	benki
[twelfθ]	twelfth	sehemu ya kumi na mbili
[sandz]	sands	mchanga

Aina hii ya silabi huweza hata kuwa na konsonanti nne katika sehemu ya mwisho ya silabi kwa mfano;

<b>silabi</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>tafsiri</b>
[twelfθs]	Twelfths	sehemu za kumi na mbili
[prompts]	Prompts	kuchochea sana

### **Silabi ya konsonanti + konsonanti + konsonanti + irabu + konsonanti [KKKIK]**

Aina hii ya silabi hupatikana pale ambapo konsonanti tatu hungana na irabu na kisha konsonanti ili kuunda tamko moja. Hutokea katika maneno machache katika lugha hii kama vile;

<b>silabi</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>tafsiri</b>
[struck]	struck	piga
[split]	split	gawanya

Kimsingi sehemu ya mwanzo ya silabi za Kiingereza huweza kuwa na konsonanti moja, mbili au tatu. Silabi iliyo na konsonanti tatu katika sehemu ya mwanzo huanza kwa konsonanti /s/ mathalani; [split, stream, sky, square, struck]. Sehemu ya mwisho wa silabi huweza kuwa na konsonanti moja, mbili, tatu au hata nne.

Kwa kuwa kila lugha ina muundo wake wa silabi na jinsi anavyodai Mgullu (1996) kwamba silabi ni kipashio kimojawapo kinachotumika katika kuelezea muundo wa lugha hasa katika kiwango cha fonolojia arudhi, katika sehemu hii tumeainisha miundo ya silabi katika lugha zote tatu za utafiti huu ili kutuwezesha kubainisha namna msamiati ulio na muundo tofauti wa silabi katika lugha changizi huingizwa katika lugha pokezi.

Kutokana na uchunguzi huu wa fonimu na silabi katika lugha hizi tatu, tulibainisha kwamba pana upekee wa mfumo wa fonimu na silabi katika lugha hizi tatu. Kwa

hivyo,, ni kotokana na tofauti hizi ambapo msamiati wa Kiingereza na Kiswahili hufanyiwa mabadiliko mbalimbali ya kimofonemiki ili kuafikiana na mfumo wa kifonolojia na kimofolojia wa Kikipsigis.

### **3.5 Hitimisho**

Ilibainika kwamba mfumo wa fonimu katika lugha hizi tatu zinatofautiana kwa njia mbalimbali kwa mfano, kuna irabu na konsonanti zilizopo katika Kiingereza na Kiswahili lakini hazipo katika Kikipsigis kama vile irabu unganifu, irabu tatu-unganifu, vikwamizwa /f/, /v/, /θ/ na glota /h/ miongoni mwa mengine. Kwa kuzingatia silabi, Kiingereza na Kiswahili huruhusu mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno lakini Kikipsigis hakiruhusu. Sura hii ni muhimu katika kutuwezesha kufahamu namna Kikipsigis kinaposhughulikia tofauti hizi ili kuruhusu msamiati mkopo kukubalika katika mfumo wake wa kifonolojia.



## SURA YA NNE

### MABADILIKO YA KIMOFOFONEMIKI KATIKA MSAMIATI MKOPO WA KIKIPSIGIS

#### 4.0 Utangulizi

Katika sehemu hii tulichunguza namna msamiati mkopo kutoka Kiingereza na Kiswahili hutoholewa ili ufuate mfumo wa kifonolojia wa Kikipsigis. Utohozi hufanya msamiati mkopo kuchukua muundo wa msamiati katika Kikipsigis. Kwa hivyo tulijiuliza je utohozi unaathiri vipi irabu na konsonanti za lugha husika? Tulichunguza mabadiliko haya kwa kuzingatia utohozi wa fonimu ambapo tulianza kwa kuchunguza utohozi wa irabu na kisha utohozi wa konsonanti. Utafiti ulibainisha kwamba mabadiliko mbalimbali ya kimofonemiki hubainika katika utohozi wa fonimu kutoka lugha hizi mbili katika Kikipsigis.

#### 4.1 Utohozi wa Irabu za Kiingereza

Kiingereza kina irabu saba fupi [ɪ, ʊ, ʌ, æ, ɒ, e, ə] irabu tano ndefu [i:, ɜ:, ɑ:, ɔ:, u:] na irabu unganifu nane. Vile vile kina irabu tatu-unganifu. Kikipsigis kwa upande mwingine kina irabu tisa. Hali hii inabainisha kuwa kuna tofauti kati ya irabu za lugha hizi mbili ambapo kuna irabu zilizopo katika Kiingereza (kama vile irabu unganifu) lakini hazipo katika Kikipsigis. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza namna irabu hizi za Kiingereza hutoholewa katika Kikipsigis na je ni nini kinachoamua uteuzi wa irabu fulani kujaza pengo la irabu isiyokuwepo katika Kikipsigis. Tulibanisha kwamba utohozi wa fonimu irabu hutokea kupitia michakato ifuatayo:

#### 4.1.1 Ufupishaji wa irabu ndefu

Irabu ndefu hurejelea irabu zilizo na urefu kimatamshi zikilinganishwa na irabu fupi katika muktadha unaofanana (Roach 2000). Urefu wa irabu hutofautiana kulingana na muktadha wa matumizi kwa mfano aina ya sauti inayofuata irabu husika na vilevile kuwepo au kutokuwepo kwa mkazo.

Ilibainika katika utafiti huu kwamba irabu ndefu katika msamiati wa Kiingereza hufupishwa unapoingizwa katika Kikipsigis. Kwa mfano irabu ndefu /ɜ:/ hufupishwa kuwa irabu fupi /a/ au /ɔ/. Hali hii hutokana na kutokuwepo kwa irabu ndefu /ɜ:/ katika Kikipsigis. Mifano ifuatayo inathibitisha utohozi huu:

	/ɜ:/ → /a/		
<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>	
[nɜ:səri]	→	[nasaret]	‘nursery’
	ɜ: →	A	
[əɜ:məs]	→	[tamɔsit]	‘thermos’
	ɜ: →	a	
	/ɜ:/ → /ɔ/		
<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>	
[rizɜ:v]	→	[rɛsɔp]	‘reserve’
	ɜ: →	ɔ	

Irabu /ɜ:/ imebadilishwa kuwa /a/ kwa sababu irabu hizi mbili zinakaribiana kimatamshi ambapo irabu /ɜ:/, ni irabu ya kati-wastani ilhali /a/ ni irabu ya kati-chini. Hivyo basi irabu hizi mbili zina sifa ya kuwa ni irabu za kati.

Katika utohozi wa msamiati [rizɜ:v], irabu /ɜ:/ imebadilishwa kuwa /ɔ/ kwa kuwa Kikipsigis hakina irabu ndefu /ɜ:/. Kwa hivyo, irabu /ɜ:/ imebadilishwa kuwa /ɔ/ ili kuruhusu msamiati huu kukubalika katika Kikipsigis. Hii ni kwa sababu irabu hizi mbili ni irabu za kati ambapo /ɔ/ ni kati, nyuma ilhali /ɜ:/ ni kati mbele.

	<b>/u:/</b>	→	<b>/u/</b>	
<b>Kiingereza</b>				<b>Kikipsigis</b>
[sku:l]		→		[sugulit] ‘school’
	<b>u:</b>	→		<b>u</b>

	<b>/u:/</b>	→	<b>/u/</b>	
<b>Kiingereza</b>				<b>Kikipsigis</b>
[səlu:t]		→		[surut] ‘salute’
	<b>u:</b>	→		<b>u</b>

Katika utohozi wa msamiati [sku:l] na [səlu:t], irabu /u:/ katika Kiingereza ni irabu ndefu ya nyuma juu na haipatikani katika Kikipsigis. Kwa hivyo, kimebadilishwa kuwa irabu /u/ fupi inayotamkwa katika sehemu ya nyuma juu katika Kikipsigis. Irabu hizi mbili ni za nyuma juu ila tu /u:/ katika Kiingereza ni ndefu na kufupishwa kuwa irabu /u/ katika Kikipsigis.

#### 4.1.2 Usahilishaji wa irabu unganifu

Irabu unganifu hurejelea irabu mbili zinazotamkwa kwa kuunganishwa (TUKI 1990). Katika Kiingereza kuna irabu unganifu nane. Irabu hizi huingizwa katika Kikipsigis kwa kusahilishwa ili zikubalike katika mfumo wa kifonolojia wa Kikipsigis:

	<b>/eI/</b>	→	<b>/ε/</b>	
<b>Kingereza</b>				<b>Kikipsigis</b>
[freIm]		→		[prεmit] ‘frame’
	<b>eI</b>	→		<b>ε</b>
[reIdiəv]		→		[rεtiɔ] ‘radio’
	<b>eI</b>	→		<b>ε</b>
	əv	→		ɔ
[ləvkeIʃən]		→		[lɔkεsʃən] ‘location’
	əv	→		ɔ
	<b>eI</b>	→		<b>ε</b>

Katika mifano hii irabu unganifu /eI/ imesahilishwa kuwa irabu /ε/ katika Kikipsigis kupitia mchakato wa kusahilisha irabu unganifu kwa kuwa Kikipsigis hakina irabu unganifu.

	/əʊ/	→	/ɔ/	
<b>Kingereza</b>				<b>Kikipsigis</b>
[əʊtəl]		→	[ɔteliit]	‘hotel’
	əʊ	→	ɔ	
[ləʊkəlʃən]		→	[ləkəsʃən]	‘location’
	əʊ	→	ɔ	

Katika mifano hii, tulibainisha kuwa utohozi wa irabu unganifu /əʊ/ kuwa /ɔ/ huenda unatokana na orthografia wa msamiati mkopo katika Kiingereza. Kwa hivyo, maneno haya yametoholewa kulingana na fonolojia wa maneno haya katika Kiingereza. Kwa kuwa Kikipsigis hakina konsonanti /h/, basi inadondoshwa na ndio maana neno (hotel) likakopwa kuwa [oteliit].

	/aɪ/	→	/ai/	
<b>Kingereza</b>				<b>Kikipsigis</b>
[baɪbl]		→	[baibol]	Bible
	aɪ	→	ai	
[daɪrɛktə]		→	[taɪrɛktayət]	Director
	aɪ	→	ai	

Katika mifano hii, tunaona kwamba irabu unganifu / aɪ/ imesahilishwa kuwa irabu mbili zinazofuatana ai. Hii ni kwa sababu Kikipsigis hakina irabu unganifu lakini kinaruhusu irabu mbili kufuatana, kwa hivyo katika utohozi wa irabu hii unganifu, Kikipsigis kimeisahilisha kuwa irabu zinazokaribiana kimatamshi. Irabu za aina hii hupatikana katika maneno asilia ya Kikipsigis kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Taita</i>	kifungua mimba
<i>Baibai</i>	kuwa na furaha
<i>Kainet</i>	jina
<i>Baisiet</i>	kazi

Hali hii vilevile ilibainika katika utohozi wa irabu unganifu /aʊ/ kuwa irabu mbili zinazofuatana /aʊ/ jinsi ilivyo katika mfano ufuatao:

/aʊ/ → /aʊ/  
[taʊn] → [taʊnit]

**aʊ → aʊ**

Irabu **aʊ** zinazofuatana hukubalika katika Kikipsigis jinsi ilivyo katika msamiati asilia kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>maonatet</i>	utabiri
<i>maotiot</i>	mtabiri
<i>maone</i>	hafukuzi

**/aʊ/ → /a/**

Tulibainisha vilevile kwamba katika baadhi ya maneno, irabu unganifu /aʊ/ husahilishwa kuwa irabu /a/ jinsi ilivyo katika mifano ifuatayo:

/aʊ/ → /a/		
[kaʊnsələ]	→ [kansolayat]	councilor
[kaʊnsl]	→ [kansol]	council

### 4.1.3 Uyeyushaji

Uyeyushaji hurejelea mchakato wa kuundwa kwa Kiyeyusho /j/ ama /w/ katika neno. Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa msamiati mkopo kutoka Kiingereza ulio na irabu tatu-unganifu hutoholewa kwa kuundwa kwa kiyeyusho kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

/aɪə/ → /aja/		
<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	
[daɪəri]	→ [tajari]	‘diary’
[aɪə]	→ [aja]	
[kwaɪə]	→ [kwaja]	‘choir’
[aɪə]	→ [aja]	

Mifano hii inabainisha kuwa irabu tatu-unganifu [aIə] inatoholewa kupitia kuundwa kwa kiyeyusho kati ya irabu husika [aja].

Katika mifano hii, tuligundua vilevile kwamba kunatokea uimarikaji wa irabu ambapo irabu /I/ ambayo ni mojawapo wa irabu tatu-unganifu, imebadilishwa kuwa nusuirabu /j/. Fonimu za irabu huimarika wakati ambapo irabu husika hubadilika na kuwa nusu irabu. Kwa kuwa irabu /I/ hutumia nguvu hafifu wakati wa kutamka, inapobadilishwa kuwa /j/ inayotumia nguvu nyingi katika utamkaji wake, basi tunasema kwamba irabu /I/ imeimarika kwa kubadilishwa kuwa nusuirabu /j/.

#### 4.1.4 Muungano wa irabu

Muungano wa irabu ni mchakato unaotokea wakati ambapo irabu zinaathiriana na irabu moja kupoteza sifa zake zote bainifu kwa irabu jirani au pengine irabu zote mbili kuungana na kuzua alofoni mpya ya fonimu inayohusika (Habwe na Karanja 2004). Katika utafiti huu, tulibainisha kwamba irabu tatu-unganifu hutoholewa kupitia kwa kuunganishwa kwa irabu mbili kati ya hizo tatu-unganifu kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

$$/Iəv/ \rightarrow /iə/$$

Aina hii ya irabu tatu-unganifu hutokea mwishoni mwa neno jinsi ilivyo katika msamiati radio. Irabu hizi unganifu [Iəv], hutoholewa kuwa [iə] kupitia kuunganishwa kwa irabu mbili za mwisho, yaani [əv] kuwa [o] ili kuunda irabu [iə] inayokubalika katika Kikipsigis kama ilivyo katika mfano ufuatao;

Kiingereza		Kikipsigis	
[reIdiəv]	→	[retio]	‘radio’
[Iəv]	→	[iə]	

Kutokana na utohozi wa irabu tatu-unganifu katika 4.1.3 na 4.1.4. tunaona kwamba msamiati mkopo ulio na irabu tatu-unganifu hutoholewa kupitia ama uyeyushaji au muungano wa irabu.

## 4.2 Utohozi wa Irabu za Kiswahili

Kiswahili kina jumla ya irabu tano ambazo ni /a/, /ε/, /i/, /o/ na /u/ ilhali Kikipsigis kina irabu kumi. Hapa tunaona kwamba irabu hizi tano za Kiswahili zinapatikana katika Kikipsigis. Utafiti ulibainisha mabadiliko yafuatayo katika utohozi wa irabu za Kiswahili:

### 4.2.1 Uchopezi wa irabu

Uchopezi ni utaratibu wa kifonolojia unaotumika kudhibitia mpangilio halali wa sauti katika lugha yoyote iwayo kupitia uingizaji wa irabu, konsonanti au kiyeyusho katika msamiati (Kadurenge, 1995:96). Kwa hivyo katika mchakato huu, irabu huingizwa katika sehemu fulani ya neno linalokopwa ili kulifanya neno hilo kufuata mfumo wa kifonolojia wa lugha husika. Hali hii hutokea katika Kikipsigis jinsi inavyobainika katika mifano ifuatayo:

### Uchopezi wa irabu kati ya konsonanti mbili au zaidi zinazofuatana

Katika Kikipsigis, uchopekaji wa irabu hutokea katika msamiati mkopo ulio na konsonanti mbili au zaidi zinazofuatana mwanzoni mwa neno k.v.

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
[mceɛɛ]	[ <i>mu</i> ceɛɛk]
[mkateɛ]	[ <i>ma</i> gatiat]
[mkɔra]	[ <i>ma</i> ɔrajat]
[mʃahara]	[ <i>mu</i> sjara]
[stima]	[ <i>si</i> timet]

Katika mifano hii, tunaona kuwa uchopezi wa irabu huathiri maneno yanayoanzia kwa nazali /m/ na kufuatwa na konsonanti nyingine, kwa hivyo irabu huchopekwa ili kuruhusu msamiati mkopo kufuata muundo wa maneno katika Kikipsigis.

### **Uchopezi wa irabu mwanzoni mwa msamiati**

Katika kutohoa msamiati wa Kiswahili unaonza kwa fonimu /<sup>n</sup>g/ na /<sup>n</sup>d/, Kikipsigis huchopeka irabu /i/ mwanzoni, yaani kabla ya fonimu hizo. Kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
ndizi	<i>indisiɔt</i>
ndege	<i>indegeit</i>
ngazi	<i>ingasit</i>
nguo	<i>ingɔriet</i>

Ilibainika vile vile kwamba msamiati unaoanza kwa konsonanti /m/ na kufuatwa na konsonanti /p/ kama vile neno mpaka, unapokopwa katika Kikipsigis, irabu /i/ huchopekwa mwanzoni kama ilivyo katika mifano ifuatayo

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
mpaka	<i>imbagait</i>
Mpira	<i>imbiret</i>

Uchopezi wa aina hii hutokea kwa sababu Kikipsigis hakina mfuatano wa konsonanti /m/ na /p/. Kwa hivyo hubadilishwa kuwa /<sup>m</sup>b/ na kutanguliwa na irabu /i/ inayochopekwa mwanzoni. Hali hii ipo katika msamiati asilia wa Kikipsigis kwa mfano:

<b>Kikipsigis</b>	<b>tafsiri</b>
<i>imbareɪt</i>	shamba
<i>imbɔcɛt</i>	shangazi
<i>imbɔlɔkyat</i>	aina ya tunda la mwituni unaofanana na tikitimaji
<i>imbɔrɔcɔt</i>	aina ya mboga ya kienyeji



#### 4.2.2 Kuafikiana kwa irabu

Mchakato huu hurejelewa pia kama tangamano la irabu. Kuafikiana kwa irabu ni ule utaratibu wa irabu fulani kukubali kuandamana katika mazingira maalum (Mgullu 1999:92). Tulibainisha kwamba utaratibu huu katika Kikipsigis husababishwa na irabu iliyo mwishoni mwa msamiati mkopo ambapo;

- Ikiwa irabu /a/ hutokea mwishoni mwa msamiati unaokopwa, basi utohozi wake huchukua silabi /ait/
- Ikiwa irabu /u/ ama /ɔ/ hutokea mwishoni mwa msamiati unaokopwa, basi utohozi wake huchukua silabi /oit/

Hali hizi zinadhihirika kupitia mifano ifuatayo;

Msamiati mkopo ulio na irabu /a/

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
Picha	→	<i>pichait</i>
Saa	→	<i>sait</i>
chama	→	<i>chamait</i>
Chupa	→	<i>chupait</i>

Msamiati mkopo ulio na irabu /u/ ama /ɔ/

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
Simu	→	<i>simɔit</i>
Kilo	→	<i>kilɔit</i>
Pingu	→	<i>pingɔit</i>

Hata hivyo, data ya utafiti huu ilibainisha kwamba kuna msamiati unaoishia kwa irabu hizi lakini hazifuati utaratibu huu wa tangamano la irabu kama vile;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
Nyanya	→	<i>nyanyat</i>
Chuma	→	<i>chumɔyɔt</i>
Kitabu	→	<i>kitaput</i>
Elfu	→	<i>eliput</i>
Bafu	→	<i>papit</i>

Hali hii ya msamiati kukosa kufuata utaratibu huu kwa maoni yetu pengine ni suala la ughairi ambapo umbo linakosa kufuata utaratibu unaotarajiwa wa kuafikiana kwa irabu.

Katika kuangazia mchakato huu wa kuafikiana kwa irabu, tuliweza kubainisha vilevile kwamba **mvutano wa irabu** hutokea katika baadhi ya msamiati kama inavyobainika ifuatavyo;

#### 4.2.3 Mvutano wa irabu

Kama tulivyoeleza hapo awali, msamiati mkopo ulio na irabu /a/ mwishoni, hutoholewa kuwa na silabi /ait/, hata hivyo katika baadhi ya msamiati, kwa mfano msamiati ‘kanisa’ unapokopwa hubadilishwa kuwa ‘kaniset’ ilhali tungetaraji ‘kanis**ait**’. Hali hii hutokana na mchakato wa mvutano wa irabu.

Irabu huvutana wakati ambapo irabu zimetokea kwa kufuatana ilhali irabu moja labda ni ya juu na nyingine ni ya chini (Mgullu, 1999). Katika hali kama hiyo irabu hizo huvutana kiasi kwamba ile irabu ya juu inavutwa chini kidogo na ile ya chini inavutwa juu kidogo. Kwa hivyo, irabu inayotokea haitakuwa ya juu wala chini bali itakuwa ya kati. Katika Kikipsigis, mvutano wa irabu hutokea kati ya irabu /a/ ambayo ni ya chini na irabu /i/ ambayo ni ya juu. Mvutano huu hivyo basi huleta sauti moja tofauti ambayo ni irabu /ε/ iliyo kati ya irabu /a/ na /i/ kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
daraja	→ <i>taraca+it</i>	→ <i>taracεt</i>
Barua	→ <i>barua + it</i>	→ <i>baruεt</i>
kanisa	→ <i>kanisa + it</i>	→ <i>kaniseεt</i>
kitanda	→ <i>kitanda + it</i>	→ <i>kitandεt</i>
Duka	→ <i>tuga + it</i>	→ <i>tugεt</i>
sitima	→ <i>sitima + it</i>	→ <i>sitimεt</i>

askari	→	<i>asigorinda + it</i>	→	<i>asigorindet</i>
barabara	→	<i>parapara + it</i>	→	<i>paraparət</i>
kikombe	→	<i>kigomba + it</i>	→	<i>kigombet</i>

#### 4.2.4 Udondoshaji wa irabu

Udondoshaji kuwa hali ya kipashio cha neno; irabu, konsonanti au silabi kutoweka kabisa katika mazingira maalum ya kifonolojia au ya kimofonemiki (Aswani 1995:61). Irabu hudondoshwa kwa sababu ya kuvunja mfuatano wa irabu katika msamiati ili kuudhibiti muundo wa silabi au ili kurahisisha matamshi na hivyo kuharakisha matamshi na mazungumzo. Hali hii hutokea Kikipsigis kinapotohoa msamiati kutoka Kiswahili ili kuruhusu msamiati huo kukubalika katika mfumo wa kifonolojia wa Kikipsigis.

Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa katika msamiati mkopo ulio na irabu mbili zinazofuatana, Kikipsigis hudondoa irabu zote mbili au moja kati ya hizo irabu na kisha kuchopeka irabu nyingine. Kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
<b>baiskeli</b>		<i>pɔskilit</i>
<b>[ai]</b>	→	<b>[ɔ]</b>
<b>[e]</b>	→	<b>[i]</b>
<b>saa</b>		<i>Sait</i>
<b>[a]</b>	→	<b>[i]</b>

Katika [baiskeli] Kikipsigis hudondoa irabu zote mbili zinazofuatana, yaani /a/ na /i/ na kisha kuchopeka irabu /ɔ/, ilhali katika [saa], Kikipsigis hudondoa irabu moja /a/ na kuchopeka irabu /i/.

### Udondoshaji wa irabu iliyo kati ya konsonanti

Vilevile kuna udondoshaji wa irabu katika msamiat ulio na irabu baina ya kimadende /r/ na kipasuo /k/ au kimadende /r/ na kipasuo /t/ kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
serikali	→	<i>sergalit</i>
	i →	∅
Korokoroni	→	<i>korgoret</i>
	o →	∅
Karatasi	→	<i>kartasit</i>
	a →	∅

### Udondoshaji wa irabu mwishoni mwa msamiati

Udondoshaji wa irabu mwishoni mwa neno hutokea ili kuufanya msamiati mkopo kukubalika katika mfumo wa Kikipsigis. Hii ni kwa sababu Kikipsigis hupendelea silabi funge. Kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
nafasi	<i>napas</i>
kabati	<i>kapat</i>
lami	<i>lam</i>

### Udondoshaji wa irabu /u/ mwanzoni mwa msamiati mkopo

Utafiti huu ulibainisha vilevile kwamba Kikipsigis hudondoa irabu /u/ katika msamiati wa Kiswahili unaoanza kwa irabu hiyo. Tazama mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
uwanja		<i>kiwancet</i>
	u →	∅
Usomaji		<i>somanet</i>
	u →	∅

#### 4.2.5 Uyeyushaji

Uyeyushaji hurejelea mabadiliko yanayokumba irabu ambapo irabu hubadilishwa kuwa nusu irabu. Mabadiliko haya hutokea katika mchakato wa utohozi ambapo irabu mbili tofauti zinapofuatana katika mazingira yasiyoruhusiwa katika Kikipsigis, hubadilishwa kuwa nusu irabu kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
Mwalimu	<i>mwalimu + iɔt</i>	→ <i>mwalimuyot</i>
Fundi	<i>pundi + ɔt</i>	→ <i>pundiyot</i>
Mkora	<i>magɔra + iat</i>	→ <i>magɔrayat</i>
Mjahara	<i>musi + ara</i>	→ <i>musyara</i>
chuma	<i>chumɔ + iɔt</i>	→ <i>chumyɔt</i>
dakika	<i>tagiga + iat</i>	→ <i>tagigayat</i>
malaika	<i>malaiga + iat</i>	→ <i>malaigayat</i>

Mifano hii imedhihirisha kwamba uyeyushaji hutokea katika baadhi ya msamiati mkopo kutoka Kiswahili ili kuepuka mfululizo wa irabu tatu. Hata hivyo ni vyema kutaja kwamba irabu hizi hubadilika kuwa viyeyusho bila kubadili maana ya msamiati husika.

#### 4.3 Utohozi wa konsonanti kutoka Kiingereza

##### 4.3.1 Kuimarika kwa fonimu konsonanti

Mgullu (1999), anaeleza kuwa utafiti wa muda mrefu uliofanywa na wanafonetiki katika maabara umethibitisha ya kuwa nguvu anazotumia mtu wakati anapotamka fonimu mbalimbali hutofautiana kutegemea aina ya sauti anayoitamka. Ziko fonimu ambazo huhitaji nguvu zaidi na zingine huhitaji nguvu kidogo. Baada ya utafiti, wanafonetiki walihitimisha ya kuwa nguvu zinazotumika kutamka fonimu zinaweza kupangwa kuanzia juu kwenda chini jinsi ilivyo katika orodha ifuatayo:

1. Vipasuo hafifu/isoghuna k.v. /p/, /t/, /k/
2. Vipasuo ghuna k.v. /b/, /d/, /g/
3. Vizuiwa kwamizwa isoghuna k.v. /c/
4. Vizuiwa kwamizwa ghuna k.v. /j/
5. Vikwamizo isoghuna k.v. /f/, /s/, /θ/
6. Vikwamizo ghuna k.v. /v/, /z/, /ð/
7. Vimadende k.v. /r/
8. Vitambaza k.v. /l/
9. Nusu irabu k.v. /j/, /w/
10. Irabu k.v. /a/, /u/

Orodha hii ina ngazi kumi kutoka ya juu (ya kwanza) inayotumia nguvu nyingi zaidi hadi ya chini (kumi) inayotumia nguvu kidogo. Orodha hii pia inadhihirisha kwamba vitamkwa visivyokuwa na mghuno hutumia nguvu zaidi kuliko vile vilivyo na mghuno. Kwa hivyo, sauti fulani huwa imeimarika kama inakuwa imebadilika kutoka kwenye aina ya sauti ambayo hutumia nguvu kidogo zaidi na kuwa sauti ambayo inatumia nguvu nyingi zaidi.

Hali hii hutokea katika Kikipsigis wakati ambapo kinapokopa msamiati ulio na konsonanti zisizopatikana katika Kikipsigis. Konsonanti hizi ni kama vile /d/, /f/, /v/, /z/, /θ/, /ð/, /j/ na /v/. Sauti hizi hubadilishwa kwa zile sauti zilizopo katika Kikipsigis zinazokaribiana katika utamkaji. Kwa kufanya hivi, sauti hizo huweza kuimarika ama kudhoofika kwa kutegemea kiasi cha nguvu za misuli na msukumo wa mkondohewa katika utamkaji wa konsonanti hizo. Mifano ya mabadiliko yanayosababisha kuimarika kwa konsonanti ni zifuatazo:

**i. Vikwamizo (-ghuna) → vipasuo (-ghuna)**

Kulingana na orodha ya Mgullu hapo juu, vikwamizo visivyo na mghuno viko chini katika ngazi ya tano ilhali vipasuo visivyo na mghuno viko juu katika ngazi ya

kwanza. Basi kikwamizo kimebadilika kutoka ngazi ya chini inayotumia nguvu kidogo hadi ngazi ya juu inayotumia nguvu nyingi. Kwa hivyo, kubadilika kwa kikwamizo (-ghuna) hadi kwa kipasuo (-ghuna) ni tendo la kuimarika kwa fonimu kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

/f/ → /p/

Sifa zao bainifu ambazo zinajitokeza ni zifuatazo;

/f/	/p/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kipasuo
+midomo-meno	+midomo
-mghuno	-mghuno

Kutokana na sifa hizi bainifu, /f/ inatofautiana na /p/ katika sifa ya aina na mahali pa kutamkia, ambapo /f/ ni kikwamizo na hutamkwa kwenye midomo meno ilhali /p/ ni kipasuo na hutamkwa kwenye midomo. Kwa hivyo, Sauti /f/ ambayo ni kikwamizo cha midomo meno haipo katika Kikipsigis, hivyo basi inapotokea katika msamiati wa Kiingereza unaoingizwa katika Kikipsigis, hubadilishwa na kuwa /p/ ambayo ni kipasuo cha midomo na hivyo kuimarika kwa mfano;

<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
factory	→	<i>paktəri</i>
forest	→	<i>pɔrɔste</i>
professor	→	<i>prɔpɛsa</i>
Fine	→	<i>pain</i>
form	→	<i>pɔmit</i>
referendum	→	<i>rɛparendam</i>
/θ/	→	/t/

Sauti /θ/ na /t/ zinabainishwa na sifa bainifu zifuatazo;

/θ/	/t/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kipasuo
+meno	+ufizi
-mghuno	-mghuno

Sauti hizi zinatofautiana katika sifa ya aina ya fonimu na mahali pa kutamkia ambapo, /θ/ ni kikwamizo cha meno ilhali /t/ ni kipasuo cha ufizi. Kwa sababu sauti /θ/ haipo katika Kikipsigis, msamiati mkopo ulio na sauti hii hubadilishwa kuwa /t/ kwa sababu sauti /t/ hukaribia sauti /θ/ kimatamshi kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
θermos	→	<i>tamɔsit</i>
Θeatre	→	<i>tietā</i>

**ii. Vikwamizo (+ghuna) → vipasuo (-ghuna)**

Kikwamizo kilicho na mghuno kipo katika ngazi ya sita na kinapobadilishwa kuwa kipasuo kisicho na mghuno huwa imeimarika kama ilivyo katika mfano ufuatao:

/v/ → /p/

Sauti hizi zina sifa zifuatazo bainifu;

/v/	/p/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kipasuo
+midomo meno	+midomo
+mghuno	-mghuno

Sauti /v/ ambayo ni kikwamizo kinachotamkwa wakati mdomo wa chini ukiwa umegusa meno ya juu, hubadilishwa kuwa /p/. Sauti /v/ ni sauti ghuna ilhali /p/ ni sauti isoghuna na kwa kuwa sauti isoghuna ina nguvu matamshi kuliko sauti ghuna, basi /v/ kubadilishwa kuwa /p/ huifanya kuimarika. Kwa mfano;



<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
reverend	→	<i>reparen</i>
driver	→	<i>inderepa</i>
gɔrvənər	→	<i>kapana</i>
televiʒən	→	<i>telepisiɔn</i>
verandah	→	<i>paranda</i>

**iii. Vipasuo (+ghuna) → vipasuo (-ghuna)**

**/g/ → /k/**

Sauti hizi zina sifa zifuatazo bainifu;

/g/	/k/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+kaakaa laini	+kaakaa laini
+mghuno	-mghuno

Kutokana na sifa hizi, tunaona kwamba sauti hizi zina sifa zinazofanana isipokuwa katika sifa ya mghuno ambapo /g/ ni sauti iliyo na mghuno ilhali /k/ ni sauti isiyokuwa na mghuno. Mabadiliko haya hufanya /g/ kuimarika kuwa /k/ kwa sababu sauti kuwa na mghuno au kutokuwa na mghuno hutegemea jinsi mkondohewa kutoka mapafuni hupita katikati ya nyuzi za sauti. Kwa hivyo, sauti /k/ iliyo katika ngazi ya kwanza katika orodha ya Mgullu (1999) hapo juu, haina mghuno na ina nguvu katika matamshi kuliko sauti /g/ iliyo na mghuno na iliyo katika ngazi ya pili, hivyo basi kuimarika. Mifano;

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
glass	→	<i>kilasit</i>
gɔrvənər	→	<i>kapana</i>
grəʊp	→	<i>kurupit</i>
gəzɪt	→	<i>kasetit</i>
ɡoʊl	→	<i>kɔl</i>
ɡreɪd	→	<i>Kiretit</i>

Data ya utafiti huu ilibainisha kwamba hali hii ya sauti /g/ kubadilishwa kuwa /k/ hutokea pale ambapo sauti /g/ huja mwanzoni mwa msamiati kama ilivyo katika mifano tuliotoa hapo juu. Hata hivyo sauti hii /g/ itokeapo katikati au mwishoni mwa neno hali huwa tofauti kwani sauti hiyo /g/ hubaki kuwa /g/ kwa mfano:

<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
<i>Jug</i>	→	<i>chagit</i>
<i>Sugar</i>	→	<i>sugaruk</i>

**/d/→/t/**

Sifa bainifu za sauti hizi ni zifuatazo;

/d/	/t/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+ufizi	+ufizi
+mghuno	-mghuno

Sauti /d/ ni kipasuo cha ufizi na vile vile /t/ ni kipasuo cha ufizi. Kwa sababu Kikipsigis hakina sauti /d/, kinapokopa msamiati kutoka Kiingereza ulio na sauti /d/, konsonanti hii hubadilika kuwa /t/. Hii ni kwa sababu sauti hizi zinakaribiana kimatamshi. Hata hivyo, /d/ ni sauti ghuna ilhali /t/ sio ghuna hivyo basi kubadilishwa kwa /d/ kuwa /t/ huifanya sauti hii kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
director	→	<i>tairekta</i>
doctor	→	<i>tagitari</i>
diploma	→	<i>tiploma</i>
ward	→	<i>wɔtit</i>
digital	→	<i>ticitɔl</i>

**/b/ → /p/**

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

<b>/b/</b>	<b>/p/</b>
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+midomo	+midomo
+mghuno	-mghuno

Sauti hizi mbili ni vipasuo vya midomo, tofauti kati yazo ni kwamba /b/ ni sauti ghuna ilhali /p/ sikhuna. Kikipsigis hata hivyo haina sauti /b/, kwa hivyo, kinapokopa msamiati ulio na sauti hii, hubadilishwa kuwa /p/ hivyo kuimarika. Kwa mfano;

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>
bɔ:k	→ <i>pukuit</i>
bill	→ <i>pilit</i>
billion	→ <i>piliɔnit</i>
bycle	→ <i>pɔskilit</i>
rubber	→ <i>rapa</i>
bus	→ <i>pasit</i>
bruʃ	→ <i>purasit</i>

#### **4.3.2 Kudhoofika kwa fonimu konsonanti**

Mgullu (1999) anaeleza kwamba kudhoofika kwa fonimu ni dhana ambayo wanaisimu hutumia kuelezea ile hali ya fonimu fulani kubadilika kutoka fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu zaidi na kuwa sauti ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali kama inavyobainika katika mifano ifuatayo;

**i) Vipasuo (-ghuna) → vipasuo (+ghuna)**

**/k/ → /g/**

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

/k/	/g/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+kaakaa laini	+kaakaa laini
-mghuno	+mghuno

Kutokana na sifa hizi, ni wazi kwamba sauti hizi zinafanana isipokuwa tu katika sifa ya mghuno ambapo sauti /k/ haina mghuno ilhali /g/ ina mghuno. Msamiati mkopo kutoka Kiingereza iliyo na sauti /k/ hubadilishwa kuwa /g/ inapoingizwa katika Kikipsigis kama ilivyo katika mfano ufuatao;

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
wi:k	→	wigit

Sauti isoghuna /k/ inapobadilishwa kuwa sauti ghuna /g/ huifanya kudhoofika kwa sababu sauti isoghuna ina nguvu matamshi kuliko sauti ghuna.

**ii) Vipasuo (-ghuna) → vipasuo ng'ong'o (+ghuna)**

**/t/ → /<sup>n</sup>d/**

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

/t/	/ <sup>n</sup> d/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo ng'ong'o
+ufizi	+ufizi
-mghuno	+mghuno

Sauti /t/ ni kipasuo cha ufizi kisicho kuwa na mghuno ilhali /<sup>n</sup>d/ ni kipasuo ng'ong'o cha ufizi kilicho na mghuno. Kwa kuwa utamkaji wa sauti isoghuna /t/ humia nguvu

zaidi kuliko utamkaji wa sauti /<sup>n</sup>d/ iliyo na mghuno basi badiliko hili ni la kudhoofika kwa fonimu. Mifano:

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
printer	→	<i>purindait</i>
kaunti	→	<i>kɔundi</i>
kɔntrækt	→	<i>kɔndrakt</i>
Kaunter	→	<i>kaɔnda</i>

/p/→/<sup>m</sup>b/

Sauti hizi zinabainishwa na sifa zifuatazo:

<b>/p/</b>		<b>/<sup>m</sup>b/</b>
+konsonanti	→	+konsonanti
+kipasuo	→	+kipasuo ng'ong'o
+midomo	→	+midomo
-mghuno	→	+mghuno

Sauti /p/ ni kipasuo kinachotamkwa kwenye midomo na haina mghuno. /<sup>m</sup>b/ ni sauti ambayo hutamkwa vilevile kwenye midomo na ina mghuno. Katika msamiati asilia wa Kikipsigis, sauti hii hupatikana katika maneno kama vile;

<b>Kikipsigis</b>	<b>tafsiri</b>
<i>imbaret</i>	shamba
<i>kambaget</i>	uzushi
<i>imbɔcɛt</i>	ƴangazi

Ilibainika kwamba baadhi ya msamiati mkopo kutoka Kiingereza ulio na konsonanti /p/ unapoingizwa katika Kikipsigis, hubadilishwa kuwa /mb/ kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
kɔmputer	→	<i>kɔmbyuta</i>
k^mpəni	→	<i>kambunit</i>

Katika mifano hii tunaona kuwa sauti /p/ isiyokuwa na mghuno imebadilishwa kuwa saui /mb/ iliyo na mghuno. Mchakato huu wa kubadilisha /p/ isiyokuwa na mghuno kuwa /mb/

iliyo ghuna hufanya sauti hii kudhoofika kwani sauti isoghuna ina nguvu matamshi kuliko sauti ghuna. Mabadiliko haya huenda yanatokea kwa sababu Kikipsigis hakina mfuatano wa silabi /mp/ lakini ina /mb/.

### 4.3.3 Udondoshaji wa sauti /h/

Ingawa Towett (1979) aliorodhesha sauti /h/ kama mojawapo wa konsonanti zilizopo katika Kikipsigis, utafiti wetu ulibainisha kuwa sauti hii haipo katika Kikipsigis. Hii inadhihirika kupitia msamiati unaokopwa ulio na sauti /h/, unapoingizwa katika Kikipsigis, hudondoshwa kwa kuwa haipo katika Kikipsigis. Kwa mfano;

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
hɔspitl	→	<i>sipitaliit</i>
helikɔpte	→	<i>elicoptait</i>
hɔlidei	→	<i>ɔliteiit</i>
hall	→	<i>ɔliit</i>

Katika mifano hii tunaona kwamba sauti /h/ imedondoshwa na kisha nafasi yake kufidiwa kwa kurefushwa kwa irabu mwishoni mwa maneno husika kabla ya kimalizio.

## 4.4 Utohozi wa Konsonanti kutoka Kiswahili

### 4.4.1 Kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti

Jinsi ilivyobainika katika mabadiliko ya konsonanti za Kiingereza, kuna kuimarika na kudhoofika vilevile katika utohozi wa konsonanti za Kiswahili. tulivyoeleza hapo awali, wanafonetiki wamethibitisha ya kuwa nguvu anazotumia mtu wakati anapotamka foni mbalimbali hutofautiana kutegemea aina ya sauti anayoitamka. Ziko fonimu ambazo huhitaji nguvu zaidi na zingine huhitaji nguvu kidogo; vitamkwa hafifu hutumia nguvu zaidi kuliko vile vitamkwa ghuna. Vilevile, Habwe na Karanja

(2004), wanaeleza kuwa kuimarika na kudhoofika kwa fonimu kunaielezeka kutegemea kiasi cha nguvu za misuli na msukumo wa mkondohewa. Kiasi cha kudhoofika au kuimarika kwa fonimu hutegemea kiasi cha mwanya kati ya alatuli na alasogezi zinazohusika katika utoaji wa sauti inayohusika, pia jinsi mwanya huu unavyopanuka ndivyo nguvu zinavyopungua na kusababisha kudhoofika kwa sauti.

#### 4.4.2 Kuimarika kwa konsonanti

Sauti huwa imeimarika kama imebadilika kutoka kwenye aina ya sauti ambayo hutumia nguvu kidogo zaidi na kuwa sauti ambayo inatumia nguvu nyingi zaidi (Mgullu, 1999). Kuimarika kwa konsonanti ya Kiswahili unapoingizwa katika Kikipsigis hutokea kupita mifano ifuatayo:

##### i. Vikwamizo (-ghuna) → vipasuo (-ghuna)

/f/ → /p/

Konsonanti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

/f/	/p/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kipasuo
+midomo meno	+midomo
-mghuno	-mghuno

/f/ ni kikwamizwa cha midomo meno, hutamkwa wakati ambapo midomo wa chini unagusa meno ya juu. Kwa kuwa konsonanti hii haipo katika Kikipsigis, basi ili msamiati mkopo ulio na sauti hii uweze kukubalika katika Kikipsigis hubadilishwa kuwa /p/ ambayo ni kipasuo cha midomo hivyo kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
ɛlfu	→	<i>eliput</i>
safari	→	<i>saparit</i>
faida	→	<i>paita</i>
bafu	→	<i>papit</i>

**ii. Vikwamizo (+ghuna) → vipasuo (-ghuna)**

**/v/ → /p/**

Konsonanti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

/v/	/p/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kipasuo
+midomo meno	+midomo
+mghuno	-mghuno

Konsonanti /v/ ni kikwamizo kinachotamkwa wakati ambapo mdomo wa chini unagusa meno ya juu. Sauti hii vilevile ina mghuno. Kwa kuwa sauti hii haipo katika Kikipsigis, hubadilishwa kuwa /p/ ambayo ni kipasuo kinachotamkwa midomoni isiyo ghuna na hivyo kuimarika kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
viazi	→	<i>Piasinik</i>
dereva	→	<i>Inderepainedet</i>

**/ɣ/ → /k/**

Sauti hizi mbili zina sifa bainifu zifuatazo;

/ɣ/	/k/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kipasuo
+kaakaa laini	+kaakaa laini
+mghuno	-mghuno



Konsonanti /ɣ/ ni kikwamizo cha kaakaa laini hubadilishwa kuwa /k/ ambayo ni kipasuo cha kaakaa laini kwa kuwa /ɣ/ haipo katika Kikipsigis hivyo kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
gharama	→	<i>karamait</i>
ghorɔfa	→	<i>kɔrɔpait</i>

### iii. Vipasuo (+ghuna) → vipasuo (-ghuna)

/d/ → /t/

Sauti hizi mbili hubainishwa na sifa bainifu zifuatazo;

/d/	/t/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+ufizi	+ufizi
+mghuno	-mghuno

Konsonanti hizi /d/ na /t/ ni vipasuo vinavyotamkwa kwenye ufizi. Hata hivyo tofauti kati yazo ni kwamba /d/ ni sauti iliyo na mghuno ilhali /t/ haina mghuno. Sauti kuwa na mghuno au kutokuwa ghuna hutokana na mkao wa glota unaobainisha namna mkondohewa kutoka mapafuni hupita kwenye nyuzi sauti. Hivi kwamba mkondohewa unapopita kwa kuzifinya nyuzi sauti na kusababisha mrindimo basi sauti itokayotolewa huwa ghuna na iwapo mkondohewa unapita bila kuzifinya nyuzi sauti basi hakutakuwepo mrindimo na sauti itokayo huwa si ghuna kama ilivyo katika utamkaji wa sauti /t/. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), sauti isiyo na mghuno ina nguvu matamshi kuliko sauti ghuna, basi sauti ghuna /d/ kubadilishwa kuwa /t/ isiyo na mghuno huifanya kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
dakika	→	<i>tagigait</i>
daraja	→	<i>taracet</i>
duka	→	<i>tugɛt</i>
dirisha	→	<i>tirisyo</i>
faida	→	<i>paita</i>

### **/b/ → /p/**

Sauti /b/ na /p/ zina sifa bainifu zifuatazo;

/b/	/p/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+midomo	+midomo
+mghuno	-mghuno

Kwa kuwa Kikipsigis hakina konsonant /b/, inapotokea katika msamiati mkopo kutoka Kiswahili, hubadilishwa kuwa /p/ kama ilivyo katika mifano ifuatayo. Hii ni kwa sababu sauti hizi zinakaribia kimatamshi.

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
bei	→	<i>peit</i>
bafu	→	<i>papit</i>
katiba	→	<i>katipa</i>
kitabu	→	<i>kitaput</i>

Kwa kuwa /b/ ni sauti ghuna ilhali /p/ sauti isoghuna, kubadilishwa kwa /b/ kuwa /p/ huifanya kuimarika.

### **/g/ → /k/**

Sauti hizi mbili zina sifa bainifu zifuatazo;

/g/	/k/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+kaakaa laini	+kaakaa laini
+mghuno	-mghuno

Sauti hizi ni vipasuo vinavyotamkwa kwenye kaakaa laini. Tofauti ni kwamba /g/ ni sauti ghuna ilhali /k/ haina mghuno. Kwa kuwa /g/ haipo katika Kikipsigis, mzungaumzaji wa Kikipsigis hubadilisha sauti hii kuwa /k/ hivyo kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
gari	→	<i>karit</i>
mgomo	→	<i>komanet</i>

#### iv. Vikwamizo (+ghuna)→ vikwamizo (-ghuna)

*/z/ → /s/*

Sifa bainifu za sauti hizi mbili ni zifuatazo;

<i>/z/</i>	<i>/s/</i>
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kikwamizo
+ufizi	+ufizi
+mghuno	-mghuno

Sauti hizi mbili /z/ na /s/ ni vikwamizwa vya ufizi. Tofauti iliyopo baina yao ni kwamba /z/ ina mghuno ilhali /s/ haina mghuno. Kwa sababu /z/ haipo katika Kikipsigis, msamiati unaokopwa kutoka Kiswahili ulio na sauti hii hubadilishwa kuwa /s/. Kwa kuwa /s/ ni ghuna ilhali /s/ haina mghuno basi badiliko hili husababisha sauti hii kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
meza	→	<i>meset</i>
kazi	→	<i>kasit</i>
mandazi	→	<i>mandasi</i>
viasi	→	<i>piasinik</i>

v. **Vipasuo kwamizwa (+ghuna) → vipasuo kwamizwa (-ghuna)**

**/j/ → /c/**

Sauti hizi mbili zina sifa bainifu zifuatazo;

/j/	/c/
+konsonanti	+konsonanti
+kizuiwa kwamizo	+kizuiwa kwamizo
+kaakaa gumu	+kaakaa gumu
+mghuno	-mghuno

Kizuiwa kwamizo cha kaakaa gumu /j/ hubadilishwa kuwa kizuiwa kwamizo cha kaakaa gumu /c/ kwa kuwa /j/ haipo katika Kikipsigis. Hata hivyo kwa sababu /j/ ni sauti ghuna na /c/ haina mghuno badiliko hili husababisha /j/ kuimarika. Kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
jɛla	→	<i>cɛla</i>
jikɔni	→	<i>ciget</i>
ajali	→	<i>acali</i>
njugu	→	<i>nchuguk</i>

vi. **Vikwamizwa (+ghuna) → vipasuo ng'ong'o (+ghuna)**

**/v/ → /mb/**

Ingawa sauti /mb/ haipo katika jedwali la AKIKI, Ashton (1994) aliorodhesha sauti zifuatazo kama vipasuo ng'ong'o /mb/, /mv/, nd/, nz/, /nj/ na /ng/ katika Kiswahili. Utafiti huu ulibainisha kuwa wakati mwingine msamiati unaokopwa ulio na konsonanti /v/ hubadilishwa kuwa /mb/ ambayo ni kipasuo ng'ong'o kinachotamkwa kwenye midomo hivyo kuongeza nguvu za matamshi na kuimarika jinsi ilivyo katika mfano ufuatao:

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
chumvi	→	<i>chumbik</i>

#### 4.4.3 Kudhoofika kwa fonimu

Mgullu (1999) analeza kuwa kudhoofika kwa fonimu ni dhana ambayo wanaisimu hutumia kuelezea ile hali ya fonimu fulani kubadilika kutoka fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu zaidi na kuwa sauti ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Kwa hivyo, hali hii husababisha upunguzaji wa nguvu za matamshi kwa kuwa fonimu inayotamkwa kwa kutumia nguvu zaidi hubadilishwa kuwa fonimu inayotumia nguvu kidogo. Utafiti huu ulibainisha kuwa hali hii hutokea katika Kikipsigis katika fonimu /k/ kama ifuatavyo;

##### i. Vipasuo (-ghuna) → vipasuo (+ghuna)

/k/ → /g/

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

/k/	/g/
+konsonanti	+konsonanti
+kipasuo	+kipasuo
+kaakaa laini	+kaakaa laini
-mghuno	+mghuno

Sauti /k/ ambayo ni kipasuo cha kaakaa laini kisicho na mghuno hubadilishwa kuwa /g/ ambayo ni kipasuo cha kaakaa laini kilicho na mghuno na hivyo kudhoofika kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
askari	→ <i>asigərindet</i>
mkate	→ <i>magatiat</i>
hekalu	→ <i>egalut</i>
kikombe	→ <i>kigombet</i>
malaika	→ <i>malaigajat</i>
mkora	→ <i>magorajat</i>

Mabadiliko haya hutokea hata ingawa sauti /k/ ipo katika Kikipsigis, hii ni kwa sababu /k/ katika Kikipsigis hutumika mwanzoni na mwishoni mwa msamiati ilhali /g/ hutumika katikati ya maneno kama ilivyo katika msamiati asilia wa Kikipsigis ifuatayo;

<b>Kikipsigis</b>		<b>Tafsiri</b>
<i>kalyet</i>	→	amani
<i>kɔnda</i>	→	jico
<i>kelyek</i>	→	miguu
<i>kɔgeny</i>	→	tena

Tulibainisha pia kwamba konsonanti /k/ hukubalika katikati ya msamiati wa Kikipsigis wakati ambapo imetanguliwa na irabu na kufuatwa na fonimu /s/ au /t/ kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Kikipsigis</b>		<b>Tafsiri</b>
<i>melɛktɔ</i>	→	mfahara
<i>rɛktɔ</i>	→	huteremka
<i>walaksei</i>	→	hubadilika

Hata hivyo katika msamiati mkopo, /k/ hutokea katikati mwa maneno iwapo imetanguliwa na konsonanti /s/ au r/ kama ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
<i>baiskeli</i>	→	pɔskilit
<i>serikali</i>	→	sɛrkalit
<i>kɔrkɔrɔni</i>	→	kɔrkɔrɛt

Tulibainisha katika utafiti huu pia kuwa kuna mabadiliko ya konsonanti yasiyohusisha kuimarika wala kudhoofika kwa fonimu. Mabadiliko haya ni kama yafuatayo:

**ii. Vikwamizo (-ghuna) → vikwamizo (-ghuna)**

/θ/ → /s/

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

/θ/	/s/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kikwamizo
+meno	+ufizi
-mghuno	-mghuno

Konsonanti /θ/ ni kikwamizo kinachotamkwa kwenye meno ilhali /s/ ni kikwamizo cha ufizi. Kwa sababu Kikipsigis hakina sauti /θ/ maneno yanayosharabiwa yaliyo na sauti hii hubadilishwa kuwa /s/ kwa kuwa sauti hii inakaribiana kimatamshi na /s/ na vilevile ni kikwamizo. Sauti hizi mbili hazina mghuno kwa hivyo zinatamia nguvu sawa katika matamshi na hivyo basi kutoimarika wala kutodhoofika, mifano:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
θumuni	→ <i>sumɔnit</i>
θɛlaθini	→ <i>salasini</i>

/ʃ/ → /s/

Sauti hizi zina sifa zifuatazo;

/ʃ/	/s/
+konsonanti	+konsonanti
+kikwamizo	+kikwamizo
+meno na ufizi	+ufizi
-mghuno	-mghuno

Kikwamizo cha kaaka gumu /ʃ/ hubadilishwa kuwa kikwamizo cha ufizi /s/. Hii ni kwa sababu katika Kikipsigis hakuna sauti /ʃ/ kwa hivyo, msemaji wa lugha hii huibadilisha kuwa sauti inayokaribiana kimatamshi ambayo ni /s/ kwani sauti hizi mbili ni vikwamizo na zote pia hazina mghuno. Kwa kuwa sauti hizi mbili hazina mghuno na ziko katika kategoria, vikwamizwa hafifu, moja jinsi ilivyobainishwa na Mgullu, basi mabadiliko haya hayahusishi kuimarika au kudhoofika. Kwa kufanya

hivi Kikipsigis huziba pengo la ukosefu wa sauti /ʃ/ kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
ufuru	→	<i>aisurut</i>
mʃipi	→	<i>mɔsipit</i>
ʃetani	→	<i>setani</i>
ʃilingi	→	<i>silingit</i>

Tulibainisha kuwa sauti /ʃ/ hubadilishwa kuwa /s/ hasa inapotangulia irabu /u/, /e/ na /i/ kama ilivyo katika *shetani*, *shilingi* na *ushuru*.

Tulibainisha vile vile kwamba uyeyushaji hutokea katika baadhi ya msamiati iliyo na konsonanti /ʃ/. Hii ni kwa kuwa baadhi ya msamiati iliyo na konsonanti /ʃ/ hubadilishwa kuwa /sy/ kama ilivyo katika mifano ifuatayo. Mabadiliko haya hutokea kwa sababu Kikipsigis hakina konsonanti /ʃ/.

<b>Kiswahili</b>			<b>Kikipsigis</b>
mshahara	→	<i>musi+ara</i>	→ <i>musjara</i>
dirisha	→	<i>tirisi+a</i>	→ <i>tirisjet</i>
ʃati	→	<i>si+atit</i>	→ <i>sjatit</i>

Hali hii hutokea hasa wakati ambapo /ʃ/ imetangulia irabu /a/ kama inavyobainika katika mifano tuliyotoa kwa mfano katika neno ‘*mshahara*, *shati*’.

#### **4.4.4 Uchopezi wa konsonanti**

Katika Kiswahili, asilimia kubwa ya msamiati huwa na silabi wazi, hata hivyo hali ni tofauti katika Kikipsigis kwani hupendelea muundo wa silabi funge. Kwa hivyo, Kikipsigis kinapokopa msamiati kutoka Kiswahili, msamiati huo hutoholewa kwa kuchopekwa konsonanti mwishoni mwa neno ili kuunda silabi funge kama inavyobainika katika mifano ifuatayo;



<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>		
simu	→	<i>simɔit</i>		
chupa	→	<i>cupɔit</i>		
ngano	→	<i>nganuk</i>		
maharagwe	→	<i>marakwe:k</i>		
ʃeherekea	→	<i>sjeregean</i>		
meza	→	<i>mesait</i>	→	<i>meset</i>
mpira	→	<i>imbirait</i>	→	<i>imbiret</i>
kanisa	→	<i>kanisait</i>	→	<i>kaniset</i>

Mifano hii imedhihirisha kwamba Kikipsigis hutohoa msamiati wa Kiswahili ulio na silabi wazi kwa kuongeza konsonanti mwishoni mwa neno husika ili msamiati huo ukubalike katika Kikipsigis. Konsonanti inayochopekwa sana ni /t/ na wakati mwingine /k/ na /n/.

#### **4.4.5 Udondoshaji wa konsonanti**

Utafiti huu ulibainisha kuwa upo ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa Kikipsigis hudondosha konsonanti kutoka baadhi ya msamiati mkopo kutoka Kiswahili. Konsonanti zinazodondoshwa ni zile ambazo hazipatikani katika lugha hii, kwa hivyo, zinapopatikana katika msamiati unaokopwa hudondoshwa na nafasi zao kuachwa wazi au kuchukuliwa na konsonanti nyingine inayokaribiana kimatamshi na konsonanti inayodondoshwa.

#### **Udondoshaji wa konsonanti /h/**

Ingawa Toweett (1979) aliorodhesha fonimu /h/ kama mojawapo wa konsonanti za Kikipsigis, data ya utafiti huu umebainisha kwamba fonimu hii haipo katika lugha hii. Hii ni kwa sababu konsonanti hii /h/ hudondoshwa katika msamiati wa Kiswahili unaosharabiwa katika Kikipsigis kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

### Udondoshaji wa /h/ mwanzoni mwa msamiati

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
hesabu	→	<i>esapuuk</i>
hekalu	→	<i>egaluut</i>
harusi	→	<i>arusiit</i>
hoteli	→	<i>oteliit</i>
hema	→	<i>emait</i>

Mifano hii inaonyesha kwamba, /h/ inapotokea mwanazoni mwa neno hudondolewa na nafasi yake kuachwa wazi kwa sababu sauti hii haipo katika Kikipsigis.

Hata hivyo tunaona kwamba katika maneno mengine, udondoshaji wa /h/ mwanzoni mwa msamiati hufidiwa kwa kurefushwa kwa irabu inayotokea mwishoni mwa neno hilo kama ilivyo katika [hekalu → ekaluut], [hoteli → oteliit].

### Udondoshaji wa /h/ katikati ya msamiati

Katika udondoshaji wa /h/ katikati mwa neno tulibainisha kwamba sauti hii hudondoshwa na nafasi yake ama kuachwa wazi au kuundwa kwa kiyeyusho [j] au pia /h/ kudondoshwa pamoja na irabu inayofuata mathalani;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
sahani	→	<i>saniit</i>
maharagwe	→	<i>marakweek</i>
bahari	→	<i>pariit</i>
bahafa	→	<i>pasjait</i>
mƣahara	→	<i>musjara</i>
mhogɔ	→	<i>mɔgɔ</i>
ruhusa	→	<i>rusa</i>
ƣeherekea	→	<i>syeregean</i>
mƣahara	→	<i>musyara</i>

Udondoshaji wa /h/ na nafasi yake kuachwa wazi hubainika katika;

mhogo → *mogo*

Udondoshaji wa /h/ na nafasi yake kuchukuliwa na kiyeyusho [j];

bahafa → *pasjait*

mjahara → *musyara*

sheherekea → *sjeregean*

Udondoshaji wa /h/ pamoja na irabu katikati ya neno;

Sahani → *saniit*

bahari → *pariit*

ruhusa → *rusa*

maharagwe → *marakwεek*

Katika mifano hii, /h/ inapodondoshwa, irabu mbili zitafuatana na hivyo kuibua muundo usioleta maana katika Kikipsigis kwa mfano;

Sahani → *saniit*

bahari → *pariit*

Kwa hivyo, Kikipsigis haina budi kuondoa irabu moja kati ya hizo mbili ili kunda msamiati unaokubalika na ulio na maana katika Kikipsigis mathalani;

**Sahani** → **saani** → **saniit**

**bahari** → **paari** → **pariit**

Mifano hii hivyo basi imedhihirisha kwa uwazi kuwa sauti /h/ haipo katika Kikipsigis na hii ndio sababu sauti hii hudondolewa katika msamiati mkopo wa Kiswahili unapoingizwa katika lugha hii.

#### 4.5 Ongezeko la Silabi katika Msamiati Mkopo

Kutokana na tofauti ya miundo ya silabi katika lugha zote tatu za utafiti huu, yaani lugha changizi (Kiswahili na Kiingereza) na lugha pokezi (Kikipsigis), ni sharti msamiati ulio na muundo usiokubalika katika Kikipsigis ufanyiwe mabadiliko ili kuuruhusu msamiati huo kukubalika katika Kikipsigis.

##### 4.5.1 Usilabishaji kupitia uchopezi wa irabu

Kwa mujibu wa nadharia ya fonolojia zalishi ya KI ni kwamba kunazo kanuni zinazoongoza mchakato wa usilabishaji katika lugha kwa kudai kuwa kila lugha ina kanuni zake maalum za usilabishaji. Kanuni hizi huweza kubadilisha viambajengo vya konsonanti na vya irabu katika neno husika. Tulibainisha kwamba Kikipsigis hakiruhusu mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa maneno jinsi ilivyo katika lugha changizi. Akiunga mkono dhana hii, Lehiste (1992) anaeleza kwamba usilabishaji husababishwa na haja ya lugha pokezi kuondoa miundo ya kifonolojia isiyokubalika katika msamiati mkopo kutoka lugha changizi. Kwa hivyo Kikipsigis hutohoa msamiati wa aina hii kupitia uchopezi wa irabu jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
Gru:p	→	kurupit
sku:l	→	sugul
grade	→	kiretit
bruf	→	purasit
printer	→	purindait

Inadhihirika katika mifano hii kwamba Kikipsigis hairuhusu mfululizo wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Kwa hivyo ili msamiati mkopo ulio na mfululizo wa aina hiyo uweze kukubalika katika lugha hii basi huchopekwa irabu kati ya konsonanti husika.


Irabu inayochopekwa huweza kuwa /a/, /e/, /i/, /o/ au /u/ kwa kutegemea namna inavyotamkwa.

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
mcele	→	<i>mucelek</i>
mkoba	→	<i>makupet</i>
mkate	→	<i>magatiat</i>
mkora	→	<i>magorajat</i>
mjarahara	→	<i>musjara</i>
stima	→	<i>sitimet</i>


Kiswahili vilevile huruhusu konsonanti kufuatana mwanzoni mwa neno jinsi ilivyo katika **mchele**, **mkoba**, **mkate** na kadhalika. Kwa vile mfululizo huu hauruhusiwi katika Kikipsigis mwanzoni mwa maneno basi Kikipsigis huchopeka irabu kati ya konsonanti husika ili kuufanya muundo wa mwanzo wa silabi uwe wazi.

Kwa mfano katika neno mchele, irabu /u/ huchopekwa kati ya konsonanti /m/ na /c/ ili kupata neno [**mu**chelek] na hivyo kukubalika katika muundo wa silabi katika Kikipsigis. Kwa hivyo katika neno mchele muundo wa silabi wa **KKIKI** unabadilishwa kuwa **KIKIKIK** katika Kikipsigis. Mifano hii huweza kuwakilishwa katika michoro ifuatavyo:

Mkate → magatiat



Grup → kurupit



#### 4.5.2 Usilabishaji kupitia uchopezi wa konsonanti

Tulibainisha kwamba Kikipsigis hupendelea silabi funge kwa hivyo msamiati mkopo kutoka Kiingereza na Kiswahili ulio na silabi wazi hubadilishwa kuwa silabi funge kupitia uchopezi wa konsonanti /t/ katika umoja na /k/ katika wingi ili kuufanya ukubalike katika muundo wa kimofonemiki wa Kikipsigis jinsi inavyobainika katika mifano ifuatayo:

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>
pəli:s (police)	→	pəlisiɔt
keɪs (case)	→	kesit
baɪclɛ	→	pəskilit
<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
chuma	→	cumɔjɔt
mkɔra	→	magɔraɔjat
mwalimu	→	molimujɔt
malaika	→	malaigayɔt
kitanda	→	kitandɛt
kitabu	→	kitaput
bafu	→	papit
kanisa	→	kaniset
daraja	→	taracet
mkate	→	magatiat

Hata hivyo data ya utafiti huu ulibainisha kwamba hata katika maneno mengine yanayokopwa yaliyo na silabi funge, Kikipigis huchopeka silabi kwa mfano:

<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kikipsigis</b>
taʊn (town)	→	<i>taʊnit</i>
ɒfɪsə (officer)	→	<i>ɒpɪsayat</i>
gru:p (group)	→	<i>kurupit</i>
wɔ:d (ward)	→	<i>wɔtit</i>
lɔrɪ (lorry)	→	<i>lɔrit</i>
θɜ:mɒs (thermos)	→	<i>tamɔsit</i>
kɒndʌktɔ (conductor)	→	<i>kɒndaktayat</i>

Katika mifano hii kuna uwezekano wa msamiati kama vile [taʊn] kukopwa kama [taʊn] ambayo ni silabi funge lakini tunaona kwamba unatoholewa kuwa [taʊnit]. Hali hii ilituwezesha kubainisha kwamba Kikipsigis hutumia konsonanti /t/ katika umoja hivyo basi ili kuufanya msamiati [taʊn] ukubalike katika mfumo wa Kikipsigis hutoholewa kuwa [taʊnit] ambapo mbali na konsonanti ya umoja /t/ kuchopekwa, silabi /it/ huchopekwa.

Tulibainisha kanuni zifuatazo za usilabishaji:

- a) Ø o#.....
- b) Ø a#.....
- c) Ø i#.....
- d) Ø u#.....
- e) Ø t/.....
- f) Ø it/.....
- g) Ø yat/.....
- h) Ø yot/.....

Kanuni hizi za usilabishaji huruhusu irabu na konsonanti kuchopekwa katika msamiati mkopo ili kufuata muundo wa silabi katika Kikipsigis. Kwa sababu mabadaliko ya aina hii huhusisha kubadilika kwa silabi katika msamiati mkopo unapongizwa katika lugha pokezi basi hurejelewa kama mabadiliko ya

kimofonemiki. Lengo la mabadiliko haya ni kuufanya msamiati mkopo kufuata muundo wa silabi katika lugha pakezi ili kuufanya msamiati mkopo kukubalika katika lugha husika.

#### **4.6 Kategoria za Kisarufi za Msamiati Mkopo**

Katika uchanganuzi wetu wa data tulibainisha kwamba pana haja ya kutambua viambishi vya umoja na vya wingi katika msamiati mkopo wa Kikipsigis. Ingawa sehemu hii haikuwa katika madhumuni yetu ya utafiti. Dorney (2007) anaeleza kuwa uchanganuzi wa kisifa huruhusu mabadiliko yanayoweza kutokea katika kiwango cha uchanganuzi wa data au ukusanyaji wa data bora mabadiliko hayo yana umuhimu katika utafiti husika. Kwa hivyo tulibainisha viambishi vya umoja na wingi katika msamiati mkopo wa Kikipsigis. Hii ni kwa sababu viambishi hivi huathiri muundo wa maneno. Kwa mfano, neno '*picha*' hutoholewa kuwa '*pichait*' katika umoja na '*pichainik*' katika wingi ihali neno '*chuma*' linatoholewa kuwa '*chumoyot*' katika umoja na '*chumoinik*' katika wingi. Maneno haya mawili yanaishia kwa irabu 'a' ilhali yanatoholewa kwa njia tofauti. Kwa hivyo tulioa kwamba kuna umuhimu wa kubainisha namna msamiati unavyoteuliwa kuchukua mofu fulani katika umoja na nyingine katika wingi.

Kwa mujibu wa Verma na Krisinaswamy (1994) mofolojia hurejelea uchunguzi wa maneno na ubainishaji wa muundo wa maneno husika kwa kuzingatia mofimu. Kwa hivyo, katika kushughulikia mofolojia ya msamiati mkopo katika Kikipsigis, tulichunguza muundo wa maneno hayo katika umoja na wingi kama ilivyobainika ifuatavyo;



### 1. Kikundi 1 (-it → -inik au -isiek)

Ilibainika kwamba misamiati mkopo katika kikundi hiki, huchukua mofu [-it] katika umoja na ama [-inik] au [-isiek] katika wingi. Kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis umoja</b>		<b>wingi</b>
Picha	→	<i>pichait</i>	→	<i>pichainik</i>
chama	→	<i>chamait</i>	→	<i>chamaisiek</i>
safari	→	<i>saparit</i>	→	<i>saparisiek</i>
chupa	→	<i>chupait</i>	→	<i>chupainik</i>
kazi	→	<i>kasit</i>	→	<i>kasisiek</i>
kilo	→	<i>kiloit</i>	→	<i>kiloisiek</i>
gari	→	<i>karit</i>	→	<i>karisiek</i>
sahani	→	<i>saniit</i>	→	<i>sanisiek</i>
tarehe	→	<i>tarigiit</i>	→	<i>tarigisiek</i>

Kutokana na data hii tunaona kwamba kuna uchopezi wa silabi ‘it’ mwishoni mwa neno linakopwa katika hali ya umoja. Ni katika maneno yaliyo na konsonanti /h/ ambapo konsonanti hudondoshwa na kisha kufidiwa kwa kupitia matumizi ya irabu mbili. Hii ni kwa sababu Kikipsigis hakina konsonanti /h/. Hata hivyo katika msamiati ‘tarehe’ kumetokea uchopezi wa konsonanti /g/ baada ya kudondoshwa kwa konsonanti /h/. Katika hali ya wingi, konsonanti /t/ katika mofu ‘it’ ya umoja hudondoshwa na kisha mofu –inik au –isiek kutumika kama alomofu za wingi.

Katika Kiiingereza vilevile kunayo maneno yanayoingia katika kikundi hiki:

<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis umoja</b>		<b>wingi</b>
town		<i>taonit</i>		<i>taonisiek</i>
book		<i>puguit</i>		<i>puguisiek</i>
school		<i>sugulit</i>		<i>sugulisiek</i>
glass		<i>kilasit</i>		<i>kilasisiek</i>
thermos		<i>tamosit</i>		<i>tamosisiek</i>

group	<i>kurupit</i>	<i>kurupisiek</i>
word	<i>wotit</i>	<i>wotisiek</i>

Katika mifano hii jinsi ilivyokuwa katika msamiati mkopo kutoka Kiswahili, kuna uchopezi wa silabi 'it' mwishoni mwa neno linalokopwa katika hali ya umoja. Katika hali ya wingi, konsonanti /t/ katika mofu 'it' ya umoja hudondoshwa na kisha mofu – isiek kutumika.

Kama tulivyoeleza hapo awali, msamiati mkopo ulio na irabu /a/ mwishoni, hutoholewa kuwa na silabi /ait/. Hata hivyo, katika misamiati ifuatayo hali ni tofauti; kwa mfano msamiati 'kanisa' unapokopwa hubadilishwa kuwa 'kaniset' ilhali tungetaraji 'kanisait'. Hali hii hivyo basi hutokana na mvutano wa irabu unaozalisha sauti moja tofauti ambayo ni irabu /ε/ kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>	
daraja	→	<i>taracha+it</i>	→ <i>tarachet</i>
barua	→	<i>barua + it</i>	→ <i>baruet</i>
kanisa	→	<i>kanisa + it</i>	→ <i>kaniset</i>
kitanda	→	<i>kitanda + it</i>	→ <i>kitandet</i>

Msamiati wa aina hii huchukua mofu [-ok] katika wingi jinsi inavyobainika kaika mifano ifuatayo;

		<b>Umoja</b>	<b>wingi</b>
kitanda	→	<i>kitandet</i>	→ <i>kitandok</i>
barua	→	<i>baruet</i>	→ <i>baronok</i>
daraja	→	<i>tarachet</i>	→ <i>tarachok</i>
kikombe	→	<i>kigombet</i>	→ <i>kigombok</i>
ghorofa	→	<i>koropet</i>	→ <i>koropok</i>
korokoroni	→	<i>korgoret</i>	→ <i>korgorok</i>
dirisha	→	<i>tirisyet</i>	→ <i>tirisyok</i>

Mifano ghairi,

Duka	→	<i>tuget</i>	→	<i>tugosiek</i>
Nguo	→	<i>ingoriet</i>	→	<i>ingoroik</i>

## 2. Kikundi 2 (-oit/ -yot → -inik)

Katika kikundi hiki, misamiati huchukua mofu [-oit] ama [yot] katika umoja na [-inik] katika wingi kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis umoja</b>		<b>wingi</b>
chuma	→	<i>chumoyot</i>	→	<i>chumoinik</i>
fundi	→	<i>pundiyot</i>	→	<i>pundinik</i>
ndizi	→	<i>indisiot</i>	→	<i>indisinik</i>

Katika mifano hii tulibainisha kwamba msamiati mkopo unaochukua mofu [-yot] au [-oit] katika umoja, hubadilishwa kuwa mofu [-inik] katika wingi. Hapa, kiyeyusho /j/ hutokana na mchakato wa uyeyushaji kwa sababu ya kufuatana kwa irabu tatu mathalani fundi → tunapata pundi-**iot**, chuma → chumo-**iot**, kwa hivyo ili kuepuka kufuatana kwa irabu tatu, basi kunatokea uyeyushaji pundi-**yot**, chumo-**yot**.

Katika msamiati mkopo wa Kiingereza hatukupata msamiati unaoingia katika kikundi hiki. Hata hivyo tulibainisha maneno yanaoishia kwa mofu [-yon] katika umoja na kisha kuchukua mofu [-isiek] katika wingi kwa mfano:

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis umoja</b>	<b>wingi</b>
location	<i>lokesyon</i>	<i>lokesyonisiek</i>
station	<i>stesyon</i>	<i>stesyonisiek</i>
television	<i>telepisyon</i>	<i>telepisyonisiek</i>

Katika mifano hii, tunaona kwamba msamiati mkopo katika umoja umechukua mofu [-yon] na kisha kuongeza mofu [-isiek] katika wingi. Mofu hii ya umoja kwa mtazamo wetu imetokana na ukopaji wa kimatamshi.

### 3. Kikundi 3 (-at/ -yat → -inik au -aek)

Katika kikundi hiki misamiati huchukua mofu [-at] au [-yat] katika umoja na [-nik] au [-aek] katika wingi, kwa mfano:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis (umoja)</b>	<b>wingi</b>
mkate	<i>magatiat</i>	<i>magatinik</i>
viasi	<i>pyasiat</i>	<i>piasinik</i>
risasi	<i>risasiat</i>	<i>risasinik</i>
mandazi	<i>mandasiat</i>	<i>mandasinik</i>
	<b>yat</b>	<b>ek</b>
<i>malaika</i>	<i>malaigayat</i>	<i>malaigaek</i>
<i>mkora</i>	<i>magorayat</i>	<i>magoraek</i>
<i>dereva</i>	<i>inderepayat</i>	<i>inderepaek</i>

Mifano ghairi:

chungwa	<i>machungwat</i>	<i>machungwek</i>
nyanya	<i>nyanyat</i>	<i>nyanyek</i>

Mifano hii inabainisha kwamba katika kikundi hiki cha msamiati unaohusu binadamu huishia kwa mofu [yat] katika umoja na kisha mofu [-aek] katika wingi. Kwa mfano msamiati malaika, dereva na kivumishi cha sifa mkora jinsi inavyobainika hapo juu.

Katika Kiingereza msamiati mkopo huingia katika kategoria hii kwa mfano:

<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis (umoja)</b>	<b>wingi</b>
minister	<i>ministayat</i>	<i>ministaek</i>
director	<i>tairktayat</i>	<i>tairktaek</i>
mechanic	<i>maganikayat</i>	<i>maganikaek</i>
member	<i>membayat</i>	<i>membraek</i>
counselor	<i>kansolayat</i>	<i>kansolaek</i>

Mifano hii inabainisha kwamba Kikipsigis katika kikundi hiki huchukua mofu [-yat] katika umoja na kisha mofu [-aek] katika hali ya wingi.

#### 4. Kikundi 4

Kikundi hiki kinajumuisha msamiati mkopo unaoishia kwa irabu ambapo tulibainisha kwamba haubadiliki katika wingi, kwa mfano:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis (umoja)</b>	<b>wingi</b>
katiba	<i>katipa</i>	<i>katipa</i>
mhogo	<i>mogo</i>	<i>mogo</i>
mshahara	<i>musyara</i>	<i>musyara</i>
<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis (umoja)</b>	<b>wingi</b>
cement	<i>semendi</i>	<i>semendi</i>
choir	<i>kwaya</i>	<i>kwaya</i>
sabath	<i>sapato</i>	<i>sapato</i>
forest	<i>poroste</i>	<i>poroste</i>
test	<i>testi</i>	<i>testi</i>
scheme	<i>sigiim</i>	<i>sigiim</i>

Katika mifano iliyotolewa hapo juu, tunaona kuwa takriban misamiati yote huishia kwa konsonanti /t/ katika umoja na konsonanti /k/ katika wingi. Uchunguzi wetu ulibainisha kwamba hali hii haidhihiriki tu katika msamiati mkopo, ila pia katika msamiati asilia wa Kikipsigis kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

<b>Umoja</b>	<b>wingi</b>	<b>tafsiri</b>
<i>ketit</i>	<i>ketiik</i>	mti
<i>metit</i>	<i>metoek</i>	kichwa
<i>keldet</i>	<i>keleek</i>	jino
<i>pandyat</i>	<i>pandek</i>	mahindi
<i>muryat</i>	<i>murek</i>	panya
<i>logoiyat</i>	<i>logoek</i>	machungwa
<i>suswot</i>	<i>suswek</i>	nyasi
<i>kot</i>	<i>korik</i>	nyumba

Kimsingi, uchanganuzi wa mabadiliko ya kimofofonemiki katika msamiati mkopo wa Kikipsigis kutoka Kiingereza na Kiswahili umebainisha kuwa irabu katika msamiati wa Kiingereza hutoholewa kupitia ufupishaji wa irabu ndefu, usahilishaji wa irabu unganifu, uyeyushaji na muungano wa irabu. Katika irabu za Kiswahili, utohozi hufanyika kupitia uchopezi wa irabu, tangamano la irabu/kuafikiana kwa irabu, mvutano wa irabu na udondoshaji wa irabu. Kwa upande mwingine, michakato inayotumika katika utohozi wa konsonanti za Kiingereza na Kiswahili zinafanana. Michakato hiyo ni pamoja na kuimarika kwa konsonanti, kudhoofika kwa konsonanti, uchopezi wa konsonanti na vilevile udondoshaji wa konsonanti. Usilabishaji hufanyika kupitia uchopezi wa irabu mwanzoni mwa msamiati ulio na mfuatano wa konsonanti mbili. Usilabishaji pia hufanyika kupitia uchopezi wa konsonanti mwishoni mwa msamiati ulio na muundo wa silabi wazi. Hii kwa sababu Kikipsigis hupendelea muundo wa silabi funge.

## SURA YA TANO

### SABABU ZA KIISIMUJAMII ZINAZOCHANGIA UINGIZWAJI WA

#### MSAMIATI MKOPO KATIKA KIKIPSIGIS

##### **5.0 Utangulizi**

Katika sura hii, tulichunguza sababu mbalimbali za kiisimujamii zinazochangia ukopaji wa msamiati katika lugha ya Kikipsigis. Myers-Scotton (2002) anaeleza kuwa mitagusano baina ya lugha husababisha athari mbalimbali katika lugha hizo. Matokeo ya mtagusano wa lugha ni pamoja na ukopaji wa msamiati, ujozi lugha na uundaji wa Pijini na Krioli. Mbali na kwamba ukopaji hutokea moja kwa moja katika mtagusano, ujozi lugha pia huchangia ukopaji wa elementi za kileksia baina ya lugha husika.

Myers-Scotton (kama hapo juu) anafafanua kwamba sifa iliyo wazi ya kiisimujamii kuhusu ukopaji wa msamiati ni kuwa katika lugha nyingi ulimwenguni, ukopaji huelekea katika upande mmoja ambapo wasemaji wa lugha iliyo na hadhi ya chini huchukua msamiati/maneno kutoka lugha iliyo na hadhi ya juu. Nchini Kenya, kwa mfano, lugha za Kiswahili na Kiingereza zinachukuliwa kuwa lugha zilizo na hadhi ya juu kwa sababu Kiingereza ni lugha rasmi na hutumika katika mawasiliano ya kimataifa, Kiswahili kwa upande wake kimepewa hadhi katika jamii kwa kuwa ni lugha ya taifa na vilevile ni lugha rasmi.

Katika kiunzi chake cha ukopaji wa kileksia, Myers-Scotton anabainisha aina mbili za ukopaji: ukopaji wa msamiati wa kiutamaduni na ukopaji wa msamiati wa kimtindo. Katika ukopaji wa kiutamaduni, msamiati unaokopwa ni ule unaorejelea dhana geni ambayo haijakuwepo katika utamaduni wa lugha inayokopa. Kwa upande mwingine, ukopaji wa kimtindo hurejelea ukopaji wa msamiati wa kigeni wakati ambapo kuna kisawe au msamiati asilia unaorejelea dhana hiyo hiyo. Ukopaji wa aina hii kwa

mujibu wa Myers-Scotton husababishwa na ubadilishaji msimbo. Vilevile, lugha huweza kukopa msamiati hata wakati ambapo ina msamiati wake asilia kwa sababu maneno mkopo huwa mafupi. Anatoa mfano kutoka lugha ya Shona ambapo msamiati wa Kiingereza unaorejelea takwimu hupendelewa kwa kuwa ni mfupi hata ingawa lugha hiyo ina msamiati wake asilia wa kurejelea takwimu.

Deroy (1956) anaeleza kuwa msamiati unaokopwa huwa katika mfumo tofauti wa kiisimu wa lugha changizi, na kuingizwa kwake katika lugha pokezi husababishwa na sababu za kijamii. Anazidi kufafanua kuwa ukopaji wa kileksia kwa ujumla husababishwa na haja ya kujaza pengo la msamiati usiokuwepo katika utamaduni wa lugha husika au haja ya lugha pokezi kujinasibisha na lugha iliyo na hadhi ya juu. Hali hii ya kutaka kujinasibisha na lugha iliyo na hadhi ya juu hutokea pale ambapo lugha inakopa msamiati ilhali inayo msamiati wa kiasili wa kurejelea dhana husika. Utafiti huu unakubaliana na mawazo haya ya Deroy kwamba lugha hukopa msamiati ili kujaza pengo la ukosefu wa msamiati hasa kwa dhana ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa lugha hiyo husika.

Katika utafiti huu, mawazo ya Myers-Scotton (kama hapo juu) yalituongoza katika kubainisha sababu za kiisimujamii zilizochangia ukopaji wa msamiati wa Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis. Ukopaji unaodhihirika katika Kikipsigis ni wa aina mbili:- Ukopaji wa msamiati wa kiutamaduni na ukopaji wa msamiati wa kimtindo. Ilibainika kwamba msamiati geni huweza kukopwa kwa njia ya moja kwa moja (kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kikipsigis) au kwa njia ya ukopaji wa kidaraja (kutoka Kiingereza ukapitia Kiswahili kabla ya kuingizwa katika Kikipsigis).



Ili kubainisha sababu zinasosababisha ukopaji wa msamiati katika Kikipsigis, tuliangazia msamiati mkopo katika nyanja mbalimbali za maisha katika jamii ya wakipsigis. Nyanja hizo ni:

- a) Uwanja wa sayansi / teknolojia
- b) Uwanja wa elimu
- c) Uwanja wa dini
- d) Uwanja wa vifaa vya kinyumbani
- e) Uwanja wa siasa
- f) Uwanja wa kilimo
- g) Uwanja wa vyakula
- h) Uwanja wa uchumi na biashara
- i) Uwanja wa usafiri na miundo msingi
- j) Uwanja wa michezo
- k) Uwanja wa ajira
- l) Uwanja wa mavazi
- m) Uwanja wa tiba na masuala ya afya

Uchanganuzi uliendelezwa kwa misingi ifuatayo:- ukopaji wa msamiati wa kiutamaduni, ukopaji wa kimtindo, ukopaji wa msamiati mahususi, ukopaji wa msamiati ili kuondoa utata wa kimaana, ukopaji wa kurahisisha mawasiliano na ukopaji wa msamiati kutoka lugha ya Kiingereza kupitia Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia msamiati unaokopwa moja kwa moja kabla ya kushughulikia ukopaji wa kidaraja.

## 5.1 Ukopaji wa Kiutamaduni

Myers-Scotton (kama hapo juu) anaeleza kwamba lugha hukopa msamiati ili kukidhi haja ya kurejelea dhana geni isiyokuwepo katika utamaduni wa lugha husika. Hali hii imedhihirika katika Kikipsigis ambapo lugha hii imekopa msamiati kutoka Kiswahili na Kiingereza ili kurejelea dhana geni katika nyanja mbalimbali jinsi inavyodhihirika ifuatavyo:

### 5.1.1 Uwanja wa sayansi na teknolojia

Katika utamaduni wa Wakipsigis, vifaa vya kisayansi na teknolojia havikuwepo. Vifaa hivi viligunduliwa na wanasayansi. Kwa hivyo, Kikipsigis kimekopa na kutohoa msamiati wa kisayansi kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili kutumika kuzirejelea dhana geni za kisayansi:

<b>1. (a)</b>	<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>	
	simu	→	<i>simoit</i>	
	stima	→	<i>sitimet</i>	
	chuma	→	<i>chumoiyot</i>	
	risasi	→	<i>risasyat</i>	
	bunduki	→	<i>pundugit</i>	
<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>		<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	factory	→	<i>paktori</i>	kiwanda
	machine	→	<i>mosyinit</i>	mashine
	bomb	→	<i>pomit</i>	bomu
	type	→	<i>taipen</i>	piga taipu
	digital	→	<i>tichitol</i>	dijitali

Kwa kuwa misamiati hii haikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis, lugha hii imelazimika kukopa msamiati kutoka lugha hizi bebwa ili kurejelea dhana hizo geni.

Kembo-sure (1993) katika utafiti wake wa msamiati mkopo wa Kiingereza katika Dholuo anaeleza kuwa asilimia kubwa ya msamiati mkopo wa Kiingereza katika Dholuo ilitoka katika nyanja za elimu, sayansi na teknolojia kwa kuwa nyanja hizi

zilikuwa geni katika utamaduni wa Wajaluo. Utafiti huu unakubaliana na dhana hii kwa kuwa Kikipsigis vilevile kimekopa msamiati kutoka nyanja za elimu, sayansi na teknolojia, kazi, uchumi na biashara ambazo zilikuwa geni katika Kikipsigis.

### 5.1.2 Uwanja wa afya na matibabu

Kabla ya majilio ya wamishenari na wakoloni, magonjwa katika jamii ya Wakipsigis yalitibiwa na wazazi kwa kutumia dawa za kienyeji. Wazazi waliposhindwa kutibu walimtegemea tabibu wa kienyeji (*chepkerichot*) aliyeaminika kuwa na uwezo wa kutibu kwa kutumia dawa za kienyeji. Kulikuwepo pia na mganga aliyekuwa na uwezo wa kimiujiza wa kutibu magonjwa mbalimbali aliyetitwa *chepsogeyot*.

Kwa hivyo wakoloni walipofika nchini na kuleta matibabu ya kisasa, Wakipsigis walilazimika kukopa msamiati ili kurejelea dhana geni za utabibu ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa Kikipsigis:

<b>2. (a)</b>	<b>Kiswahili</b> sindano uzi	<b>Kikipsigis</b> <i>sindanut</i> <i>usit</i>	
<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b> mortuary ward net laboratory admit	<b>Kikipsigis</b> <i>mochari</i> <i>wotit</i> <i>netit</i> <i>lapit</i> <i>atmiten</i>	<b>Kiswahili</b> mochari wodi chandarua maabara laza

Kutokana na mifano hii, ilibainika pia ya kwamba ukopaji wakati mwingine huchukua ufupisho wa neno kwa mfano neno la Kiingereza ‘*laboratory*’ kutohozwa kuwa *lapit*.

### 5.1.3 Uwanja wa elimu

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (1948), elimu ni haki ya kimsingi ya kila mtu duniani. Hali ilivyo nchini Kenya ni kwamba kila Mkenya sharti apate elimu ya msingi (chekechea, msingi na upili) (RoK, 2010). Ili kulitimiza lengo hili, serikali ya

Kenya imehakikisha kuwa elimu inatolewa bila malipo katika shule za msingi tangu mwaka wa 2003, na katika shule za upili za kutwa tangu 2008 (RoK, 2008).

Kwa kuwa elimu ya kisasa ililetwa na wamishenari na wakoloni Waingereza, vifaa vya kufundishia havikuwepo katika utamaduni wa Kikipsigis. Wageni hawa ndio walioleta utamaduni wa kusoma na kuandika nchini Kenya. Vinginevyo, mfumo wa elimu wa Wakipsigis ulijumuisha mafunzo ya nyumbani hasa kupitia sherehe za tohara. Hali ilibadilika nchini Kenya elimu ya kizungu ilipoingia. Hivyo basi jamii mbalimbali ikiwemo jamii ya Wakipsigis walikopa msamiati katika sekta hii kutoka Kiswahili na Kiingereza ili kurejelea dhana geni iliyotokana na elimu. Vifaa hivi ndivyo vinavyotumika katika elimu ya kisasa inayohusu kusoma, kuandika na hata kuchapisha. Ingawa Wakipsigis walikuwa na elimu yao ya kitamaduni, vifaa vya kisasa kama vile kalamu, tarakilishi na hata vitabu havikuwepo; elimu ilipitishwa tu kimaongezi au kupitia kwa simulizi mbalimbali kama inavyodhihirika kupitia kwa mifano ifuatayo:

<b>3. (a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	mwalimu	<i>mwalimuyot</i>	
	tarehe	<i>tarigit</i>	
	kalamu	<i>kilamit</i>	
	masomo	<i>somanet</i>	
	karatasi	<i>kartasit</i>	
	hesabu	<i>esapuuk</i>	
<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	book	<i>puguit</i>	kitabu
	project	<i>prohekt</i>	mradi
	test	<i>testi</i>	mtihani
	nursery	<i>nasaret</i>	chekeche
	rubber	<i>rapait</i>	kifutio
	diploma	<i>tiploma</i>	stashahada

#### 5.1.4 Uwanja wa vifaa vya nyumbani

Vifaa vinavyotumiwa na wanajamii huweza kudhihirisha utamaduni wao. Hapa, kifaa kina maaana ya kitu au chombo kinachotumika katika kutekeleza kazi au kusudi fulani katika mazingira ya nyumbani. Kwa mfano, kifaa kinachoitwa *sotet* (kibuyu cha kuhifadhi maziwa) huhusishwa na jamii ya Wakalenjin nchini Kenya jinsi ambavyo mnazi unahusishwa na jamii ya Waswahili. Jamii moja inapoingiliana au kutagusana na jamii nyingine, huweza kuathiriana kwa njia mbalimbali na hutokea mabadiliko mbalimbali katika kuathiriana huko. Mabadiliko haya yanaweza kubainika kupitia kwa lugha inapotumika kurejelea vifaa vya kigeni vilivyoingizwa katika jamii. Mathalan, vifaa vinavyotumika nyumbani huweza kubainisha athari tofauti tofauti ambazo jamii moja hupata kutokana na kuingiliana na jamii nyingine.

Data ya utafiti huu, ilibainisha kwamba baada ya kuja kwa wakoloni (Waingereza), kumetokea mabadiliko katika jamii ambapo utamaduni wa Uingereza umeathiri pakubwa utamaduni wa Wakenya kupitia elimu, utandawazi na hata dini. Wakipsigis kwa mfano, wamekumbatia usasa ulioletwa na utamaduni huo wa kigeni pamoja na vifaa vyao. Kwa mfano, kuna matumizi ya kibuyu cha plastiki ili kuhifadhi maziwa badala ya kibuyu cha zamani (*sotet*). Vilevile usasa umeleta matumizi ya “kitanda” na “godoro” kama vifaa vya kulalia. Kabla ya majilio ya vifaa hivi vya kisasa, Wakipsigis walitumia aina ya kitanda kilichotengenezwa kwa kutumia udongo kilichoitwa *kitogit* na *muito* (ngozi ya ng’ombe) kama godoro. Kutokana na hali hii, Kikipsigis kimejazimika kukopa msamiati wa lugha nyingine ili kurejelea dhana hizi za kigeni. Kwa mfano:-

<b>4. (a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	kitanda	<i>kitandet</i>	
	sahani	<i>saniit</i>	
	kikombe	<i>kigombet</i>	
	chupa	<i>chupoit</i>	
	kioo	<i>kioyit</i>	
<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	thermos	<i>tamosit</i>	chupa ya chai
	glass	<i>kilasit</i>	gilasi
	stool	<i>stulit</i>	kiti kidogo
	carpet	<i>kapetit</i>	zulia
	bag	<i>pagit</i>	begi

Hata hivyo, ilibainika kwamba ingawa baadhi ya vifaa hivi vililetwa na Waingereza, Kikipsigis pia kilikopa baadhi ya misamiati kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano msamiati *kitandet* kimekopwa kutoka kwa msamiati wa Kiswahili. Hali hii inadhihirisha kwamba ukopaji wa msamiati kutoka Kiingereza katika Kikipsigis hausababishwi na hali ya Kiingereza kuwa na hadhi ya juu kuliko Kiswahili na lugha nyinginezo za Kiafrika.

### 5.1.5 Uwanja wa siasa

Jamii ya Wakipsigis tangu zamani ilikuwa na mfumo wake wa uongozi. Waliishi katika makundi ya kijamii yaliyojulikana kama ‘*kokwotinwek*’ (*kokwet* katika umoja) ambapo waliongozwa na viongozi waliochaguliwa na wazee. Viongozi hao walitoa mwelekeo katika jamii na kusuluhisha mizozano ya kifamilia, urithi miongoni mwa masuala mengineo. Hata hivyo, majilio ya Waingereza katika karne ya kumi na tisa yalileta mitawanyiko katika jamii hii kwani walowezi walinyakua mashamba mengi ya Wakipsigis katika maeneo ya Kericho, Sotik na Bomet.

Waingereza hao walileta mabadiliko katika jamii kupitia elimu, sayansi na teknolojia na hata utandawazi. Mabadiliko haya yaliathiri uongozi katika jamii mbalimbali nchini ikiwemo jamii ya Wakipsigis. Kutokana na misamiati iliyochunguzwa katika

sekta hii, ilibainika kwamba Kikipsigis kimekopa msamiati katika sekta hii ili kurejelea dhana geni ambayo haikuwepo katika jamii ya wakipsigis jinsi ilivyobainika katika mifano ifuatayo:-

5. (a)	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	chama	<i>chamait</i>	
	kura	<i>kurayat</i>	
	serikali	<i>serkalit</i>	
	bendera	<i>penderet</i>	
	askari	<i>asigorindet</i>	
	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	referendum	<i>reparendum</i>	kura ya maoni
	minister	<i>ministayat</i>	waziri
	parliament	<i>paliamen</i>	bunge
	ward	<i>wotit</i>	kata

### 5.1.6 Uwanja wa dini

Wakipsigis walikuwa na imani zao za kidini tangu jadi. Kwa mujibu wa Sambu (2007), Wakalenjin walimwabudu Mungu wao aliyerejelewa kama 'Asis'. Maabadi yao yalikuwa milima, misitu au chini ya mti. Palikuwepo na misamiati maalum, kama vile *saet* (maombi), *Asis* (Mungu), *tengekto* (dhambi), *chamyet* (upendo), *kaperuret* (Baraka) na kadhalika. Misamiati hii iliakisi utamaduni wa jadi wa Wakipsigis ambao uliathiriwa na dini ya Kikristo iliyoletwa na Wamishenari.

Kwa kuwa dini ni sehemu ya utamaduni wa jamii, basi tunaweza kubainisha namna imani za kidini za Wakipsigis zimekumbwa na mabadiliko kutokana na dini mpya ya ukristo pamoja na msamiati mkopo kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa mfano, dhana ya Yesu Kristo imetokana na majilio ya dini ya Kikristo ambayo iliibua misamiati mingine iliyoingizwa katika utamaduni wa Wakipsigis:

6. (a)	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	kanisa	<i>kaniset</i>	
	ubatizo	<i>kapatisanet</i>	
	padre	<i>potiryot</i>	
	msalaba	<i>msalapet</i>	
	Yesu	<i>cheiso</i>	
	hekalu	<i>egalut</i>	
	bibilia	<i>bukuit ne tilil</i>	
	(b)	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b> <b>Kiswahili</b>
		Christians	<i>kristianik</i> wakristo
		reverend	<i>reparen</i> padre
		Jehovah	<i>cheopo</i> Mungu

### 5.1.7 Uwanja wa uchumi na biashara

Uchumi ni sayansi ya uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa bidhaa. Ununuzi na uuzaji wa bidhaa, yaani biashara huchangia uchumi wa nchi. Uchumi wa nchi yoyote una mchango mkubwa katika taasisi mbalimbali za jamii. Hii ni kwa sababu nchi inapokuwa na nguvu kiuchumi, basi wanajamii wana uwezo wa kujitegemea. Zamani kabla ya kuja kwa Waingereza nchini Kenya, jamii mbalimbali zilikuwa na mifumo yao ya kibiashara. Kwa mfano, Wakipsigis walibadilishana bidhaa na jamii jirani ya Wakikuyu waliopakana nao katika sehemu za Molo. Katika ubadilishanaji huu, wakipsigis walibadilisha mahindi kwa viazi kutoka kwa Wakikuyu. Kwa hivyo jamii ya Wakipsigis kama ilivyokuwa jamii nyinginezo nchini ilikuwa na mifumo yake ya kuendesha biashara.

Hata hivyo, uvumbuzi wa pesa kama njia ya kubadilishana bidhaa, umeleta mabadiliko katika sekta ya biashara. Biashara imejengeka kutoka kwa kiwango ya kijamii hadi kimataifa. Hali hii imechangia pakubwa lugha ya Kikipsigis kukopa msamiati kutoka Kiswahili na Kiingereza. Uchanganuzi wa data ulibainisha kwamba



Kikipsigis kimekopa msamiati katika uwanja huu ili kurejelea dhana geni ambazo hazikuwepo katika utamaduni wake jinsi inavyobainika katika (8):-

7. (a)	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	thumni	<i>sumonit</i>	
	thelathini	<i>salasini</i>	
	gharama	<i>karamait</i>	
	bei	<i>peit</i>	
	elfu	<i>elipuut</i>	
	sabini	<i>sapini</i>	
	tisini	<i>tisaini</i>	
	(b) <b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	shares	<i>syecit</i>	hisa
	dollar	<i>tolait</i>	dola
	stamp	<i>stamput</i>	stempu
	fine	<i>pain</i>	faini

### 5.1.8 Uwanja wa ajira/ kazi

Katika utamaduni wa Wakipsigis, mzee alipewa hadhi na heshima kwa kutegemea wingi wa watoto wake. Watoto wengi walithaminiwa kutokana na manufaa yao katika utekelezaji wa majukumu nyumbani. Vilevile, watoto wa kike walithaminiwa kwa sababu ya kuolewa na kuleta mahari. Kwa hivyo, katika jamii hii hapakuwepo na vijakazi au vibarua ila watoto waliwasaidia wazazi katika kufanya kazi nyumbani kama vile ukulima na ufugaji wa mifugo bila malipo. Vilevile katika jamii watu mbalimbali walishirikiana kwa pamoja kama jamii katika kufanya kazi kama vile kulima shamba bila malipo yoyote.

Hata hivyo, mabadiliko katika jamii yaliyoletwa na elimu na usasa, yamewalazimu Wakipsigis kukumbatia elimu kwa ajili ya kupata ajira baada ya kufuzu. Kutokana na hali hii, lugha ya Kikipsigis imelazimika kukopa msamiati ili kurejelea dhana geni

kuhusiana na ajira ambazo hazikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

8. (a)	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	wakili	<i>ogilyot</i>	
	mshahara	<i>musyara</i>	
	kazi	<i>kasit</i>	
	faida	<i>paita</i>	
	fundi	<i>pundiyot</i>	
	mgomo	<i>komanet</i>	
	(b)	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>
		director	<i>tairktayat</i>
		manager	<i>menechayat</i>
			<b>Kiswahili</b>
			mkurugenzi
			meneja

### 5.1.9 Uwanja wa vyakula na vinywaji

Uwanja wa vyakula, vinywaji na viungo vya vyakula ni miongoni mwa nyanja ambazo zimekumbwa na mabadiliko mengi kutokana na maendeleo katika sayansi na teknolojia (Wamalwa, 1997). Kwa sasa, kunavyo vyakula na vinywaji ambavyo vililetwa na wageni humu nchini kama vile mchele, ndengu, soda, sharubati na kadhalika. Vyakula hivi pamoja na vinywaji vimetufikia nchini Kenya kutokana na uwezo wa kuvisafirisha kutoka nchi za ng'ambo. Pia kutokana na uvumbuzi wa njia za kisasa za kilimo. Vilevile, uwezo wa kielimu umewawezesha wasomi nchini kuviandaa baadhi ya vyakula na vinywaji hivyo humu nchini. Kwa hivyo, Kikipsigis kimekopa msamiati katika uwanja huu ili kurejelea dhana geni katika utamaduni wa wakipsigis jinsi inavyodhihirika kupitia mifano ifuatayo;

<b>10 (a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	mchele	<i>muchelek</i>	
	chumvi	<i>chumbik</i>	
	mkate	<i>magatiat</i>	
	chai	<i>chaik</i>	
	machungwa	<i>machungwat</i>	
	soda	<i>sota</i>	
	mandazi	<i>mandasinik</i>	
	<b>(b) Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	<i>lunch</i>	<i>lunchi</i>	chamcha
	<i>soup</i>	<i>supu</i>	supu
	<i>supper</i>	<i>sapa</i>	chajio
	<i>Fry</i>	<i>isus</i>	karanga

#### 5.1.10 Uwanja wa kilimo

Jamii ya Wakipsigis tangu zamani imekuwa ya wafugaji na kutokana na mabadiliko katika jamii, walianza ukulima huku wakiendeleza ufugaji wa mifugo mbalimbali wakiwemo ng'ombe, kondoo na mbuzi. Jamii hii inapatikana katika maeneo yenye rotuba katika mkoa wa bonde la ufa hasa katika sehemu za Kericho, Litein na Bomet jinsi ilivyoelezwa katika sura ya kwanza. Kwa hivyo jamii ya wakipsigis huthamini sana sekta hii ya kilimo.

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi nchini Kenya. Kinachangia asilimia 51 kila mwaka ya mauzo ya ndani nchini na vilevile asilimia 65 ya mauzo katika nchi za nje na zaidi ya asilimia 70 ya ajira katika sehemu za mashambani, mbali na kuchangia asilimia 18 ya ajira katika sehemu za mijini (RoK, 2012). Kwa hivyo, sekta ya kilimo ni sehemu muhimu sana katika ukuaji wa uchumi nchini.

Hali hii hivyo basi ni dhihirisho kwamba sekta ya kilimo ni muhimu sio tu katika jamii ya wakipsigis bali katika nchini nzima ya Kenya. Kutokana na maendeleo na

mabadiliko kote ulimwenguni katika sekta hii ya kilimo, nchi ya Kenya vilevile haijaachwa nyuma na hivyo imekumbatia mabadiliko hayo. Kwa mfano mbinu na vifaa vya ukulima na pembejeo mpya imeibuliwa ili kuboresha uzalishaji wa kilimo.

Mabadiliko haya yaliibua misamiati mipya ya kuvirejelea. Kwa mfano:

<b>11. (a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
	kilo	<i>kiloit</i>	
	panga	<i>panget</i>	
	uma	<i>umait</i>	
	reki	<i>regit</i>	
	mpera	<i>maperyat</i>	
	machungwa	<i>machungwat</i>	
<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	tractor	<i>terektait</i>	tingatinga
	phosphate	<i>pospet</i>	mbolea
	fertilizer	<i>patalaisa</i>	mbolea
	pump	<i>pambit</i>	pampu

#### 5.1.11 Uwanja wa mavazi

Kabla ya majilio ya wakoloni, Wakenya walikuwa na njia zao za kutengeneza mavazi yao ili kujisetiri. Mavazi hayo yalikuwa ya kipekee katika jamii mbalimbali na hivyo ilikuwa rahisi kutambua mtu fulani anatoka jamii gani kutokana na mavazi. Kwa mfano, Wamaasai ambao hadi sasa baadhi yao wanaendelea kudumisha njia zao za kuvaa, wangetambulika kwa urahisi kutokana na namna walivyovaa.

Mavazi ya kiutamaduni vilevile yaliakisi mazingira ya jamii husika. Kwa mfano, jamii ya Wakipsigis kwa sababu walikuwa wafugaji wa mifugo, walivalia ngozi (*muito*) ya ng'ombe, kondoo au mbuzi ili kujisetiri.

Wageni walipofika nchini, walileta mavazi ya utamaduni wao ambapo nguo za aina mbalimbali hushonwa kwa kutumia mashine. Kwa kuwa wakoloni hawakupenda mavazi ya kiutamaduni ya jamii mbalimbali ikiwemo Kikipsigis, waliwafanya kuyaacha na kukumbatia mavazi yao na hivyo kulazimika kukopa msamiati ili kurejelea dhana za mavazi ya kigeni jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

<b>12.</b>	<b>(a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	
		nguo	<i>ingoriet</i>	
		mshipi	<i>mosipiit</i>	
		kitambaa	<i>kitambaet</i>	
		rinda	<i>marindet</i>	
		leso	<i>lesoit</i>	
		kibeti	<i>kipetit</i>	
	<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
		blanket	<i>purangetit</i>	blanketi
		mattress	<i>matresit</i>	godoro
		towel	<i>towelit</i>	taulo
		jacket	<i>chegetit</i>	jaketi

#### 5.1.12 Uwanja wa usafiri na miundo misingi

Katika uwanja huu, takriban misamiati yote imekopwa ili kurejelea dhana za kigeni kwa sababu vifaa hivi vya usafiri havikuwepo nchini Kenya kabla ya majilio ya wageni na uvumbuzi wa kiteknolojia. Kwa sababu dhana hizi geni hazikuwa na istilahi ya kuzirejelea katika lugha pokezi, Kikipsigis kikalazimika kukopa msamiati kutoka lugha changizi. Mifano:

<b>13.</b>	<b>(a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
		ndege	<i>indegeit</i>
		gari	<i>karit</i>
		daraja	<i>tarachet</i>

pikipiki	<i>pigipigit</i>
barabara	<i>paraparet</i>
lami	<i>lamit/lam</i>
meli	<i>melit</i>

<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	bycle	<i>poskiliit</i>	baiskeli
	tractor	<i>terehtait</i>	trekta

### 5.1.13 Uwanja wa michezo

Uwanja huu ni mojawapo ya nyanja zinazowawezesha watu kutumia vipawa vyao katika michezo mbalimbali kama vile riadha, mpira wa magongo, mpira wa gofu, mpira wa kikapu, mpira wa meza, na kadhalika. Jamii ya Wakalenjin kwa jumla hujulikana sana katika riadha kwani washindi wengi wa riadha za nchini na hata katika mashindano ya kimataifa hutoka katika jamii hii. Wakipsigis wana msamiati asilia wa kurejelea riadha ambayo ni ‘*ng’waek*’. Michezo mingineyo mbali na riadha ililetwa nchini Kenya na Waingereza na kwa hivyo wasemaji wa Kikipsigis wamelazimika kukopa msamiati wa kigeni ili kurejelea dhana za michezo ambazo hazikuwepo katika utamaduni wao jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

<b>14.</b>	<b>(a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
		uwanja	<i>kiwanchet</i>
		mpira	<i>imbiret</i>
		mchezo	<i>mcheset</i>

<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>Kiswahili</b>
	points	<i>poindsiek</i>	alama
	medal	<i>mendilet</i>	nishani
	gold	<i>kolt</i>	dhahabu
	silver	<i>silpa</i>	fedha
	race	<i>resit</i>	mashindano

## 5.2 Ukopaji wa Kimtindo

Ukopaji wa aina hii huhusisha ukopaji wa msamiati kutoka lugha bebwa ilhali lugha solo una msamiati asilia. (Myers-Scotton (2002:41). Hali hii husababishwa na ubadilishaji msimbo. Tofauti na ukopaji wa kiutamaduni ambapo msamiati hukopwa ghafla ili kurejelea dhana geni na kujaza pengo la ukosefu wa msamiati, katika ukopaji huu, msamiati mkopo huingia katika lugha asilia kiutaratibu. Uchanganuzi ulibainisha kuwa, kutokana na elimu ya kimsingi, wanaujozi lugha wa Kikipsigis, Kiswahili na Kiingereza wameingiza misamiati ya lugha hizi bebwa katika Kikipsigis hata ingawa kuna msamiati asilia jinsi inavyobainika katika nyanja zifuatazo:

### 5.2.1 Uwanja wa vifaa vya kinyumbani

Utafiti ulibainisha kwamba Kikipsigis hukopa msamiati wa kigeni ili kurejelea vifaa vya kinyumbani ilhali kuna msamiati asilia wa Kikipsigis kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

<b>15.</b>	<b>(a) Kiswahili</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>msamiati asilia</b>
	mlango	<i>mlangoit</i>	<i>kurget</i>
	kitanda	<i>kitandet</i>	<i>kitogit</i>
	kifuniko	<i>kipuniget</i>	<i>kereywot</i>
	<b>(b) Kiingereza</b>	<b>msamiato mkopo</b>	<b>msamiati asilia</b>
	stool	<i>stulit</i>	<i>ng'echeret</i>
	brush	<i>purasit</i>	<i>kipsitet</i>

Katika mifano hii, ilibainika kwamba ingawa Kikipsigis kina msamiati wa kiasili wa kurejelea dhana hizi, wanatumia msamiati uliotoholewa kutoka Kiswahili na Kiingereza. Wanaujozi lugha ndio huingiza misamiati hii mikopo katika Kikipsigis, baada ya matumizi ya muda, inakubalika katika jumuiya lugha ya Wakipsigis na hivyo hata wale ambao hawana elimu wanaweza kuitumia.

Ilibainika kuwa ukopaji wa aina hii hutokana na ubadilishaji msimbo ambapo wanaujozi lugha wanapendelea msamiati mkopo kuliko msamiati asilia kwa mfano msamiati *kipuniket* umekopwa kutoka Kiswahili ilhali neno la kiasili ni *kereywot*.

### 5.2.2 Uwanja wa siasa

Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka Kiswahili na Kiingereza katika uwanja huu ilhali kuna visawe katika Kikipsigis. Hii ni kwa sababu msamiati unaokopwa ni sahili na mfupi ukilinganishwa na kisawe chake cha kiasili. Kwa mfano:

16.	(a)	<b>Kiswahili</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>msamiati asilia</b>	
		uhuru	uuru	<i>katiagnatet</i>	
		rais	rais	<i>kandoindet</i>	<i>nebo emet</i>
	(b)	<b>Kiingereza</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>msamiati asilia</b>	<b>Kiswahili</b>
		<i>chief</i>	chip	<i>kirwogindet</i>	chifu
		<i>youths</i>	yuts	<i>parnotik</i>	vijana

Mifano hii inabainisha kwamba wanaujozi lugha wa Kiingereza, Kiswahili na Kikipsigis wanapotaka kujieleza kwa urahisi hutumia msamiati uliokopwa badala ya msamiati asilia. Hii ni kwa sababu maneno haya mkopo ni mafupi kwani yana silabi chache yakilinganishwa na visawe vyao katika Kikipsigis. Kwa mfano neno ‘uuru’ lina silabi tatu ‘u-u-ru’ kwa hivyo, ni rahisi kutamkwa likilinganishwa na kisawe chake katika lugha asilia ‘ka-ti-ag-na-tet’ lililo na silabi tano. Hivyo basi ni rahisi kutamka neno ‘uuru’ kuliko ‘katiagnatet’ na hivi ndivyo hali ilivyo katika mifano mingine iliyotolewa. Myers-Scotton (kama hapo juu) anaeleza kuwa lugha huweza kukopa msamiati hata ikiwa na msamiati asilia wakati ambapo maneno mkopo ni mafupi. Anatoa mfano wa lugha ya Shona ambayo imekopa msamiati wa Kiingereza unaorejelea takwimu ilhali ina msamiati wa kiasili. Anaeleza kuwa msamiati mkopo hupendelewa kwa kuwa ni mfupi.



### 5.2.3 Uwanja wa mavazi

Utafiti huu ulibainisha kwamba wakati mwingine Kikipsigis hukopa mamiati ilhali imebuni msamiati asilia wa kurejela dhana za kimavazi ambazo hazikuwepo katika utamaduni wake. Kwa mfano:

<b>17.</b>	<b>(a)</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>Kikipsigis asilia</b>	
		leso	lesoit	anget	
		kofia	kopiet	kiroisit	
		kichanuo	kichanuet	kipsunuwet	
	<b>(b)</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>Kikipsigis asilia</b>	<b>Kiswahili</b>
		Sweater	swetait	chosit	sweta
		Mattress	matresit	mutoit	godoro

Hali hii inasababishwa na haja ya wasemaji wa Kikipsigis kutaka kujinasibisha kihadhi na lugha bebwa iliyo na hadhi ya juu.

### 5.3 Ukopaji wa Msamiati Kukidhi Haja ya Kutumia Msamiati Mahususi

Utafiti huu ulibainisha kwamba Kikipsigis hukopa msamiati ili kujaza pengo la ukosefu wa msamiati mahususi jinsi navyodhirika katika nyanja zifuatazo:

#### 5.3.1 Uwanja wa kidini

Ilibainika kwamba Kikipsigis kimekopa msamiati katika uwanja huu wa kidini ili kutimiza haja ya kutumia neno mahususi badala ya kutumia maelezo marefu. Kwa mfano:

<b>18.</b>	<b>(a)</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>Kiswahili</b>
		<i>kap korosut</i>	kaniset	kanisa
		<i>kechut beek asi kotililin tamirmiriet ne tilil</i>	kapatisanet	ubatizo
		<i>betut ne kigisiche laitoriat</i>	krismas	krismasi
		<i>betut ab otisyet</i>	sapato	sabato

<b>b) Kikipsigis</b>	<b>msamiati mkopo</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>bik che sigunotin</i>	kristianik	Christians	wakristo
<i>chito ne lipwop</i>	pastayat	pastor	mhubiri

### 5.3.2 Uwanja wa vyakula na vinywaji

Katika uwanja huu vilevile, Kikipsigis kimekopa msamiati mahususi jinsi inavyobainika katika mifano ifuatayo:

<b>19.</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>msamiati asila</b>
	supper	sapa	omitwogik chepo lang'at
	lunch	lanchi	omitwogik chepo peet

Mifano hii inadhihirisha kwamba Kikipsigis hakina msamiati mahususi wa kurejelea dhana hizo, hivyo basi kimekopa msamiati ili kujaza pengo hilo.

### 5.3.3 Uwanja wa msamiati wa kijumla

Katika uwanja huu Kikipsigis kimekopa mifano ifuatayo:

<b>20.</b>	<b>(a) Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>msamiati asilia katika Kikipsigis</b>
	scheme	sigiim	emet ne kimenye chumbek
	<b>(b) Kiingereza</b>	<b>Kikipsigis</b>	<b>msamiati mkopo</b>
	wiki	wigit	kasartab betusiek tisap

Neno *wiki* limekopwa kama '*wigit*' ilhali kuna kisawe chake '*kasartab betusiek tisap*' kwa kuwa Kikipsigis hakina neno moja la kurejelea dhana hii. Hivyo ndivyo hali ilivyo katika msamiati '*scheme*' ambao umekopwa kama '*sigiim*'.

#### **5.4 Ukopaji wa Msamiati ili Kuondoa Utata wa Kimaana**

Ili kuondoa utata wa kimaana baina ya maneno yanayorejelea dhana zinazokaribiana kimaana, Kikipsigis hukopa msamiati kutoka Kiswahili na Kiingereza ili kutofautisha maana hizo. Hali hii hudhihirika kupitia mifano katika njanya zifuatazo:

##### **5.4.1 Uwanja wa afya na matibabu**

Uchanganuzi wa data ulibainisha kwamba Kikipsigis kimekopa baadhi ya msamiati ili kuondoa utata wa maana. Kwa mfano, msamiati mkopo '*tagitari*' unatumika kumrejelea mtaalamu aliyehitimu katika elimu ya dawa, yaani tabibu wa dawa za kisasa ilhali msamiati asilia '*chepkericho*' unatumika kumrejelea tabibu wa dawa za kienyeji.

##### **5.4.2 Uwanja wa mavazi**

Tulibainisha kwamba wakati mwingine Kikipsigis hukopa msamiati ili kutofautisha maana katika maneno yaliyo na maana zaidi ya moja. Kwa mfano neno '*anget*' lina maana kadhaa: lesu, pazia, shiti au kitambaa cha kupanguza makamasi. Kwa hivyo,, ili kutofautisha maana baina ya dhana hizi, wasemaji wa Kikipsigis hutumia msamiati mkopo '*lesoit*' kwa maana ya lesu, '*ankachip*' kwa maana ya kitambaa cha kupangusia makamasi, '*sitit*' kwa maana ya shiti na '*pasyait*' kwa maana ya pazia.

##### **5.4.3 Uwanja wa msamiati wa kijumla**

Katika mfano wa '*forest*', tunaona kwamba Kikipsigis kimekopa msamiati '*porosti*' ilhali kina msamiati wa kiasili '*osnet*'. Uchanganuzi wetu ulibainisha kwamba wasemaji wa Kikipsigis wanatumia msamiati huu '*porosti*' kurejelea mahali palipo na miti mingi iliyopandwa ilhali neno la kiasili '*osnet*' linatumika kurejelea mahali penye vichaka na miti ya kiasili isiyopandwa. Kwa hivyo Kikipsigis kimekopa msamiati ili kutofutisha baina ya dhana hizo mbili zinazokaribiana kimaana.

## 5.5 Ukopaji wa Msamiati ili Kurahisisha Mawasiliano

### 5.5.1 Uwanja wa uchumi na biashara

Baadhi ya misamiati iliyokopwa katika uwanja huu imebainisha kwamba wasemaji wa lugha hii wamekopa msamiati ili kutimiza haja ya kutaka kujieleza kwa haraka na kwa urahisi iwezekanavyo. Hali hii imebainika kupitia tarakimu ambapo Kikipsigis kimekopa msamiati wa Kiswahili ilhali kina msamiati asilia wa kurejelea tarakimu hizo. Kwa mfano;

<b>21.(a) Kiswahili</b>	<b>Msamiati mkopo</b>	<b>Msamiati asilia</b>
sitini	sitini	tamanwogik lo
sabini	sapini	tamanwogik tisap
themanini	tamanini	tamanwogik sisit
tisini	tisaini	tamanwogik sogol

Katika kuangazia tarakimu asilia katika Kikipsigis, tunapata kwamba kumi, ishirini, thelathini, arobaini, hamsini na mia zinarejelewa kwa msamiati mahususi ilhali sitini, sabini, themanini na tisini hazina msamiati mahususi na hivyo hutajwa kwa maelezo kama inavyobainika ifuatavyo:

<b>(b) Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis asilia</b>	<b>msamiati mkopo</b>
Kumi	<i>taman</i>	-
ishirini	<i>tiptem</i>	-
thelathini	<i>sosom</i>	salasini
arobaini	<i>artam</i>	-
hamsini	<i>konom</i>	-
sitini	<i>tamanwogik lo</i>	sitini
sabini	<i>tamanwogik tisap</i>	sapini
themanini	<i>tamanwogik sisit</i>	tamanini
tisini	<i>tamanwogik sogol</i>	tisaini
mia	<i>pogol</i>	-

Tunapata kwamba Kikipsigis kimekopa msamiati wa kurejelea tarakimu zinazorejelewa kwa kutumia maelezo yaani (tamanwogik lo, tamanwogik tisap, tamanwogik sisit, tamanwogik sogol) jinsi inavyobainika hapo juu ili kurahisisha mawasiliano. Hivi kwamba badala ya kusema “tamanwogik tisap” msemaji anajieleza kwa urahisi na kwa haraka kwa kutumia msamiati mkopo “sapini” na hivyo ndivyo hali ilivyo katika sitini, themanini na tisini.

## 5.6 Ukopaji wa Kidaraja

Ukopaji wa kidaraja hurejelea hali ambapo lugha solo hukupa msamiati wa lugha fulani kupitia lugha nyingine. Utafiti huu ulidhihirisha kwamba Kikipsigis kimekopa misamiati ya Kiingereza kupitia kwa lugha ya Kiswahili jinsi inavyodhihirika katika mifano kutoka nyanja zifuatazo:

### 5.6.1 Uwanja wa sayansi na teknolojia

Katika uwanja huu, mifano ifuatayo inadhihirisha ukopaji wa aina hii:

22.	<b>Kiingereza</b>		<b>Kiswahili</b>		<b>Kikipsigis</b>
	computer	→	kompyuta	→	<i>kombyuta</i>
	company	→	kampuni	→	<i>kombunit</i>
	gazette	→	gazeti	→	<i>kasetit</i>
	team	→	timu	→	<i>timit</i>
	case	→	kesi	→	<i>kesit</i>
	report	→	ripoti	→	<i>ripotit</i>
	licensce	→	lesheni	→	<i>lesyenit</i>
	bank	→	benki	→	<i>pengit</i>

Hali hii inatokana na dhana kwamba Kiingereza ni lugha ya kimataifa inayochukuliwa kuwa ya kitaaluma. Kwa hivyo Wakipsigis hawajatangamana sana na wasemaji wa Kiingereza jinsi wanavyofanya na wasemaji wa Kiswahili ambayo ni

lugha ya kiafrika na vilevile lugha ya kitaifa. Asilimia kubwa ya msamiati wa kisayansi ililetwa na wasemaii wa Kiingereza (Waingereza) nchini Kenya.

### 5.6.2 Uwanja wa elimu

Uwanja huu vilevile una msamiati ambao umekopwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza kupitia kwa lugha ya Kiswahili. Hii inadhihirika kupitia mifano ifuatayo;

23.	<b>Kiingereza</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
	week	wiki	wigit
	professor	professa	propesayat
	report	ripoti	ripotit
	degree	digrii	tigirii

### 5.6.3 Uwanja wa uchumi na biashara

24.	<b>Kiingereza</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>msamiati mkopo</b>
	bank	benki	pengit
	shilling	shilingi	silingit
	billion	bilioni	pilionit
	note	noti	notit
	million	milioni	milionit

### 5.6.4 Uwanja wa ajira/ kazi

Mifano ya misamiati katika uwanja huu ni kama ifuatayo;

25.	<b>Kiingereza</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kikipsigis</b>
	driver	dereva	inderepayat
	officer	afisa	opisayat
	police	polisi	polisyot
	office	ofisi	opisit
	conductor	kondakta	kondaktayat

Hali hii huenda inasababishwa na uhusiano wa karibu baina ya lugha ya Kiswahili (kama lugha ya Kiafrika) na lugha ya Kikipsigis tofauti na hali ilivyo baina ya Kikipsigis na Kiingereza (kama lugha ya Waingereza).

### 5.6.5 Uwanja wa usafiri na miundo misingi

Uchunguzi ulibainisha kwamba misamiati ifuatayo imeingizwa katika Kikipsigis kupitia kwa Kiswahili:

26.	Kiingereza	Kiswahili	Kikipsigis
	lorry	lori	<i>lorit</i>
	bus	basit	<i>pasit</i>
	driver	dereva	<i>inderepa</i>
	helicopter	helikopta	<i>elikoptait</i>

### 5.6.6 Uwanja wa michezo

27.	Kiingereza	Kiswahili	Kikipsigis
	Team	timu	<i>timit</i>
	card	kadi	<i>katit</i>
	premier	primia	<i>primia</i>
	league	ligi	<i>ligit</i>
	match	mechi	<i>mechit</i>

Mifano hii inabainisha kwamba misamiati hii imeingizwa katika Kikipsigis kutoka Kiswahili. hii ni kutokana na mpangilio wa silabi ambapo tunaona kuwa mfuatano wa silabi katika msamiati uliokopwa umekaribia ule wa lugha ya Kiswahili kwa mfano: team (Kiingereza) → timu (Kiswahili) → timit (Kikipsigis).

## 5.7 Hitimisho

Katika sura hii tulilenga kubainisha sababu za kiisimujamii zinazochangia uingizwaji wa msamiati mkopo katika Kikipsigis. Ilibainika kwamba Kikipsigis hukopa msamiati ili kurejelea dhana geni. Aidha, Ilibainika kwamba Kikipsigis hukopa msamiati japo

kina msamiati asilia wa kurejelea dhana husika ili kuondoa utata wa kimaana baina ya maneno na kurahisisha mawasiliano.

Ilibainika pia kwamba Kikipsigis hukopa msamiati kutoka kwa Kiingereza kupitia kwa Kiswahili. Hali hii husababishwa na uhusiano wa karibu uliopo baina ya wasemaji wa Kikipsigis na wale wa Kiswahili. Uhusiano huu ni wa kimaeneo. Hii inatokana na sababu kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya, Kikipsigis nacho kikiwa lugha mojawapo nchini Kenya. Kwa hivyo, pana uhusiano wa karibu baina ya Kikipsigis na Kiswahili ikilinganishwa na Kikipsigis na Kiingereza amabayo ni ya kimataifa.

Kimsingi, ukopaji wa msamiati katika Kikipsigis una athari chanya kwa sababu hujaza pengo la hitaji la msamiati wa kurejelea dhana geni.



## SURA YA SITA

### MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.0. Utangulizi

Katika utafiti huu tulitambua na kuainisha msamiati mkopo kutoka Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis. Tulilinganisha pia mifumo ya kifonolojia ya lugha zote tatu ili kuweza kuelewa mchakato wa utohozi wa msamiati mkopo. Aidha tulibainisha michakato ya kimofonemiki yanayotumuka ili kuruhusu msamiati mkopo kuingizwa katika Kikipsigis na kisha kubainisha kategoria za kisarufi za msamiati mkopo kwa kuzingatia fonimu za umoja na wingi. Vilevile tulibainisha sababu zinazochangia ukopaji wa msamiati katika Kikipsigis. Matokeo ya utafiti huu ni yafuatayo:

#### 6.1. Matokeo

Katika kutambua na kuainisha msamiati mkopo katika Kikipsigis, ilibainika kuwa msamiati umekopwa katika nyanja mbalimbali kama vile uwanja wa sayansi na teknolojia, elimu, ajira, uchumi na biashara, siasa, usafiri na miundo misingi, mavazi, afya na vifaa vya nyumbani. Vilevile asilimia kubwa ya msamiati uliokopwa hurejelea dhana ambazo hazikuwepo katika utamaduni ya Wakipsigis kama vile dhana za kisayansi, kielimu, miundo misingi, mavazi na hata vifaa vya nyumbani vya kigeni.

Tasnifu imebainisha pia kwamba Kikipsigis kimekopa nomino zaidi ya aina nyingine ya maneno kwa sababu nomino hutumika sana katika mawasiliano semi au andishi kuliko aina nyingine ya maneno kama vile vitenzi au vielezi.

Kama ilivyobainika katika sura ya pili kwenye tasnifu, kuna tofauti za kimsingi: ya fonimu na miundo ya silabi baina ya mifumo ya kifonolojia ya lugha ya Kiingereza,

Kiswahili na Kikipsigis. Hivyo basi ni kutokana na tofauti hizi ambapo msamiati mkopo wa Kiingereza na Kiswahili hufanyiwa mabadiliko ya kimofonemiki ili kuufanya msamiati huo mkopo kukubalika katika mfumo wa kifonolojia wa Kikipsigis.

Katika kushughulikia mabadiliko ya kimofonemiki katika msamiati mkopo wa Kiingereza, utafiti ulibainisha kuwa Kikipsigis hufupisha irabu ndefu katika msamiati mkopo. Kwa mfano irabu /ɜ/ hufupishwa kuwa /a/ au /ɔ/ ilhali /u:/ hufupishwa kuwa /u/. Uchanganuzi ulionyesha pia kuwa irabu hizi ndefu hufupishwa kuwa zile irabu zinazokaribiana kimatamshi. Utafiti ulitambua vilevile kuwa Kikipsigis hakina irabu unganifu kwa hivyo irabu za aina hii husahilishwa ili zikubalike katika mfumo wa kifonolojia wa lugha hii. Kwa mfano: /eɪ/ → /ɛ/, /əv/ → /ɔ/, /aʊ/ → /a/ na /aɪ/ → /ai/. Irabu hizi unganifu zimesahilishwa kuwa zile zinazokaribiana kimatamshi. Utafiti ulitambua vilevile kuwa irabu tatu unganifu hutoholewa kupitia ama mchakato wa muungano wa irabu ambapo irabu mbili huungana na kuzua alofoni mpya ya fonimu husika kwa mfano: /Iəv/ → /iə/ au kupitia uyeyushaji ambapo irabu tatu unganifu hutoholewa kwa kuundwa kwa kiyeyusho kwa mfano /aIə/ → /aja/.

Clements na Keyser (1983) wakizungumzia miundo ya silabi, wanaeleza kuwa muundo wa silabi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa hivyo, katika kuangazia utohozi wa irabu katika msamiati wa Kiswahili, utafiti ulibainisha kuwa Kikipsigis hakiruhusu mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno hivyo basi hutohoa msamiati ulio na mfuatano wa konsonanti mwanzoni kwa kuchepeka irabu katikati ya konsonanti hizo kama ilivyo katika neno *mchele* linalotoholewa kuwa *muchelek*, *mkate* hutoholewa kuwa *magatiat*. Ilibainika vilevile kwamba katika msamiati unaoanza kwa fonimu /<sup>n</sup>g/ na /<sup>n</sup>d/, irabu huchopekwa mwanzoni mwa fonimu hizi kwa mfano: ndizi → indisiot, ndege → indegeit, ngazi → ingasit, nguo →

ingoriet. Mchakato mwingine uliobainika ni wa kuafikiana kwa irabu unaosababishwa na irabu iliyo mwishoni mwa msamiati ambapo ikiwa irabu /a/ hutokea mwishoni mwa msamiati mkopo, basi utohozi wake huchukua mofu /ait/ ilhali msamiati unaoishia kwa irabu /u/ au /ɔ/ huchukua mofu /oit/. Hata hivyo tulibainisha pia kwamba mvutano wa irabu hutokea wakati ambapo irabu zimetokea kwa kufuatana ilhali irabu moja ni ya juu na nyingine ni ya chini. Kwa mfano katika msamiati *kitanda*, jinsi ilivyoelezwa katika kuafikiana kwa irabu tungetarajia neno kitanda kutoholewa kuwa *kitandait* lakini tunapata *kitandet*. Hii ni kwa sababu ya mvutano wa irabu unaotokea kati ya irabu /a/ ambayo ni ya chini na irabu /i/ ambayo ni ya juu. kwa hivyo mvutano huu huleta sauti moja tofauti ambayo ni irabu /ɛ/ iliyo kati ya rabu /a/ na /i/. Aidha katika utohozi wa fonimu konsonanti, Kiswahili na Kiingereza hutumia michakato sawa: Kuimarika kwa konsonanti, kudhoofika kwa konsonanti, udondoshaji wa konsonanti na uchopezi wa konsonanti.

Katika kategoria za kisarufi za msamiati mkopo, tulibainisha makundi manne ambapo kikundi cha kwanza kilichukua mofimu [it] katika umoja na [inik] au [isiek] katika wingi, kikundi cha pili kilichukua mofu [oit] au [yot] katika umoja na [inik] katika wingi, katika kikundi cha tatu mofu [at] au [yat] katika umoja na [inik] au [aek]. Tulibainisha kwamba kikundi hiki cha tatu mofu ya umoja [yat] huchukua msamiati unaohusu binadamu kama vile *malaigayat*, *inderepayat*, *membayat*, *ministayat*. Kimsingi tulitambua kuwa iwapo msamiati mkopo una mofu /u/ au /i/ katika mzizi basi huchukua mofu /inik/ katika wingi ilhali ikiwa na irabu /a/, /ɔ/ au /e/ basi huchukua mofu /isiek/ katika wingi. Kwa mfano:

<b>Kiswahili</b>	<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>	<b>Kiingereza</b>	<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>
Chupa	chupait	chupainik	rubber	rapait	rapainik
Picha	pichait	pichainik			
Kazi	kasit	kasisiek	glass	kilasit	kilasisiek
Kilo	kiloit	kiloisiek	school	sugulit	sugulisiek
Tarehe	tarigit	tarigisiek	thermos	tamosit	tamosisiek

Katika utohozi wa msamiati mkopo kutoka Kiingereza ilibainika kuwa katika utohozi wa fonimu irabu michakato ifuatayo hutumika: ufupishaji wa irabu ndefu, usahilishaji wa irabu unganifu, muungano wa irabu na uyeyushaji. Kiswahili katika upande mwingine hutumia michakato ifuatayo: uchopezi wa irabu, kuafikiana kwa irabu, mvutano wa irabu, udondoshaji wa irabu na uyeyushaji.

Tukizingatia sababu za ukopaji, ilibainika kwamba Kikipsigis hukopa msamiati ili kurejelea dhana geni isiyokuwepo katika utamaduni wake kama vile msamiati wa kisayansi, elimu, mavazi na nyanja nyinginezo. Hata hivyo, utafiti ulionyesha kwamba Kikipsigis wakati mwingine hukopa msamiati hata kama kina msamiati wake wa kiasili kwa sababu msamiati mkopo ni sahili, mfupi na rahisi kutamkwa ukilinganishwa na ule wa kiasili wa Kikipsigis.

## **6.2. Hitimisho**

Kimsingi, tasnifu hii ilibainisha kwamba ukopaji wa msamiati ni jambo lisiloepukika katika mitagusano ya lugha kwani katika kutagusana kunatokea uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine.

Tukirejelea mabadiliko ya kimofonemiki katika msamiati mkopo, ilibainika kwamba msamiati mkopo hauingizwi tu katika lugha solo jinsi ilivyo katika lugha

bebwa ila hufuata kanuni za kifonolojia za lugha solo. Hivyo basi msamiati mkopo hubadilishwa ili ukubalike katika mfumo wa lugha husika.

Ilibainika pia kwamba, Kikipsigis kimekopa msamiati kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza bila kuzingatia kuwa Kiingereza kina hadhi ya juu kuliko Kiswahili

Kwa kuhitimisha, utafiti huu ulionyesha kwamba ukopaji wa msamiati hausababishi kudidimia kwa Kikipsigis ila huongeza msamiati katika dafina ya msamiati asilia ya Kikipsigis haswa misamiati ya kurejelea dhana geni kutoka tamaduni mbalimbali.

### 6.3. Mapendekezo

Tasnifu hii inapendekeza kuwa utafiti ufanywe kuhusu utohozi wa vitenzi, vivumushi na vielezi vilivyokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza au hata lugha nyingine za kiasia ambazo zimetagusana na Kikipsigis kama vile Kikuyu na Ekegusii. Hii ni kwa sababu katika ukusanyaji wa data ilibainika kuwa Kikipsigis kimekopa aina hizi za maneno ila utafiti huu ulijikita tu katika utohozi wa nomino. Utafiti wa aina hii itakuwa muhimu ili kuweka wazi namna Kikipsigis kinavyotohoa nomino na aina nyingine za maneno.

Utafiti huu ulibainisha alomofu za umoja na wingi katika msamiati mkopo ambapo mofu ya umoja **{-it}** huchukua mofu **{-inik au -isiek}** katika wingi, ilhali mofu **{-oit/ -yot}** ya umoja huchukua mofu **{-inik}** kisha mofu **{at/ -yat}** kuchukua mofu **{-inik au -aek}** katika wingi. Ni muhimu utafiti ufanywe kuhusu mofosintaksia wa msamiati mkopo katika Kikipsigis ili kubainisha namna lugha hii inavyoshughulikia msamiati mkopo katika sentensi

## MAREJELEO

- Asher, R.E., & Simpson, J.M.Y. (1994). *The Encyclopedia of Language and Linguistics*. Vols. 1 & 4. Oxford: Pergamon Press.
- Ashton, E.O. (1994). *Swahili Grammar*. Longman Green & Co. Ltd. London.
- Bright, W. (1997). Social Factors in Language Change. Katika Coulmas, F (Mhr.), *The Handbook of Sociolinguistics*. Cambridge: Blackwell Publishers Ltd.
- Bynon, T. (1977). *Historical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press
- Clements, G.N., & Keyser, S.J. (1983). *C.V. Phonology*. Cambridge Mass, MIT Press
- Crystal, D. (1997). *The Cambridge Encyclopedia of Language, 2<sup>nd</sup> edition* . Cambridge : Cambridge University Press
- Dorney, Z. (2007). *Research Methods in Applied Linguistics*. Oxford University Press. New York.
- Dzahene-Quarshie, J. (2010). English in Contact with Swahili: Enrichment or Threat? *Katika Journal of LETUNK 2010/4. 55-74*. Accra, Ghana
- Fromkin, V., & Rodman, R. (1988). *An Introduction to Language (fourth ed)*. USA: Harcourt Brace Jovanovich College Publishers
- Halliday, M.A. (1998). *Language as Socio-Semiotic: The Social Interpretation of Language and Meaning*. London: Edward Arnold
- Haugen, E. (1950). The Analysis of Linguistic Borrowing. *Katika Journal of Language 26:210-231*
- Heath, J. (2001). Borrowing. Katika Mesthrie, R. (Mhr.), *Concise Encyclopedia of Sociolinguistics*, Oxford: Elsevier Science Ltd: 432-442
- Iribemwangi, P.I., & Mukhwana A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd
- Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar Es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).
- Katamba, F. (1993). *Morphology*. London: macmillan publishers
- Kembo-Sure & Ogechi, N. O. (2006). Language planning and language reform in Kenya. Katika Kembo-Sure, S. Waitiki & N. O. Ogechi (Whr.), *Language Planning for Development in Africa. (UK. 37 – 54)*. Eldoret: Moi University Press.
- \_\_\_\_\_. (2009). *Linguistic Human Rights and the Language Policy in the Kenyan Education System*. Addis Ababa: OSSREA
- Kembo-Sure, (1993). Grammatical and Phonological Integration of English loanwords into Dholuo. *Katika Journal of multilingual & multicultural Development 14.4:329-344*

- LaCharite, D., & Paradis, C. (2000). Phonological evidence for Bilingualism of Bilinguals. In: J. Jensen & G. Van Herk (Eds.), *Proceedings of the 2000 Annual Conference of 'The Canadian Linguistics Association'* Ottawa: Cahiers Linguistiques d'Ottawa.
- Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., & Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A synthesis in developments, research and literature*. Nairobi, Kenya Literature bureau
- McMahon, A. (1994). *Understanding Language Change*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mgullu, S.R. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longman Publishers. Nairobi
- Mohanan, K. (1986). *The Theory of Lexical Phonology*. Dordrecht: Riedel
- Myers-Scotton, C., & Jake, J.L. (2000). Testing the 4-M model: Introduction, katika *International Journal of Bilingualism*. 4. 1. March 2000
- Myers-Scotton, C. (2006). *Multiple Voices, An Introduction to Bilingualism*. Oxford: Blackwell Publishers.
- \_\_\_\_\_. (2002). *Contact Linguistics: Bilingual Encounters and Grammatical Outcomes*. New York, Oxford University Press
- \_\_\_\_\_. (1997). *Duelling languages: Grammatical Structure in Codeswitching (with a new Afterword)*. Oxford: Clarendon Press.
- \_\_\_\_\_. (1992). 'Codeswitching as a Mechanism in Deep Borrowing, Language Shift, and Language Death', in Matthias Brenzinger (Ed.), *Language Death, Factual and Theoretical Explorations with Special Reference to East Africa*, 31-58. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Nchimbi, A.S. (1979). "Mfumo wa Matamshi ya Fonimu za Kiswahili" katika *Journal of Baragumu*. 1. 2. 1979 Maseno University.
- Odhiambo, K., & Oduma, R. (2011). Morphophonemic Adaptation of English and Kiswahili Loanwords into Dholuo and Ateso. Katika Ogechi, N.O. (Ed.), *Themes in Language, Education & Development in Kenya*. Nsema Publishers
- Oduma, R. (2006). Phonological Adaptation of Loanwords in Ateso. Moi University. Unpublished Mphil, Thesis
- Ogechi, N.O. (2011). *Themes in Language, Education and Development in Kenya*. Nsema publishers
- Osama, A. na Wenzake (2004). An OT Approach to Loanword Adaptation in Cairene Arabic. *Kansa Working Papers in Linguistics* vol. 27: 1-19
- Paradis, C., & LaCharite, D. (1997). Preservation and Minimality in Loanword Adaptation. *Journal of Linguistics*. Vol. 33, No. 2: 379-430

- Polome, E. (1967). *A Handbook of Kiswahili Language*. Institute of African and Oriental Languages. London
- Roach, P. (2000). *English Phonetics and Phonology: A Practical Course*. Cambridge: Cambridge University Press
- RoK (2008). *The Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printer
- RoK (2010). *The Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printer
- Sambu, K. (2007). *The Kalenjin People's Egypt Origin Legend Revisited: Was Isis Asiis*: Longhorn Publishers. Nairobi.
- Sang, H.K., & Jerono, P. (2012). The Phonology of Loanwords in three Kalenjin Dialects. Katika Ogechi, N.O, Jane A. & Iribemwangi, P. (Whr). *The Harmonization and Standardization of Kenyan Languages*. Cape Town: CASAS
- Thomason, S.G., & Kauffman, S.K. (1976). Loanwords and the Borrowing Language's Pre-Borrowing Phonology. Katika Christie Jnr (Mhr) *Current Progress in Historical Linguistics*. New York: North Holland Publishing Company
- Towett, T. (1979). *A Study of Kalenjin Linguistics*. Kenya Literature Bureau. Nairobi].
- Walusimbi, L. (2002). The Influence of Foreign Languages on Ugandan Languages: A Case Study of borrowing in Luganda. Katika I. Rissum (Mhr.), *language in Contrast*. Bayreuth: African Studies Series
- Wamalwa, M.N. (1997). *Kusharabu kwa msamiati wa Kiswahili katika Kibukusu*. Moi University. Unpublished Mphil, Thesis
- Webb, V., & Kembo-Sure. (2000). *African Voices: An introduction to the language and linguistics of Africa*. Cape Town: Oxford University press.
- Whitefield, L.H. (1970). *Language: An Introduction*. Madison: University of Wisconsin Press
- Yule, G. (2006). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press



**VIAMBATISHO****Kiambatisho I: Barua**

Cherono Naomi Jescah,  
Moi University,  
P.O. BOX 3900,  
ELDORET  
30<sup>TH</sup> January, 2015

TO WHOM IT MAY CONCERN

Dear Sir/Madam,

**RE: INTRODUCTORY LETTER**

My name is Cherono Naomi Jescah, I am currently a Masters' student at Moi University, Department of Kiswahili and Other African Languages. I am carrying out research on loan words in Kipsigis from Kiswahili & English. My research title is **"MSAMIATI MKOPO KATIKA KIKIPSIGIS: UCHANGANUZI WA KIMOFOFONEMIKI NA KIISIMUJAMII"**

I am kindly requesting you to participate in this research by verifying if the words below are found in Kipsigis by using a tick (✓). Please check the spelling and make corrections where necessary.

For any questions or comments please contact me through e-mail: [jessname@gmail.com](mailto:jessname@gmail.com) or mobile number 0728734380.

Your time and assistance in this research is highly appreciated. I look forward to learning from you.

Yours sincerely

Cherono Naomi Jescah

SASS/PGK/04/13

**Kiambatisho II: Hojaji**

**MSAMIATI MKOPO KATIKA KIKIPSIGIS: UCHANGANUZI WA  
KIMOFOFONEMIKI NA KIISIMUJAMII**

Kindly fill in the questionnaire by ticking (✓) the appropriate response. For confidentiality please do not indicate your name or the name of your institution anywhere in this questionnaire.

**PERSONAL INFORMATION**

1. Gender: Female [  ] Male [  ]
2. Age bracket (years)  
35 -39 [  ] 40-44 [  ] 45-49 [  ] 50-54 [  ] 55-59[  ]
3. Highest level of training  
PhD [  ] Bachelors [  ] Diploma [  ] Certificate [  ]
4. Are you a native speaker of Kipsigis? Yes [  ] No [  ]

**Msamiati Wa Kikipsigis**

	<b>WORD</b>	<b>TICK</b>	<b>CORRECT SPELLING</b>
1.	Esapuuk		
2.	Taonit		
3.	Katipayat		
4.	Mochari		
5.	Nasaret		
6.	Bukuit		
7.	Kitabuut		
8.	Simoit		
9.	Nchuguuk		
10.	Porosti		
11.	Piasinik		
12.	Sikiim		
13.	Nyanyiik		
14.	Sukulit		
15.	Elipuut		
16.	Ministayaat		
17.	Asikarindet		
18.	Islamiek		
19.	Meset		
20.	Testi		
21.	Pichait		
22.	Klasit		
23.	Mucheleek		
24.	Tairektayat		
25.	Kasiit		
26.	Rearendum		
27.	Takigaisiek		
28.	Pilotit		
29.	Ndekeit		
30.	Reparen		
31.	Kariit		
32.	Mendilet		
33.	Chamait		
34.	Timit		
35.	Serkaliit		
36.	Koundy		
37.	Tarachet		
38.	Spikayat		
39.	Kiwancheet		